Nipashe
Jumatatu Januari 6, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580120
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## Mtoto afa kwa kugongeshwa kichwa kwenye gogo akicheza

UKURASA 3




UKURASA 13

# CAG afichua zilipo tril.1.46/- mikopo kwa wanafunzi



• **Mashirika** 11 taabani, 14 yachechemea, NIC yaelemewa madeni...*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**TCRA YAFICHUA UTAPELI MPYA FEDHA MITANDAONI**

WANANCHI wametakiwa kutokutoa namba za siri za huduma za kifedha...

## Abiria wasota usafiri mabasi mikoani

UKURASA 3




Hali ya usafiri katika kituo kikuu cha mabasi cha Moshi Mjini bado ni tete, kutokana na idadi kubwa ya abiria wanaorudi mikoani pamoja na wanafunzi wanaorejea shuleni. **PICHA: MARY MOSHA**






Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

## Homa ya uchaguzi 2020 yapanda CCM, Chadema

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA YAUMIA, YANGA KICHEKO UK.32 | **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# CAG afichua zilipo tril. 1.46/- mikopo wanafunzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

OFISI ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), imesema Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imeshindwa kuwapata wanufaika wa mikopo yenye thamani ya Sh. trilioni 1.46.

Kutokana na wanafaika hao kushindwa kurudisha mikopo kwa wakati, baadhi ya wanafunzi wapya na wanaoendelea na masomo wameshindwa kupata mikopo hiyo.

Hayo yamo kwenye toleo maalum la Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/18.

"Kutopatikana kwa wanufaika hao kunapunguza uwezo wa bodi kutoa mikopo kwa wanafunzi wapya na wanaoendelea," ilisema sehemu ya kitabu hicho katika ukurasa wa 42.

CAG alitoa mapendekezo kwa HESLB kushirikiana na taasisi nyingine na vyanzo vingine vya taarifa kuboresha kanzi data yake ili kuwatambua wanufaika wa mikopo ambao bado hawajatambulika.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma, kuhusu ukaguzi unaofanywa na ofisi yao, Mkaguzi kutoka Ofisi ya CAG, Henry Naiman, alisema eneo la mikopo ilibainika kuwa jambo hilo limekuwa kikwazo.

Alisema kutopatikana kwa wanufaika hao kumesababisha bodi hiyo kupunguza uwezo wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wapya na wale wanaoendelea.

"Ni vyema bodi hiyo ikashirikiana na taasisi nyingine lengo wanufaika wa mikopo wajulikane," alisisitiza Naiman katika kipengele hicho.

Mwishoni mwa mwezi Desemba, wanafunzi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ilitangaza mgomo kwa madai

INAENDELEA UK. 8

# Homa ya uchaguzi CCM, Chadema yapanda

**Na Waandishi Wetu**

UNAWEZA kusema sasa homa ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu imeanza kupanda ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Hali hiyo inatokana na kauli mbalimbali za viongozi wa vyama hivyo kuhusiana na uchaguzi huo. Baadhi ya kauli zinahusu kuonya makada, baadhi ya makada kutangaza majimbo wanayotarajia kugombea, wengine kuelekeza wanachama kuanza kuomba vibali kwa Jeshi la Polisi kuhusu mikutano ya kisisasa na wengine kutaka wabunge wao kutekeleza ilani yao ya uchaguzi.

WABUNGE CCM WABANWA ILANI

Chama Cha Mapinduzi (CCM), kimewataka wabunge kutekeleza ahadi zote walizoahidi wakati wa kampeni katika uchaguzi uliopita na kuongeza kasi ya utendaji kazi, ili kumaliza malalamiko yanayotolewa na wananchi ambao ndiyo waliowaweka madarakani.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Tanzania Bara, Rodrick Mpogolo, alitoa agizo hilo juzi alipokutana na wajumbe wa Jimbo la Singida Mjini na kupokea taarifa ya utekelezaji wa Mbunge Musa Sima, katika kipindi chake cha miaka minne.

"Nawaomba wabunge wote, tekelezeni ahadi zenu mlizoahidi kwenye kampeni, ili mjenge imani kwa wananchi, chama na serikali... tudumishe ushirikiano, hatuwezi kupata maendeleo bila ya kuwa na ushirikiano wa kutosha ndani yetu," alisema Mpogolo.

Alifafanua kuwa, CCM inachokitafuta hivi sasa ni maendeleo ya watu na kumtaka Mbunge Sima kuchapa kazi, kwa ajili ya kuwaletea wananchi wa Jimbo la Singida Mjini maendeleo.

Aliwataka watendaji wa serikali kuhakikisha wanamsaidia Rais John Magufuli, kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo mikubwa ya kimkakati ili kuwaletea wananchi maendeleo, na hivyo kuliwezesha taifa kusonga mbele.

Aliwapongeza wananchi wa Singida kwa ushiriki wao madhubuti wa kujiletea maendeleo, ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambayo mkoa huo ulikuwa nyuma na kuwa kati ya mikoa duni zaidi nchini.

Alisema hivi sasa hali hiyo haipo, kutokana na uwapo wa viashiria vya maendeleo, hususani nyumba nzuri za kisasa, tofauti na miaka ya nyuma ukipita kwenye barabara kuu ya Mwanza-Dar es Salaam kupitia Singida, nyumba nyingi zilizokuwapo ni za nyasi na tembe.

Akimkaribisha Naibu Katibu

INAENDELEA UK. 8


## TATHIMINI YA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA KIJAMII

### TAARIFA KUHUSU MRADI TARAJIWA WA DHAHABU WA NYAMULILIMA, KWA AJILI YA KAMPUNI YA GEITA GOLD MINING LIMITED, WILAYA YA GEITA, MKOA WA GEITA

Mradi tarajiwa wa uchimbaji wa dhahabu katika eneo la Nyamulilima upo ndani ya ukanda wa madini wa ziwa Victoria takribani kilometa 20 hadi 25 kwa njia ya barabara kutokea mji wa Geita. Mradi pendekezwa unamilikiwa na kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) ambayo ni kampuni tanzu ya AngloGold Ashanti. Mradi huu upo ndani ya leseni mahsusi ya uchimbaji madini yenye yaani ***Special Mining Licence (SML)*** namba 45/99 iliyotolewa Juni 1999. Sehemu ya leseni ulipo mradi ipo ndani ya kata Nyamwilolelwa, wilaya ya Geita, Mkoa wa Geita.

Mgodi wa Geita umekuwa ukifanya uchimbaji wa madini kwa kutumia njia ya mashimo ya wazi na uchimbaji wa chini ya ardhi an uchenjuaji kwa kutumia sayanadi. Hata hivyo, rasilimali ya dhahabu iliyobaki kwa mgodi wa Geita inaonekana kuisha mwishoni mwa mwaka 2020. Hivyo, kwa mgodi wa Geita kuendelea kutoa mchango muhimu katika uchumi wa Tanzania, utafiti ulisaidia kugundua maeneo mengine mbadala ndani ya leseni yenye madini. Maeneo ya Nyamlilima yamethibitishwa kuwa na ukanda wenye hifadhi ya dhahabu ambao utaweza kupatikana na kuingizwa katika uzalishaji kwa kupitia njia ya uchimbaji wa mashimo ya wazi na pengine uchimbaji wa chini ya ardhi hapo baadae.

Hifadhi ya madini ya dhahabu iliyopopo na inayopendekezwa kuchimbwa kutoka eneo la Nyamlilima ni miongoni miradi ya uchimbaji ambayo itasaidia kuendelea kuwepo kwa shughuli za uchimbaji zinazofanywa kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML)hata baada ya mwaka 2020. Ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi huu, tathmini ya athari za kimazingira na kijamii inahitajika kama ilivyoainishwa katika Sheria ya usimamizi wa mazingira, 2004 na Sheria ya Madini, 2010.

Pia ili kukidhi mahitaji ya sheria ya mazingira ya taifa na kuhakikisha shughuli zinaendana na viwango vinavyokubalika kimataifa kwa ajili ya usimamizi wa mazingira na mahitaji ya kijamii; kampuni ya GGML imeiteua kampuni ya ushauri iitwayo MTL kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii zinazoweza kutokana na mradii. Utafiti huo utachunguza faida pamoja na athari na kuelezea hatua zote mbadala zitakazotumika ili kuongeza faida na kupunguza athari.

Ili kufikia mahitaji ya kisheria ya ndani ya nchi na yale ya kimataifa katika kufanya utafiti huu wa athari za kimazingira na kijamii, majadiliano na wadau wanaohusika na mradi ni muhimu. Na hivyo tangazo hili linawakaribisha wadau wote wenye maslahi, ushauri au taarifa muhimu kuhusu athari zozote ama za kimazingira au kijamii kuhusiana na mradi huu kuwasiliana kwa simu au kwa kutoa mawazo kwa Msahuri Mwelekezi kupitia anuani ifuatayo:

**Mkurugenzi Mtendaji**
**MTL Consulting Company Limited,**
**Masaki, Nyumba namba 2,Kitalu 689,**
**S.L.P 77894, Barabara ya Sandvik**
**Dar es Salaam, Tanzania.**
**Tel./Fax: +255 22 2600594**
**Cellular: +255 (0) 767 360 225**
**Email: emasasila@mtlconsulting-tz.com**

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)**
**S.L.P 63154, Regent Estate Plot No. 29/30,**
**Dar es Salaam, Tanzania.**
**Tel: +255 22 2774889**
**Email: dg@nemc.or.tz**

215573802


# TCRA yafichua utapeli mpya wa fedha mitandaoni

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WANANCHI wametakiwa kutokutoa namba za siri za huduma za kifedha ikiwamo mitandao ya simu na akaunti za benki kwa baadhi ya watu wanaohusika na usajili wa laini za simu kwa njia ya alama za vidole.

Angalizo hilo limetolewa baada ya kuibuka kwa kundi la watu waliobuni mbinu mpya kwa kutumia fursa hiyo kufanya utapeli jijini Mwanza kwa kuwashawishi kuwa usajili wa laini za simu kwa alama za vidole kwa kutumia kitambulisho cha taifa unaendana na uhakiki wa akaunti ya benki ya mhusika.

Akizungumza katika kikao kazi cha kutoa taarifa ya hali ya mawasiliano Kanda ya Ziwa kilichowajumuisha viongozi wa Jeshi la Polisi wilaya za Ilemela na Nyamagana, Ofisa Usajili kutoka Mamlaka ya Taifa ya Vitambulisho (Nida), watoa huduma wa makampuni ya simu na wanahabari, Mkuu wa Mamalaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Ziwa, Francis Mihayo, alisema baada ya zoezi la usajili kuongezewa muda limeibuka kundi la vijana linaloingia mtaani kuwatapeli wananchi.

Aliongeza kuwa vijana hao wanakuwa wamevalia sare za watoa huduma kutoka kampuni za mitandao ya simu hupita majumbani, mitaani na sehemu za biashara na kuwalaghai baadhi ya wananchi kuwa usajili wa namba za simu kutumia alama za vidole unafanyika sambamba na uhakiki wa akaunti za benki, hivyo kusababisha watu wengi kuibiwa fedha zao kwa kutumia mitandao.

"Baada ya Rais kuongeza muda wa usajili tumebaini kuongezeka wimbi la utapeli unaofanywa na wakala wao wasio waaminifu, hivyo wananchi watambue zoezi linaloendelea ni la usajili wa laini za simu kwa njia ya kibiometria kwa kutumia kitambulisho cha Taifa au namba ya kitambulisho cha Taifa na siyo uhakiki wa akaunti za benki, hivyo akitokea mtu anayemtaka kufanya hivyo atoe taarifa mapema," alisema Mihayo.

Aidha, alisema, takwimu zinaonyesha hadi Desemba 31, mwaka jana idadi ya laini zilizosajiliwa ni 48,321,949, ambapo laini zilizosajiliwa kwa alama za vidole ni 24,021,757 sawa na asilimia 49.7 ya laini zote, huku laini ambazo hazijasajiliwa kwa alama za vidole ni 24,300,192.

Naye Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Nyamagana, Mrakibu wa Polisi Juma Jumanne, alisema, utapeli wa mitandao ya simu umeanza muda mrefu, na unabadilika kutokana na wakati, lakini usajili wa alama za vidole utasaidia kupunguza vitendo hivyo.

Hata hivyo, alisema baada ya siku za usajili kuongezwa, vitendo vya utapeli vimeongezeka, hivyo wananchi wachukue tahadhari na wawe makini.

Raphael Manase, Ofisa Msajili Mkoa wa Mwanza, aliwataka wananchi kuzingatia maelekezo wanayopewa na kufuata utaratibu uliopo pamoja na kutokukubali kupewa maelekezo mengine ya upotoshwaji, kitu ambacho kitasababisha kutapeliwa.

HABARI KITAIFA

# Abiria wasota usafiri wa mabasi mikoani

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ABIRIA katika kituo kikuu cha mabasi cha Moshi mjini wanaoelekea mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro, Arusha na mikoa ya Kanda ya Ziwa, wamesema kukodishwa kwa mabasi ya abiria na baadhi ya shule kwa ajili ya kubebea wanafunzi, kumesababisha wengi wao kusota kwa muda mrefu kituoni.

Jana kwa nyakati tofauti, abiria waliozungumza na Nipashe kuhusu hali ya usafiri kituoni hapo, walisema sababu hiyo ndiyo inayochangia kuwapo kwa uhaba wa mabasi yaendayo mikoani.

Licha ya adha hiyo kuelekea kupungua kutokana na kuwapo kwa safari za treni ya abiria ya De Lux kati ya mikoa ya Kilimanjaro, Tanga na Dar es Salaam, bado abiria wanalazimika kusubiri kwa muda mrefu usafiri badala ya kupata kwa wakati kama ilivyozoeleka.

HappyGod Reuben, aliyekuwa akielekea Mbezi, jijini Dar es Salaam, alisema alifika kituoni hapo tangu saa 11 alfajiri, lakini alifanikiwa kupata basi majira ya saa 4:00 asubuhi baada ya abiria mwenzake kughairi kuondoka siku hiyo.

"Kama sio abiria mmoja kughairi safari yake, nadhani ningeondoka mchana au ningekosa kabisa usafiri kwenda Dar, maana hakuwa akiona dalili za kupata usafiri mapema," alieleza HappyGod.

Nanderwa Mfinanga aliyekuwa akielekea mkoani Tanga, alisema hali hiyo inatokana na baadhi ya mabasi kukodishwa na wamiliki wa shule hasa msimu huu ambao wanafunzi wanafungua shule. Sijakata tamaa nimeenda nikawauliza mawakala wameniambia kwamba nitapata usafiri, lakini huenda ikawa mchana," alisema Mfinanga.

Kwa sasa, treni inayofanya safari zake kati ya Dar es Salaam na Moshi mkoani Kilimanjaro, imeongeza kivutio kingine cha nyama choma, kuuzwa ndani ya usafiri huo baada ya kuwapo kwa huduma ya bia.

Inaelezwa pia kuwa katika treni hiyo hivi sasa, huduma ya bia imeongezeka kutoka sanduku 50 hadi 150 kwa siku, kwa wasafiri wanaotoka Dar es Salaam kwenda Moshi.

Hata hivyo, abiria wanaokwenda Arusha na Morogoro, ndio wenye changamoto kubwa ya usafiri hasa kutokana na kutokuwapo na usafiri wa treni ya abiria.

Nipashe imeshuhudia maofisa wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) na askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoa wa Kilimanjaro, wakiwa bado wameweka kambi kituoni hapo kuhakikisha hali ya usafiri inakuwa katika mazingira rafiki.

Alipotafutwa ofisa wa LATRA kuzungumzia hali hiyo, Mosoud Abdalah, alisema wameweka kambi kituoni hapo kuwabana baadhi ya madereva wanaozidisha abiria na mawakala wanaopandisha nauli kutokana na wingi wa abiria uliopo.

# Mtoto afa kwa kugongeshwa kichwa kwenye gogo akicheza

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MTOTO Agnes Kiraba (3), mkazi wa Kijiji cha Mtakuja Kata ya Kirado wilayani Nkasi Mkoa wa Rukwa, amefariki dunia wakati akipatiwa matibabu hospitalini baada ya kugongeshwa kichwa kwenye gogo na mtu anayesadikiwa kuwa ni mgonjwa wa akili.

Mtoto huyo alipatwa na mauti katika Hospitali ya Wilaya ya Mkasi Januari 3, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Justine Masejo, tukio hilo lilitoke majira ya saa 1.30 za asubuhi kijijini humo.

Alisema kuwa Agnes alikuwa anacheza nje ya nyumba yao pamoja na watoto wenzake,

INAENDELEA UK. 8

PSSSF
Public Service
Social Security Fund

## TAARIFA KWA UMMA

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) unapenda kuutarifu umma kwamba unauza Nyumba na Viwanja vilivyoko maeneo mbalimbali nchini kama ifuatavyo:

**NYUMBA**
Nyumba zipo katika Mikoa ya Dar es Salaam (Buyuni-Chanika), Mtwara (Mangamba), Tabora (Usule) Morogoro (Lukobe), Shinyanga (Ibadakuli), na Iringa (Mawelewele).

Kwa sasa, mathalani nyumba zilizoko Mkoa wa Dar es Salaam, gharama zake ni kama ifuatavyo;

1. Nyumba yenye vyumba viwili bila "**master bedroom**" inauzwa shilingi milioni 31.
2. Nyumba yenye vyumba vitatu bila "**master bedroom**" shilingi milioni 35.
3. Nyumba yenye vyumba vitatu na "**master bedroom**" shilingi milioni 39.
4. Nyumba yenye vyumba vinne na "**master bedroom**" shilingi milioni 52.

Bei zote zimeonyeshwa bila Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).
Kwa bei ya nyumba tofauti na zilizoko Mkoa wa Dar es Salaam, tafadhali wasiliana nasi kupitia ofisi zetu za Mikoa ama kupitia namba ya simu 0657-151 938

**VIWANJA**
Mfuko unauza viwanja vilivyo katika maeneo ya Dar es Salaam, Pwani, Mwanza, Arusha, Lindi, Mpanda, Songea, Sumbawanga, Bukoba, Singida, Shinyanga, Mbeya, na Tabora. Viwanja hivi vinafaa kwa matumizi ya Makazi na Biashara (kama hoteli, shule, vituo vya mafuta n.k.), na viwanja vyote vina hati miliki.

Uuzaji wa Viwanja na Nyumba utafanyika kwa njia ya fedha tasilimu (**outright purchase**). Hata hivyo, kwa kuhakikisha kuwa watumishi wa umma na wananchi wengi wanapata fursa ya kumiliki kiwanja au nyumba ya kuishi, Mfuko umekamilisha mazungumzo na benki ya AZANIA, na kwa kupitia benki hiyo, watumishi wa umma na wananchi watapata mikopo itakayowawezesha kununua nyumba na viwanja hivyo kwa njia ya mkopo.
Kwa taarifa zaidi piga simu namba 0657-151-938
au wasiliana nasi kupitia ofisi yoyote ya PSSSF mikoani.

**Imetolewa na:**
**MKURUGENZI MKUU**
**MFUKO WA HIFADHI YA JAMII KWA WATUMISHI WA UMMA (PSSSF)**
**DODOMA**

Leo. Kesho. Pamoja 0800 110 040 www.psssf.go.tz PSSSFTZ

# Kalemani ampa mkandarasi mpaka Mei kukamilisha kituo

**Na Alphonce Kabilondo**, GEITA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amemtaka mkandarasi wa kampuni ya China Camc Engineer Company Limited, anayejenga kituo cha kupoza na kuzalisha umeme Halmashauri ya mji wa Geita, kukamilisha ujenzi huo Mei, mwaka huu badala ya Juni ili wananchi wapate umeme wa uhakika mapema.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akiweka jiwe la msingi katika ujenzi wa kituo cha kupozea na kufua umeme, kinachojengwa katika Mtaa wa Mpomvu, Kata ya Mtakuja, Mjini Geita.

Alisema kituo hicho kitasafirisha umeme wa kilovoti 220 kutoka katika kijiji cha Ibadakuli mkoani Shinyanga hadi Bulyanhulu na utasafirishwa hadi kwenye kituo hicho ambacho kitazalisha umeme wa megawati 85.

"Mkandarasi unayejenga kituo hiki hakikisha ujenzi wa unakamilika mwezi Mei mwaka huu badala ya mwezi Juni kama ambavyo miradi yetu ya umeme inavyokuwa ikikamilika kabla ya muda wa mkataba," alisema Dk. Kalemani.

Alisema serikali inakusudia kuunganisha umeme wa Gridi ya Taifa kwenye migodi yote ya uchimbaji wa madini ya dhahabu mkoani humo kwa kipindi cha mwaka 2020 baada ya kukamilika ujenzi wa kituo hicho.

Kadhalika, alisema kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita Shirika la Umeme nchini (Tanesco) liliunganisha umeme kwenye migodi 28 ya uchimbaji wa madini ya dhahabu mkoani humo kwa migodi yenye leseni za kati na wachimbaji wadogo na migodi saba inatarajiwa kuunganishiwa umeme wa gridi.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, akitoa salamu za Mkoa wa Geita alisema, umeme utasaidia kuinua uchumi wa kati wa viwanda na kuongeza kuwa mkoa huo una viwanda vya kuchenjua dhahabu 156 ambavyo vinahitaji umeme wa kutosha.

Alisema kwa sasa kuna ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kusafisha madini ya dhahabu na madini mengine kabla ya kuyapeleka kuyauza nje ya nchi ambacho pia kinahitaji umeme.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini, Constantine John Kanyasu amesema Rais Dk. John Pombe Magufuli, amesikiliza kilio cha muda mrefu cha wananchi wa mji wa Geita mwaka 2015, wakati alipochaguliwa kuwa mbunge wa jimbo hilo, wananchi walikuwa wakipata umeme kutoka Mkoa wa Mwanza ambao ulikuwa ukikatika kila mara.

Mwenyekiti wa Bodi ya Tanesco, Alexander Kyaruzi, amesema, shirika hilo lina mipango mahsusi ya kuhakikisha mikoa michache iliyosalia inapata umeme wa gridi ya taifa. Maeneo yanayotajwa kutokuwa kwenye gridi ya taifa ni Sumbawanga na Kigoma.

Mkurugenzi Mkuu wa Tanesco, Dk. Tito Mwinuka, akitoa taarifa ya mradi huo, alisema Mkoa wa Geita unapokea umeme kutoka njia ndogo kutoka Mwanza, lakini kutoka na shughuli nyingi za uwekezaji haukidhi mahitaji na kuamua kujenga kituo hicho.

Meneja wa Kampuni ya China Camc Engineer Company limited, Song Jianxia, anayejenga mradi huo, alisema ujenzi wa kituo hicho ulianza Januari mwaka 2019 na unatarajiwa kukamilika Juni, mwaka huu kwa mujibu wa mkataba.

Hata hivyo anasema kuwa ujenzi huo unasusua kutokana na mvua kunyesha kila mara.

# Taboa sasa yaililia TRA utekelezaji agizo la PM

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi nchini (Taboa), kimeeleza kusikitishwa na ukimya wa mamlaka zinazowasimamia, huku ikieleza kuwa wamegoma kutumia mfumo wa kielektroniki kukata tiketi za abiria.

Aidha, kamati ya utendaji wa Taboa imekutana kujadili namna bora ya kutekeleza agizo la serikali kukatisha tiketi kwa mfumo wa kielektroniki.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu wa Taboa, Enea Mrutu, alisema wamiliki hao wako tayari kuingia kwenye mfumo huo ambao utarahisisha mambo mengi.

Alisema Juni 30, mwaka jana katika kikao chao na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kushughulikia suala hilo ili kuhakikisha linakamilika kwa wakati na kuiwezesha serikali kukusanya mapato halali kutoka katika sekta hiyo.

Mrutu alisema kuwa licha ya chama hicho kukutana na TRA katika kikao kilichofanyika Oktoka mwaka jana na kukubaliana masuala mbalimbali ikiwamo kupatikana mfumo rahisi utakaorahisisha utekelezaji wa agizo hilo, pande hizo hazijaweza kukutana tena.

Pia alisema wanashtushwa na taarifa kuwa hawataki kutumia mfumo huo.

"Katika kikao chetu cha kamati tendaji tumesisitiza kuangalia namna bora ya kutekeleza mfumo huo ili kuondoa minong'ono kuwa hatuki kutumia tiketi za kielektroniki kwa sababu tulikubaliana na Waziri Mkuu na tayari tulishakutana na TRA kikao cha kwanza sasa kama kuna ucheleweshaji ni TRA," alisema na kuongeza:

"Tulipokutana na TRA tulikubaliana wafanye mambo mawili, moja waje na mfumo utakaowezesha wao kukata kodi yao na sisi kubakiwa na chetu au wafanye 'flat rate' (kiwango cha kulingana) wakadirie kila basi litalipa kiasi gani kwa mwaka ili kuondoa huu utata."

Kwa mujibu wa Mrutu, licha ya Waziri Mkuu aliziagiza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kushughulikia utaratibu wa matumizi ya mfumo wa ufuatiliaji wa mwendo wa mabasi (VTS) ili kuondoa kasoro mbalimbali zilizojitokeza katika utekelezaji wa mfumo huo, jambo hilo halijafanyika hadi sasa.

"Tangu Juni hadi leo wasafirishaji na watoa huduma tunaendelea kuumia na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Sasa tunaomba kauli ya Waziri Mkuu iheshimiwe," alisisitiza Mrutu.



Mapokezi ya Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo Taifa (Bavicha), John Pambalu, alipowasili katika ofisi za Kanda za Chadema zilizopo mkoani Mwanza akitokea Dar es Salaam jana, baada ya kuchaguliwa. **PICHA: ROSE JACOB**

# Mtumishi hospitali kortini tuhuma wizi dawa za ARV

**Na Jumbe Ismailly**, IGUNGA

MFAMASIA wa Hospitali ya Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, Francis Mlesa (33), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakmu Mkazi wa wilaya hiyo kwa tuhuma za wizi wa dawa za wagonjwa.

Mwendesha Mashtaka, Joseph Mwambwalu, alidai kuwa mshtakiwa huyo anakabiliwa na shtaka moja la wizi.

Mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Igunga, Edda Kahindi Mwambwalu, alidai Desemba 24, mwaka jana majira ya usiku, katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga, mtuhumiwa akiwa mwajiriwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, anatuhumiwa kuiba chupa 30 za vidonge vya dawa ya kufubaza Virusi vya Ukimwi (ARV) zenye thamani ya Sh. 2,116,000. Mwambwalu, alidai kuwa huku mshtakiwa huyo akitambua kwamba yeye ni mtumishi wa umma, aliamua kutenda kosa hilo kinyume cha kifungu 270 cha kanuni ya adhabu sura ya 16 mapitio ya 2002 inayozuia kutenda makosa kama hayo.

Hata hivyo, baada ya mshtakiwa huyo kusomewa shtaka lake, alikana na hakimu kuiahirisha kesi hiyo hadi Januari 31, mwaka huu, na mshtakiwa yuko nje kwa dhamana ya Sh. 300,000 kwa maandishi.

# Vyama hewa 3,436 ushirika kufutwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI inakusudia kuvifuta vyama hewa vya ushirika 3,436 kwa mujibu wa sheria ya ushirika baada ya kuvifanyia uchuguzi na kubaini kuwa havipo katika maeneo ambayo vinaonyesha vilisajiliwa wala viongozi wake hawajulikani.

Hayo yalielezwa jana na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Hasunga alisema mpaka sasa daftari la mrajisi wa vyama vya ushirika nchini lina jumla ya vyama 11,149, vilivyoandikishwa.

Alisema kati ya hivyo 3,436 havijulikani vilipo (hewa) na vyama 1,250 vimesinzia na vyama 6,463 vipo hai.

"Kutokana na kuwapo kwa vyama hewa katika daftari la mrajisi wa vyama vya ushirika, nilimwagiza kutangaza kwenye gazeti la serikali kusudio la kuvifuta vya hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika kifungu 100, ambacho kinaeleza kuwa chama kinaweza kufutwa kwa sababu mbalimbali," alisema Hasunga.

Aidha, Hasunga alizitaja sababu ambazo zinaweza kusababisha chama cha ushirika kufutwa kuwa ni pamoja na toka kiandikishwe hakina ofisi, hakijulikani kilipo na viongozi wake hawafahamiki na hawapatikani.

Sababu nyingine ni vyama hivyo vimeshindwa kutekeleza takwa la kisheria la kutayarisha makisio ya mapato na matumizi na kuyapeleka kwa marajis kuyapitia, kutayarisha taarifa ya mwaka, kufunga mahesabu na kuyapeleka COASCO, kwa ukaguzi na kutofanya mikutano ya mwaka ya wanachama wote na bodi zao.

"Sababu nyingine ni pamoja na chama kushindwa kufanya shughuli zake ndani ya miezi sita tangu kiandikishwe, idadi ya wanachama kupungua kwa mujibu wa mahitaji ya kisheria na kushindwa kuteleza matakwa ya kisheria kama vile sheria za fedda za benki kuu ya Tanzania kwa upande wa Saccos," alisema Hasunga.

Akitoa maagizo kwa mrajisi wa vyama vya ushirika nchini Hasunga alisema kwa kuzingatia sheria No. 6 ya mwaka 2013 ya vyama vya ushirika kifungu 100 na kanuni ya 26, mrajisi anatakiwa kutoa notisi ya kusudio la kutaka kufuta vyama vya ushirika kwenye gazeti la serikali kwa muda wa siku 90.

"Hivyo ninamwagiza mrajisi wa vyama vya ushirika kutangaza mara moja kusudio la kufuta vyama 3,436 ambavyo havitekelezi majukumu yake ya msingi na

INAENDELEA UK. 8

# Wakulima waahidiwa fursa zaidi

**Na Mwandishi Wetu,** RUVUMA

WAKULIMA nchini wamehakikishiwa kuendelea kunufaika kwa fursa mbalimbali zitolewazo na taasisi za fedha zikiwamo benki.

Wamepewa ahadi hiyo na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), ambayo imesema itaendelea kuchagiza maendeleo ya kilimo nchini ili kumpatia tija na kumnufaisha mkulima.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea wakulima na miradi ya kilimo iliyopewa mikopo na TADB.

Miongoni mwa miradi iliyokopeshwa na TADB ni kiwanda cha Real World cha kuchakata mahindi kilichopo mkoani hapa.

Katika ziara hiyo Justine pia alikutana na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme. Alieleza kuwa malengo makuu yao ni pamoja na kusaidia upatikanaji na utoshelezi na usalama wa chakula ambao ni endelevu nchini; na kuchangia na kusaidia mapinduzi ya kilimo kutoka kilimo cha kujikimu kwenda kilimo cha kibiashara ili kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

Alisema mikakati ya benki ni kuanza mwaka kwa kutembelea mikoa yenye uzalishaji mkubwa wa chakula nchini.

Alisema: "Ndio maana kwa kupitia viwanda, tunaamini hadi mkulima wa chini ananufaika na masoko. Pia, lengo letu ni kuanza kuwakutanisha wakulima na kushirikiana fursa katika mnyororo wa thamani."

"Kwa wanaozalisha vifungashio waweze kushirikiana na wasindikaji na wachakataji ili kwa pamoja kuinua uchumi wa nchi. Pia tungependa zaidi kuleta maendeleo ya kilimo mkoani hapa Ruvuma na tunashukuru na kupokea wito wa Mkuu wa Mkoa wa kuleta tawi mkoani hapa ili tuwahudumie wakulima kwa ukaribu zaidi."

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, ameitaka TADB kufungua tawi la benki hiyo mkoani humo ili kuwahudumia wakulima kwa ukaribu zaidi.

Alisema mkoa wa Ruvuma, ni moja ya mikoa saba Tanzania yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula, hasa uzalishaji wa mazao ya nafaka kama mahindi.

RC Mndeme alisema Ruvuma ni mkoa unategemea kilimo kwa asilimia 99.9 kama shughuli ya kiuchumi.

Na mahindi ni zao kubwa linalotegemewa kwa chakula na biashara. Na mazao mengine ni kama tumbaku, kahawa na ufuta. Na kwa msimu uliopita, ufuta tu ulizalisha Sh. bilioni 24.

Alitaja baadhi ya changamoto mbalimbali zilizopo katika kilimo ikiwamo maghala ya kutosha, pembejeo na rasilimali.

Hata hivyo, aliishukuru benki hiyo kwa kufungua fursa nyingi za kilimo kwa kuwekeza Sh. bilioni 2.8 kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kilimo ikiwamo kuyapa thamani mazao ya kilimo kupitia viwanda vinavyoongeza masoko ambapo imeleta hamasa ya uzalishaji na kuinua vyama vya wakulima 18.

RC Mdeme alisema kwa sasa mkoa huu una mkakati wa kufanya uzalishaji katika hekta milioni 1.8 ambapo msimu uliopita ilikuwa milioni 1.6 tu.

John Magogo, Meneja wa kiwanda kinachochakata mahindi cha Real World ambaye ni mmoja wa vijana waliopata ajira katika kiwanda hicho, alisema kuwa kupitia uwezeshaji wa TADB, mimi na vijana wenzangu tumenufaika kwa ajira na pia uzalishaji wa bidhaa za chakula na mifugo kiwandani umeongezeka na kupanua masoko hadi Mtwara, Liwale, Lindi na Dar es Salaam.


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

ISO 9001: 2015 IMETHIBITISHWA

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MNADA WA FORODHA KWA NJIA YA MTANDAO**

**Dar es Salaam, Januari 2, 2020:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha wananchi wote kuwa, kwa mara ya kwanza, mnada wa forodha kwa njia ya mtandao utafanyika tarehe 2 hadi 6 Januari, 2020 kupitia Tovuti ya TRA ambayo ni www.tra.go.tz.

Mnada huo utaanza saa 6:00 usiku tarehe 2 na kumalizika saa 5:59 usiku tarehe 6 Januari, 2020 ambapo washindi watatangazwa tarehe 7 Januari, 2020 kupitia tovuti ya TRA.

Ili kushiriki mnada huo kwa njia ya mtandao, mwananchi anatakiwa: -

1. Awe na kifaa kilichounganishwa na mtandao, kama vile Simu ya mkononi, Kompyuta ya mezani, Kompyuta mpakato yaani laptop n.k;
2. Awe na Namba ya Utambulisho ya Mlipakodi yaani TIN na kama hana TIN atatakiwa kujisajili kupitia tovuti ya TRA ya **www.tra.go.tz** ili kupata TIN kwanza;
3. Awe na barua pepe yaani ***email address;***
4. Awe na namba ya simu;
5. Awe amejisajili kwenye tovuti ya TRA kupitia ukurasa wa mnada kwa kubonyeza sehemu ya juu iliyoandikwa ***Auctions;***
6. Wakati wa kujisajili, mshiriki atahitajika kuhakiki kama jina alilojisajili limeshatumika na mtu mwingine ama la kwa kubonyeza kitufe cha tafuta **(Search icon)**. Hata hivyo, mtu yeyote anaweza kuona bidhaa zilizotangazwa kupitia mtandao hata kama hajajisajili;
7. Baada ya kujisajili, mshiriki ataweza kushindana na washiriki wengine kwa kuweka bei na atakuwa na uwezo wa kuongeza bei kadri ushindani utakavyokuwa ukiendelea;
8. Mshindi atapata ankara ya malipo ya awali ya asilimia 25 na ankara ya malipo ya kumalizia ya asilimia 75 kupitia mtandao na atakwenda benki kwa ajili ya kulipia;
9. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia 25 mara baada ya kupata ankara ya malipo wakati ankara nyingine ya malipo ya asilimia 75 atatakiwa kulipia ndani ya saa 48 ingawa kwa chombo cha moto kama vile gari, pikipiki n.k kutakuwa na ankara nyingine kwa ajili ya kulipia ada ya usajili; na
10. Baada ya kukamilisha malipo, mshindi atatakiwa kufika eneo la forodha mzigo ulipo kwa ajili ya kuchukua mzigo wake akiwa na uthibitisho wa kuonyesha kuwa yeye ndiye mnunuzi halali.

Kupitia taarifa hii, wananchi wote walioko ndani na nje ya nchi wanakaribishwa kushiriki mnada huo wa forodha kwa njia ya mtandao wenye haki sawa kwa kila mtu atakayeshiriki mnada.

Kwa maelezo zaidi, mwananchi anaweza kupiga simu katika Kituo cha Huduma kwa Mlipakodi kwa namba za bure **0800 75 00 75 au 0800 78 00 78.** Pia, anaweza kutuma ujumbe kwa njia ya WhatsApp namba **0744 23 33 33** au kutuma barua pepe kwenda: **huduma@tra.go.tz.**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:**

**Richard Kayombo**

**Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi**

215571902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matokeo Simba, Yanga yasichafue upepo klabuni

**BAADA** ya tambo zilizodumu tangu kuanza kwa msimu huu wa 2019/2020 wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hatimaye miamba ya soka nchini, Simba na Yanga imekutana katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi.

Mechi hiyo ya watani wa jadi ilikuwa 'dabi' ya 100 tangu zianze kukutana na Yanga ilishuka dimbani ikiwa imeshinda mara 36 wakati Simba ikishinda mara 28 huku zikitoka sare mara 35.

Hivyo, kwa matokeo ya sare ya mabao 2-2 zilizoyapata juzi, yanaifanya miamba hiyo sasa kutoka sare mara 36 na Yanga ikiendelea kushikilia rekodi ya kushinda mara nyingi zaidi.

Hakika matokeo hayo yanaweza kuwa yasiyotarajiwa hasa kutokana na jinsi kila upande ulivyokuwa ukijinasibu kuibuka na ushindi kabla ya mechi kupigwa.

Simba ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ilikuwa ikijivunia muunganiko mzuri wa kikosi chake pamoja na ubora wa mchezaji mmoja mmoja.

Kwa upande wa Yanga inayoshika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo, bado ilikuwa haijawa na muunganiko mzuri katika kikosi chake, lakini mbali na ubora wa mchezaji mmoja mmoja ilikuwa ikijivunia zaidi namna ilivyokiboresha katika dirisha hili dogo la usajili.

Hata hivyo, pamoja na kila timu kuamini ingeweza kuibuka na pointi tatu muhimu, matokeo yamekuwa tofauti na miamba hiyo imejikuta ikiambulia alama moja moja.

Tunatambua wapo mashabiki waliokwenda uwanjani wakiwa na matokeo yao mkononi kutokana na kuamini usajili walioufanya na ubora wa wachezaji wao.

Hata hivyo, hawana budi kuyapokea matokeo yaliyopatikana na kuganga mbele kwa kuwa mchezo wa soka una matokeo matatu, kushinda, kushindwa ama sare.

Kadhalika, mashabiki wa Simba na Yanga hawana budi kutambua timu hizo ndiyo kwanza zipo mikononi mwa makocha wapya hivyo hawana budi kuwapa muda zaidi.


Simba ipo mikononi mwa Sven Vandenbroeck aliyerithi mikoba ya Mbelgiji mwenzake Patrick Aussems mwezi uliopita wakati Boniface Mkwasa akikaimu mikoba ya Mwinyi Zahera mwezi mmoja na wiki kadhaa sasa.

Hivyo, ni makocha wanaohitaji muda zaidi ili kuweza kuzijenga timu zao na wachezaji kuzoea mifumo na mbinu kutoka kwao.

Tunasema hivyo kutokana na kufahamu chokochoko zinazoweza kujitokeza kutokana na mashabiki ambao huenda uwanjani na matokeo yao, kwani hawa huwa hawakawii kwa kutaka makocha watimuliwe.

Matarajio yetu ni kuona Vandenbroeck na Mkwasa wakipewa muda zaidi kuzijenga timu zao ili zitakapokutana mzunguko wa pili ziweze kutoa burudani nzuri zaidi kwa kuwa kila mmoja atakuwa amepata muda wa kutosha wa kukiimarisha kikosi chake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Jonesia alivyoitendea haki mechi ya watani

**ZIPO** taarifa kutoka kwa baadhi ya viongozi na wanachama na baadhi ya mashabiki wa Simba na Yanga wakimlaumu mwamuzi, Jonesia Rukyaa kuwa hakulimudu pambano hilo.

Baadhi ya viongozi wa Yanga wanadai kuwa mwamuzi aliwabeba Simba hasa kwa ile penalti ambao wao wanadai haikuwa halali.

Wanachama na mashabiki wa Simba nao wanalalamika kuwa bao la pili la Yanga kabla ya kufunga, Mohammed Hussein 'Tshabalala' alikuwa amefanyiwa madhambi.

Kwa kawaida kwenye mechi kubwa kama hizi, hasa za Simba na Yanga malalamiko huwa hayakosekani kwa timu yoyote ile.

Iwe timu moja imeshinda, iliyofungwa italalamika, hata zikitoka sare tabu. Inawezekana kulikuwa na makosa kadhaa kwenye mechi hiyo, lakini yalikuwa ni ya kibinadamu kama inavyotokea kwenye mechi hata za nje ya nchi.

Kwa sasa tunashuhudia kwenye Ligi Kuu hasa ya England mechi zimeanza kuamuliwa na teknolojia ya VAR, ambayo husahihisha pale mwamuzi anaposokea au kushinda kung'amua tukio lililofanyika haraka na kushindwa kulibaini.

Kama waamuzi wa kiume Ulaya inafika wakati wanaamuliwa na VAR, iweje kwa Jonesia, mwanamama Mtanzania ambaye anachezesha mechi ya watani wa jadi yenye presha ambayo inawashinda hata wanaume?

Mwamuzi huyo amechezesha mechi hiyo bila msaada ya teknolojia, hivyo kama kulikuwa na makosa madogo basi yalikuwa ni ya kibinadamu na si ya kusababisha eti watu kumbebesha lawama na kuvunja nguvu kwa kazi yake hiyo ngumu.

Tatizo lililokuwapo kwenye timu hizi mbili ni kwamba kila mmoja anataka apendelewe yeye, lakini kila moja ashinde yeye hapo ndipo mwamuzi anapoonekana ametenda haki.

Ifike mahali tukubali maamuzi ya waamuzi, lakini klabu zifundishe wachezaji wao kujua sheria za soka na si kufanya mambo mengine ya ajabu ambayo yanamweka mwamuzi njia panda.

Kwa upande wa Jonesia, maneno ya mashabiki yasimvunje moyo wala kumwondoa kwenye safari yake ya uamuzi kwani mpaka sasa amekuwa ni mwamuzi bora kabisa kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na nadhani huko mbele anaweza kuwa bora Afrika na dunia.

Jonesia achukulie kama changamoto kwani mashabiki wa soka kiasili ni walalamishi, kwani hata huko Ulaya pamoja na mwamuzi kusaidia wa teknolojia ya VAR, lakini bado wamekuwa wakiilalamikia hiyo hiyo VAR kuwa inapendelea baadhi ya timu.

Nilirejea upande wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) na Bodi ya Ligi, imefika wakati sasa wa kuangalia kurekebisha kanuni ili kuruhusu waamuzi kutoka nje kuchezesha mechi kubwa kama hizi ili kuondoa malalamiko yasiyo ya msingi.

Kanuni irekebishwe ili mechi kama hizo za Simba na Yanga zichezeshwe na waamuzi kutoka nje ya nchi kwani itachezeshwa na watu ambao hawajulikani na viongozi wala mashabiki, na wao pia watakuwa hawana presha ya mechi hiyo kwa sababu ni wageni.

Hata kama kutakuwa na makosa ya kibinadamu, kwa sababu mwamuzi kutoka nje, malalamiko yake hayatokuwa makubwa kama vile yule ni timu fulani, au kala mlungula, tofauti na waamuzi wa hapa nchini wanavyosingiziwa.

TFF haitokuwa ya kwanza kufanya hivyo kwa sababu tumeona nchi nyingi, mechi zao za watani wa jadi zinaamuliwa kwa kuletwa waamuzi ambao nao kwao ni wageni machoni, wanachezesha na kuondoka.

Hii itawafanya hata waamuzi wetu kuwa salama na kuondokana na tabia za kuwatuhumu vitu visivyo na msingi na kuwavunja moyo kwa kazi yao hiyo ngumu, inayohitaji ujasiri wa hali ya juu hasa kuchezesha mechi ya Simba na Yanga kama alivyofanya mwanamama huyo.

MJADALA

# Simba na Yanga imepita, kila timu igange yajayo

Na Adam Fungamwango

MECHI iliyokuwa ikisubiriwa kwa hamu muda mrefu sana, kati ya watani wa jadi, Simba na Yanga imemalizika Jumamosi iliyopita kwa sare ya mabao 2-2 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Ni mechi iliyokuwa na msisimko mkubwa ndani na nje ya uwanja, ikishuhudiwa na maelfu ya mashabiki waliokuwa uwanjani, lakini maelfu ya Watanzania wakiifuatilia mechi hiyo kwa njia mbalimbali kama vile kutazama kwenye runinga, baadhi kusikiliza kupitia vituo vya radio na wengine walikuwa hawasikilizi kabisa mpira zaidi ya kupata taarifa au matokeo ya mechi kwenye simu, au mitandao ya kijamii.

Mechi imemalizika kwa kila timu kupata pointi moja na magoli mawili, hivyo kujiongezea pointi moja na magoli mawili kibindoni.

Zaidi ya utani wa jadi, mechi ya Simba na Yanga ni mechi kama zilivyo mechi nyingine.

Ilikuwa ni mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kama mechi nyingine zote ambazo timu ikishinda inapata pointi tatu, ikitoa sare pointi moja na inayofungwa haipati pointi, hivyo haina maana kuwa baada ya mechi hiyo hakuna kinachoendelea.

Naandika hivi nikiwa na maana, kutokana na mazingira yenyewe ya mechi yalivyopokelewa.

Nikianza kwa upande wa Simba, wanachama na mashabiki wao wengi walionekana kusononeka na kutupa lawama baada ya timu yao kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Yanga.

Waliomini kuwa mechi hiyo wangeibuka na ushindi na hasa baada ya kuongoza kwa mabao 2-0, kabla ya magoli hayo kurejeshwa.

Wachezaji na viongozi wa Simba nao pia wameonekana kuumia kutokana na matokeo hayo.


Lakini nawaambia kuwa mechi imeisha, hivyo badala ya kuanza kupeana lawama au kuanza kumtafuta uchawi, watulie na kujipanga kwa mechi zingine za Ligi Kuu na kuachana kabisa na kukumbuka mechi dhidi ya Yanga.

Kwa sasa Simba inaongoza ikiwa na pointi 35, hivyo kinachohitajika na benchi la ufundi kuangalia mapungufu yako wapi, kuyarekebisha na kuendelea kutafuta pointi tatu kwenye mechi zinazofuata kana kwamba hakikutokea kitu chochote huko nyuma.

Hii inaweza kuwaweka karibu na ubingwa kuliko kuanza kutafuta ni kwa nini wametoka sare na Yanga.

Viongozi, wanachama, wachezaji na mashabiki wa Simba waache kunyoosheana vidole, badala yake waungane kwa ajili ya kusaka ushindi kwenye mechi zinazofuata kwa sababu mechi hiyo imemalizika na maisha lazima yaendelee.

Kitendo cha kuanza kutafutana uchawi, kinaweza kushusha morali ya wachezaji na kuanza kuboronga mechi zinazofuata na hatimaye kuukosa ubingwa.




Kwa upande wa Yanga wao wanashangilia sare kwa sababu ilionekana kana kwamba hawana uwezo wa kuifunga Simba.

Lakini kitendo cha kutanguliwa mabao mawili, lakini ikaweza kurudisha kimewafanya wawe na furaha isiyo kifani.

Ni kweli Yanga inastahili furaha, lakini isipilize kiasi mpaka kupoteza malengo iliyojiwekea ya kuhakikisha inarejesha ubingwa ambao Simba imeuhodhi kwa miaka miwili mfululizo.

Ukiangalia pamoja na kushangilia sare, lakini Yanga ipo nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi kwa pointi 26, nyuma ya Coastal Union na Azam FC zenye pointi 26 kila moja.

Pamoja na kwamba iko nyuma kwa mechi moja dhidi ya Azam na tatu dhidi ya Coastal, lakini isibweteke na sare dhidi ya Simba kwani mara nyingi tumeona wachezaji wakitoka kwenye mechi hizo kubwa huridhika na kufanya vibaya michezo inayofuata.

Viongozi wa Yanga wanapaswa wawaambie wachezaji wao kuwa hawajashinda mechi dhidi ya Simba bali wametoka sare na wanahitaji ushindi kwenye mechi zinazofuata ili kutowafanya kuanza kuzoea kuwa sare nayo ni ahueni kwao.

Baada ya mechi dhidi ya Simba, kazi ya kusaka ubingwa ni lazima iendelee na kichwani mwao wafute matokeo ya mechi hiyo kwa sababu tayari imemalizika na zinazofuata ni mechi zingine.



# Homa ya uchaguzi CCM, Chadema yapanda

INATOKA UK. 2

Mkuu, kwa niaba ya mwenyekiti wa CCM mkoa wa Singida, Juma Kilimba, Mwenyekiti wa Chama Wilaya Singida Mjini, Lucia Mwiru, aliwataka madiwani wa manispaa kushirikiana ili kudhibiti ubovu wa miundombibu ya barabara.

Aliagiza wakutane na mkuu wa wilaya hiyo, kwa lengo la kujadili miundombinu dhaifu ya barabara zinazozunguka mji wa Singida na vijijini, ambazo zinatekelezwa na wakala wa barabara wa mijini na vijijini (Tarura), ambazo ni mbovu.

Akiwasilisha taarifa yake ya miaka minne, Mbunge Sima ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano (Mazingira), alieleza kujivunia katika kipindi chake cha miaka minne kuboresha sekta ya elimu, afya na maji.

"Endeleeni kuniamini mimi kijana wenu, sasa hivi tunapigania ziwepo shule mbili za kidato cha tano hadi cha sita, na tayari zimeshapatikana... katika Shule ya Sekondari Mungumaji, tumejenga mabweni mawili na juhudi zaidi zinaendelea ili watoto wetu wapate elimu ya juu," alisema.

Naibu Katibu Mkuu alikuwa katika ziara ya siku moja, Manispaa ya Singida.

**WANAOJITANGAZA WAONYWA**

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mara, Samuel Kiboye (Namba Tatu), amesema makada wanaoendelea kuvunja kanuni za chama kwa kuanza kutangaza nia kabla ya wakati watashughulikiwa kwa kuwa mbali na kuvunja kanuni za chama pia wanaifanyia hujuma serikali iliyopo madarakani.

Kiboye alirejea msimamo huo jana baada ya kuutoa hivi karibuni mjini Butiama, Mara wakati wa sherehe fupi ya maadhimisho ya miaka 90 ya Mama Maria Nyerere ambaye ni mke wa Rais wa kwanza, Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

"Miongoni mwetu kuna watu au makada ambao hawasikii kabisa, badala ya kuheshimu kanuni za Katiba ya chama wameendelea kuivunja kwa kutangaza nia ya kuwania nafasi mbalimbali ukiwamo ubunge mkoani hapa.

"Naomba walifahamu na walielewe ili kwamba, kuvunja kanuni za chama ni miongoni mwa sababu kubwa za utovu wa nidhamu na kukidharau chama, hivyo hatuwezi kuwavumilia na hatutamwogopa mtu iwe ni kada ambaye ana cheo kikubwa, kwa kuwa muda wa kufanya hivyo bado na kuna taratibu zitapaswa kufuatwa wakati ukifika," alifafanua Kiboye.

Aliongeza kuwa, muda ukifika vikao vya chama ndiyo vitakavyoamua ni nani ambaye anapaswa kuwania nafasi ipi ikiwa anakidhi vigezo vitakavyoainishwa muda ukifika.

"Vinginevyo wanaoendelea kujitangaza watambue wanapoteza muda wao na lazima hatua kali zitachukuliwa dhidi yao," aliongeza.

**CHADEMA WAHAMASISHWA KUOMBA VIBALI MIKUTANO**

Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Nyasa ambaye ni Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, amewaagiza viongozi wa majimbo katika kanda hiyo kuandika

INAAENDELEA UK. 26




Mkurugenzi Mkuu wa Swissport Tanzania, Mrisho Yassin (wa tatu kulia), pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Mipango Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), Kitula Yango ( wa tatu kushoto), wakikata keki wakati wakiingia makubaliano ya kufanya kazi pamoja kati ya Swissport na Air Tanzania, hafla hiyo iliyofanyika katika Viwanja vya Ndege Terminal 3 Dar es Salaam jana. Wengine ni maofisa kutoka Swissport na ATCL. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CAG afichua zilipo tril. 1.46/- mikopo wanafunzi

INATOKA UK. 2

ya kutopewa mikopo tangu kufunguliwa kwa chuo hicho na kusababisha kuishi kwa tabu.

Siku chache baadaye, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alitoa onyo kali kwa wanafunzi hao waliotangaza mgomo na kuagiza uongozi wa UDSM kuchukua hatua.

Siku iliyofuata uongozi wa UDSM uliwasimamisha masomo wanafunzi na viongozi wa serikali ya wanafunzi ambao walidaiwa kuvunja kanuni za chuo hicho.

Pia serikali ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (Sua), iliiomba serikali kuharakisha upatikanaji wa mikopo kwa kuwa wanaishi maisha magumu toka vyuo hivyo vifunguliwe.

Siku chache baadaye Bodi ya Mikopo ilitangaza kuanza kutoa fedha kwa wanafunzi walioko vyuoni, ikiwamo wanafunzi 698 walioshinda rufani mbalimbali.

**MASHIRIKA 11 TAABANI**

Katika ripoti hiyo ya CAG, pia ilionyesha kuwa mashirika ya umma 11 yanajiendesha kwa hasara kwa zaidi miaka miwili na kuwa tegemezi kwa msaada kutoka serikalini.

Kwa mujibu wa Mkaguzi Naiman, mashirika hayo yanajiendesha kwa hasara tofauti na mashirika mengine.

**MENGINE 14 YASUASUA**

Alisema mashirika 14 ya umma yana changamoto za kifedha na kupata hasara ambayo inawasababishia madeni kuwa zaidi ya mitaji yao.

Ripoti hiyo ilitoa mapendekezo kwa serikali ifanye mapitio ya namna ya uendeshaji wa mashirika hayo na kuongeza mitaji ili yaweze kumudu gharama za uendeshaji.

Kadhalika ripoti hiyo ilionyesha kuwapo kwa wadaiwa sugu wa pango jumla ya wapangaji 623 wanaoendelea kupokea huduma ya upangaji katika kituo cha mikutano cha AICC licha ya kuwa na madeni sugu yanayofikia Sh. bilioni 3.8.

**NIC YAELEMEWA**

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Shirika la Bima la Taifa (NIC) limeripotiwa madai ya kiasi cha Sh. bilioni 53 wakati deni halisi ni Sh. bilioni 63 madeni hayo yana upungufu wa thamani halisi ya kiasi cha Sh. bilioni 10. "Kuna uwezekano kuwa mapato yaliyorekodiwa hayakuwa halisi hivyo serikali imependekeza mashirika halisi yanatakiwa kutekeleza sera zao za upangaji na usimamizi wa madeni ili kuwa na usimamizi imara wa mapato," ilisema ripoti hiyo. Alisema wakifanya hivyo watagawanyika kwa kiasi kikubwa kuwa na mifumo imara ya usimamizi wa mapato ya fedha ambazo zinatakiwa kupatikana.

## Mtoto afa kwa kugongeshwa kichwa

INATOKA UK. 3

ndipo alipopita mtu huyo na kumkamata mtoto huyo na kumgongesha kwenye gogo.

Baada ya kitendo hicho, wazazi wa Agnes walimkimbiza katika kituo cha afya Kirando kwa ajili ya matibabu, lakini hali yake iliendelea kuwa mbaya hali iliyo walazimu kumpa rufani na kumpeleka katika Hospitali ya Wilaya.

Kamanda Masejo alieleza kuwa Agnes alipofikishwa katika hospitali hiyo alianza kupewa matibabu, lakini alifariki dunia muda mfupi baadaye kutokana na kulalamika maumivu makali ya kichwa.

Kamanda Masejo alisema kuwa mtuhumiwa anashikiliwa na Jeshi la Polisi, na kwamba atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

## Vyama hewa 3,436 ushirika kufutwa

INATOKA UK. 5

havipo wala kujulikana vilipo vyama hivi vimetapakaa kwenye mikoa yote Tanzania Bara,"alisema Pia alifafanua kuwa asilimia kubwa ya vyama vinavyokusudiwa kufutwa vingi ni vya Ushirika wa Akiba na Mikopo ambavyo ni asilimia 73.8 ya vyama vyote. Alisema kuwa vyama hivyo vingi ni matokeo ya mfumo wa uwekezaji wa wananchi kuiuchumi ujulikano kama (Jk Fund) ambao ulilenga katika kuwezesha wananchi kiuchumi.

"Katika mpango huu wananchi walio wengi walianzisha Saccos, kwa lengo la kupata mikopo kutoka kwenye mfuko huo na vyama ambavyo havikupata mikopo havikuendelea na majukumu yake na hata vilivyopata baada ya kupata mikopo walitelekeza vyama vyao jambo ambalo lilipelekea kuwa na Saccoss, nyingi ambazo hazifanyi kazi," alisema.

Alibainisha aina ya vyama ambavyo vitafutwa kuwa Saccos 2,537, Amcos 264, Mifugo 82, Vyama vya Walaji 25, Huduma 72, Ufugaji Nyuki 17, Nyumba 8, Madini 23, Viwanda 102, Uvuvi 37, Umwagiliaji 31, Vyama vikuu 3, vinginevyo 235.

Aliitaja baadhi ya mikoa ambayo inaongoza kuwa idadi kuwa ya vyama hewa kuwa ni pamoja na Mwanza vyama 393, Pwani 335, Kagera 301, Morogoro 298, Arusha 282, Tabora 282, Kigoma 207, Mara 151, Tanga 136, Geita 119 na Iringa 92.

Wakati huo huo, Kamati ya Taifa ya Mbegu (NSC) imepitisha matumizi ya aina 40, mpya za mbegu bora zilizopendekezwa na kamati ya taifa ya kupitisha aina mpya ya mbegu (NVRC) kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya uzalishaji wa mbegu.

Waziri Hasunga alisema kufuatia hatua hiyo na baada ya kupokea ushauri wa kamati ya taifa ya mbegu na kwa mamlaka aliyonayo chini ya kifungu cha 12 cha Sheria ya Mbegu na 18 ya Mwaka 2003 na Marekebisho yake ya Mwaka 2014 ameidhinisha matumizi ya aina hizo mpya za mbegu kwa ajili ya uzalishaji wa mazao husika nchini.

"Mbegu hizo mpya zimefanyiwa utafiti na kugundulika kuwa zina sifa mbalimbali kama vile kutoa mavuno mengi, ukinzani dhidi ya magonjwa na kukomaa mapema, kupendwa na wakulima pamoja na walaji na zitaanza kuzalishwa na kutumika hapa nchini kwa mujibu wa sheria ya mbegu kunzia masimu wa 2019/2020," alisema Hasunga.

HABARI KITAIFA

# Waziri alaani wavamizi wa hifadhi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amelaani vikali vitendo vya baadhi ya watu walioanza kuvamia maeneo mapya ya Hifadhi za Misitu nchini kwa kuwazingira maofisa misitu kwa kuwapiga na wakati mwingine kuwasababishia vifo wakati wanapotekeleza majukumu yao.

Akizungumza leo wakati alipotembelea kukagua ujenzi wa ofisi na nyumba saba za watumishi zinazojengwa kwa gharama ya kiasi cha Sh. bilioni 1.3 katika shamba la miti Biharamulo lililopo katika Wilaya ya Chato mkoani Geita, Kanyasu alisema serikali imejipanga vilivyo kuwachukulia hatua kali za kisheria watu wote watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo. Alitaja mauaji ya askari wawili yaliyofanywa na wafugaji mwishoni kwa mwaka jana katika Msitu wa Hifadhi wa Isawima uliopo katika Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora kuwa yanarudisha nyuma juhudi za uhifadhi nchini

Pia, Kanyasu ameeleza tabia nyingine iliyozuka kwa baadhi ya watu kuanza kupiga mwano wanapowaona wahifadhi ikiwa ni ishara ya wananchi kujikusanya ili kuwadhuru wahifadhi hao, kuwa vitendo hivyo vinachagiza chuki baina ya wananchi na wahifadhi badala ya kujenga mahusiano mazuri baina yao.

"Nimeutaka uongozi wa Mkoa wa Tabora kuwasaka watu waliohusika na mauaji hayo popote walipo ili sheria ichukue mkondo wake.

Aidha, nimemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhakikisha wanawakamata wananchi wote waliovamia eneo la Nyabengo ndani Shamba la Miti la Biharamulo na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Alisema Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) haina misitu yake, bali inalinda misitu hiyo kwa niaba ya wananchi kwa ajili ya manufaa ya watu wote.

Katika hatua nyingine, Kanyasu amewatahadharisha watu hao kuacha tabia ya kuwazingira maofisa misitu kuwa ni hatari kwa vile wanakuwa na bunduki, na wanapozingirwa cha kwanza wanalazika kuilinda silaha, na pili kujilinda wenyewe.

"Tumeamua kuwapeleka maofisa misitu wote katika mafunzo ya kijeshi kwa muda wa miezi sita, ili waweze kupambana na watu wanaodhani kila sehemu wanaweza kulima na kuanzisha makazi," alisema Kanyasu.

"Katika kipindi cha uongozi wangu sitaki kusikia maofisa waliojitoa kulinda na kuhifadhi misitu yetu wakiendelea kuuawa na wananchi wenye tamaa ya kutaka kuendesha shughuli za kibinadamu ndani ya hifadhi, hakikisheni hali hiyo haijitokezi tena," alisisitiza Kanyasu.



Mratibu na Msimamizi Mkuu wa miradi ya ujenzi ambayo inatekelezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani jijini Dodoma, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, SSP Costantine Kiwone, akimweleza Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ramadhani Kailima (katikati) na maofisa wengine hatua mbalimbali za ujenzi wa nyumba za askari, Makao Makuu ya Polisi na makazi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) jijini Dodoma jana. **PICHA: VERONICA MWAFISI**

# Wazazi matatani kijana wao kumpa mimba mwanafunzi

**Na Hamisi Nasiri,** NEWALA

MKUU wa Wilaya ya Newala mkoani Mtwara, Aziza Mangosongo, ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuwakamata wazazi wa kijana ambaye anadaiwa kumpa ujauzito mwanafunzi wa kidato cha pili (jina linahifadhiwa) ambaye amebainika kupata ujauzito na kukatishwa ndoto ya maisha yake.

Mangosongo alitoa agizo hilo baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika Kijiji cha Makonga Kata ya Makonga ambako mwanafunzi huyo anaishi na wazazi wake, huku akiendelea kulea ujauzito wake.

Alisema licha ya serikali kukemea kila siku suala la wanafunzi kupewa ujauzito, lakini anashangazwa na jamii wilayani humo kuendelea kufanya mambo kama hayo.

Alisema baada ya kupata tetesi za tukio holo, aliamua kufanya ziara juzi usiku katika kijiji hicho anakoishi mwanafunzi huyo na wazazi wake na kuzungumza naye.

Alisema baada ya kuthibitisha kwamba mwanafunzi huyo ana ujauzito anavitaka vyombo vya ulinzi na usalama kuwakamata wazazi wa kijana ambaye alimpa mwanafunzi huyo ili waeleze wapi aliko kijana wao ili akamatwe.

Alisema wazazi hao kama hawatatoa ushirikiano wa kupatikana kwa kijana wao muhusika wa ujauzito huo, basi serikali itawafikisha wao mahakamani kwa niaba ya kujana wao.

Mangosongo alisema serikali haitovumilia kuona vitendo hivyo vinaendelea kufanyika wilayani Newala na badala yake itawachukulia hatua kali wahusika wa matukio hayo wakiwamo wazazi.

"Naagiza wazazi wa huyu kijana ambaye amesababisha mwanafunzi huyu kupata ujauzito wakamatwe mara moja waeleze kijana wao aliko ili sheria ichukuwe mkondo wake," alisema Mangosongo.

Alisema mwanafunzi huyo ameeleza kuwa alishawishika na kijana huyo na kuanzisha mahusiano kwa kununuliwa viatu, mtandio, sketi, blauzi na gauni, hivyo kukutana nae kimapenzi na kupata ujauzito.

Akizungumza, huku akitokwa na machozi, mwanafunzi huyo alisema kijana huyo alikuwa na tabia mara kadhaa ya kumshawishi kumtaka kimapenzi, lakini alikuwa akimkatalia.

Hata hivyo, alidai alishawishika kuanzisha mahusiano baada ya kununuliwa vitu hivyo, na baadaye kwenda nyumbani kwa kijana kufanya naye kitendo hicho na kujikuta akipata ujauzito.

# Watoto 3,494 waokolewa kukeketwa

**Na Rose Jacob,** TARIME

WATOTO wa kike zaidi ya 3,494 wameokolewa dhidi ya ukeketwaji ambao walitakiwa kufanyiwa mwaka 2018 na 2019 kutokana na jamii kuelimishwa juu ya madhara ya ukatili wa kijinsia.

Watoto hao waliokolewa na Shirika la Association for Termination of Female Genital Mutilation (ATFGM) Masanga, baada ya kuunda klabu 193 za haki za watoto katika shule za msingi na sekondari.

Mkurugenzi mtendaji wa kituo cha kulelea watoto ambao wamekimbia ukeketaji cha ATFGM Masanga, Sista Stella Mgaya, alisema watoto 434 ni Watanzania na 55 ni wa Kenya kwa mwaka 2019 ukiwajumlisha na watoto 3,005 wa mwaka 2018 ndio inafikia idadi ya 3,494.

"Tumekuwa tukishirikiana na serikali ya Wilaya ya Tarime na wadau wengine...tumefanikiwa kupeleka shule watoto 402 kati ya hao 150 wamefaidika na mafunzo ya ufundi, 180 shule za msingi na watoto 72 sekondari, ingawa tunakutana na ukinzani mkubwa kutoka kwa wazee wa kimila ambao wanaona asasi inaenda kinyume cha mila na desturi hasa kwenye suala la ukeketaji," alisema Sista Mgaya.

Aidha, alisema wanakumbana na changamoto ya baadhi ya wazazi kuwakataa watoto wao baada ya msimu wa kambi kuisha, na wengine wanapoenda majumbani huchelewa kurudi shuleni na wengine kushindwa kurudi shuleni kutokana na kufanyiwa ukeketaji.

"Baadhi ya vijana waliopokea elimu na kwenda tohara salama wamekuwa wakikamatwa na kupelekwa tohara ya kienyeji kwa mara ya pili, jambo ambalo limekuwa ni changamoto kubwa, hivyo baadhi ya wanajamii wanajenga uadui na taasisi," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Mtemi Msafiri, alisema serikali haitokubaliana na vikundi vya watu wachache wanaotaka kuleta madhara ndani ya jamii, na itawashughulikia wanaojihusisha na tohara zisizo salama.

# Wamabondeni watakiwa kuhama

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji wilayani Kahama mkoani Shinyanga limewataka wananchi waishio katika mabonde kuhama kwa muda kwa kuwa mvua zinazoendelea kunyesha zinaweza kusababisha maafa kutokana na mafuriko yanayojitokeza mara kwa mara kwenye makazi yao.

Hayo yalisemwa na Kamanda wa Jeshi hilo, Inspekta Duma Mohamed, wakati akizungumza na Nipashe, siku chache baada ya kutokea mafuriko katika mitaa ya Mhongolo, Sokola na Nyakato Mtakuja mjini Kahama, na kusababisha maji kujaa kwenye makazi ya watu.

Alisema katika mvua zilizonyesha hivi karibuni mjini Kahama idadi kubwa ya nyumba zilizoingiliwa na maji walishindwa kutoa msaada kwa wakati kutokana na kutokuwapo kwa miundombinu rafiki ya kuyafikia makazi hayo.

Duma alisema hali hiyo imetokana na wananchi kujenga makazi holela yasiyofuata misingi ya ujenzi wa makazi ambapo wengi wao wamejenga kwenye njia za maji, na kwamba njia pekee ni wananchi hao kuhama ili kutoendelea kuathirika.

Happynes Charles, mkazi wa Sokola Kata ya Majengo, alisema mafuriko yanayotokea yanasababishwa na daraja lililojengwa katika mtaa wa Mhongolo kuelekezea maji kwenye makazi ya watu na kwamba suala la kuhama linahitaji msaada wa serikali.

Naye Juma Idd na Janeth John walisema suala la kuhama kwenda kuishi sehemu ambayo haina mafuriko ni gumu kutokana na wengi wao wameshajenga makazi ya kudumu na kwamba serikali haina budi kujenga mitaro ya uhakika kutoka kwenye daraja lililojengwa katika mtaa wa Mhongolo hadi la Lyanzugu lililopo katika mtaa huo.

Mitaa ya Sokola, Majengo, Malunga, Igomelo, Sango, Mayila na Nyakato Mtakuja ni miongoni mwa mitaa ambayo imekuwa ikiathiriwa mara kwa mara na mafuriko ya mvua kubwa zinaponyesha katika Mji wa Kahama.

# Wananchi walia bei ya chakula kupanda

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa Shinyanga Mjini wamelalamika kupanda kwa bei ya chakula, hali ambayo inasababisha baadhi yao hasa wenye hali duni ya kimaisha kukosa fedha za kununua chakula hicho na kushinda na njaa.

Hayo yalibainishwa juzi na Diwani wa Kata ya Chamaguha Manispaa ya Shinyanga, Mourice Mugini, kwenye ziara ya Mbunge wa Shinyanga Mjini, Stephen Masele, wakati akizungumza na wajumbe wa kamati ya siasa ngazi ya matawi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwenye kata hiyo.

Mugini alisema bei ya chakula Shinyanga imepanda kwa kasi, hali ambayo inasababisha baadhi ya wananchi kushindwa kumudu kununua, hivyo kushinda na njaa, na kumwomba Mbunge Masele aangalie namna ya kuitatua changamoto hiyo ili chakula kishuke bei kuokoa maisha ya wananchi.

"Mbunge wetu changamoto kubwa ambayo inatukabili hivi sasa wananchi wa Kata ya Chamaguha na Shinyanga kwa ujumla ni kupanda kwa bei ya chakula, mfano, kilo moja ya unga inauzwa kuanzia Sh. 1,300 hadi Sh. 1,500 kutoka Sh. 1,100, mchele unauzwa 1,700 hadi 1,800 kutoka 1,500," alisema Mugini.

"Kutokana na kupanda kwa bei ya chakula, kuna baadhi ya wananchi hasa wale wenye hali duni ya maisha, wamekuwa wakishindwa kununua chakula na kushinda na njaa, hivyo kutokana na wewe mbunge wetu upo hapa jimboni tunaomba uangalie namna ya kusaidia agalau bei ya chakula ishuke," aliongeza Mugini.

Naye Masele ambaye ni Makamu wa kwanza wa Bunge la Afrika, aliahidi kuzungumza na serikali na mamlaka zingine zinazohusika na chakula ili kuona namna wafanyabiashara watakavyopata nafaka kwa bei nafuu, ili nao wapunguze bei ya chakula kuwa chini ambayo kila mwananchi ataweza kuimudu.

Aidha, aliahidi kuendelea kushirikiana na wananchi pamoja na serikali, ili kuhakikisha analeta maendeleo katika mji wa Shinyanga ambao kwa sasa unakua kwa kasi kimaendeleo baada ya uboreshaji wa huduma muhimu ikiwamo umeme, majisafi na salama, miundombinu ya barabara kiwango cha lami.

Mfanyabiashara wa Shinyanga Mjini, Bahati Mathias ambaye anauza chakula dukani, alisema bei ya chakula imepanda kutokana na wao kununua nafaka kwa gharama kubwa kutoka kwa wakulima.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akizungumza na baadhi ya makandarasi wa Shirika la Nyumba ya Taifa (NHC), baada ya kukagua ofisi na nyumba saba ambazo kukamilika kwake zitagharimu kiasi cha Sh. bilioni 1.3 katika Shamba la Miti Biharamulo lililopo Wilaya ya Chato mkoani Geita. Wengine ni watumishi wa shamba hilo. **PICHA: LUSUNGU HELELA**

# Wafugaji wakaidi kuosha mifugo kukiona

**Na Jumbe Ismailly,** DODOMA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imeziagiza kamati za majosho kutunga sheria ndogo zitakazosimamia na kuwadhibiti wafugaji wanaokwepa kupeleka mifugo yao kuogesha kwa lengo la kukabiliana na magonjwa yatokanayo na kupe.

Agizo hilo limetolewa na Kaimu Ofisa Mfawidhi kituo cha uchunguzi wa magonjwa ya mifugo Kanda ya Kati, Dk. Samuel Mngumi, wakati wa uzinduzi wa awamu ya pili ya kampeni za uogeshaji mifugo Kanda ya Kati uliofanyika katika Kijiji cha Mkoyo, Kata ya Hombolo, mkoani Dodoma.

Alisisitiza kwamba kamati za majosho ndiyo moyo wa majosho na shughuli nzima za uogeshaji, hivyo waweke sheria ndogo za kuwajibishana ili utaratibu wa kuogesha uwe endelevu. Dk. Mngumi alisema kwamba anaamini kuwa kila halmashauri imetunga sheria zake ndogo kwa baadhi ya wafugaji wachache wanaokaidi kupeleka mifugo yao kwenda kuogesha wanavyoshughulikiwa ili wasiwakatishe tamaa wafugaji wengine wenye moyo wa kupambana na magonjwa yanayotokana na kupe.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, kuna sheria nyingi zinazoongoza udhibiti wa magonjwa ya mifugo kwa sababu magonjwa yanasababishwa na vitu vingi na kutoa mfano wa sheria ya magonjwa ya wanyama ya mwaka 2003 inayoeleza kwamba ni lazima watu washiriki katika kudhibiti magonjwa.

Alieleza kuwa baada ya serikali kuona kwamba upo uwezekano kwa baadhi ya wafugaji kuwa wazito kutekeleza agizo hilo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo katika hatua za mwisho za kutoa kanuni za udhibiti wa magonjwa ya mifugo kwenye baadhi ya maeneo.

"Kwa mfano kuna kanuni ya kuogesha itatoka, na itazungumzia habari za kuogesha tu, kwamba mtu asipoogesha kuna mambo gani yatafanywa, mtu afanyweje na kadhalika, lakini kuna kanuni nyingi kulingana na juhudi za kudhibiti magonjwa," alibainisha.

Naye daktari wa mifugo wa Jiji la Dodoma, Innocent Peter, alisema kwamba tangu kampeni ya uogeshaji zilipoanza zimepunguza matukio ya magonjwa yanayotokana na kupe kulinganisha na kabla ya kampeni hiyo kuanza.

Alisema hivi sasa matukio ya magonjwa yatokanayo na kupe kwa ng'ombe na mbuzi yamepungua kutoka 30 kwa mwezi yalivyokuwapo kabla ya kampeni hadi matukio kati ya matano hadi 10 kwa mwezi kwa maeneo ya vijijini wakati kwa wafugaji wa maeneo ya mjini simu walizokuwa wakipigiwa na wafugaji wao zimepungua.

Mmoja wa wafugaji waliohudhuria uzinduzi wa kampeni hiyo, Yoro Losiwa, alisema kwamba kampeni hiyo ni nzuri kwani inalenga kupunguza na kama siyo kutokomeza kabisa magonjwa yatokanayo na kupe.

Mwenyekiti wa serikali ya Mtaa wa Mkoyo, Benjamini Lebolo, alishukuru serikali kwa kuliona suala la majosho ambalo linalolenga kupunguza na kama siyo kumaliza kabisa vifo vya mifugo.

# Hospitali yanunua CT Scan ya kisasa

**Na Allan Isack,** MANYARA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri ya Tanzania (KKKT) ya Haydom wilayani Mbulu mkoani Manyara, inayohudumia wagonjwa zaidi ya 120,000, kwa mwaka, imenunua mashine mpya ya kisasa ya uchunguzi ya mionzi (CT Scan).

Kwa takribani miaka miwili hospitali hiyo haikuwa ikitoa huduma hiyo, kutokana na kuharibika. Kwa mwaka uhudumia zaidi ya wagonjwa 105,296, wa nje na 14,020, wa ndani wa mikoa ya Manyara, Arusha, Tabora, Singida, Dodoma na Simiyu.

Mkurugenzi wa Tiba wa hospitali hiyo, Dk. Emmanuel Nuwass, akizungumza alisema Sh. milioni 800 zimetumika kuinunua mashine hiyo, Ujerumani na kuisafirisha. Dk. Nuwass, alisema awali mashine waliyokuwa nayo iliharibika miaka miwili iliyopita, hivyo wagonjwa wengi walikosa huduma ya vipimo hivyo.

Alisema kutokana na ukosefu wa mashine hiyo, iliwabidi watu wa eneo hilo kufuata vipimo kwenye hospitali za kanda ikiwamo Hospitali ya KCMC iliyopo mkoani Kilimanjaro na Bugando mkoani Mwanza. Alisema mashine hiyo itasaidia wagonjwa wengi hususani wale wasio na kipato kupata vipimo kwenye eneo la karibu.

Catherine Faustine, mkazi wa eneo hilo alisema wananchi wengi wameshindwa kupata huduma hiyo, kutokana na umbali mrefu wa kufuata huduma hiyo katika hospitali nyingine kubwa. "Kuna baadhi ya watu walifariki kwa sababu hawana fedha za kwenda kupimwa katika hospitali za mbali ikiwamo KCMC iliyopo Manispaa ya Moshi au Muhimbili Dar es Salaam, hivyo, tunashukuru kwa kupata mashine hii," alisema.

Mtaalamu wa Mionzi wa hospitali hiyo, Paulo Fissoo, alisema mashine hiyo ina uwezo mkubwa zaidi tofauti na ile ya awali iliyoharibika.

Hospitali ya Haydom inayomilikiwa na KKKT Dayosisi ya Mbulu, ilianzishwa na wamisionari wa Norway mwaka 1955 ikiwa na vitanda 50 na sasa ina vitanda 420.

Wagonjwa wanaopata huduma katika hospitali hiyo wanatoka wilaya za Mbulu, Hanang na Babati mkoani Manyara, Karatu mkoani Arusha, Igunga mkoani Tabora, Iramba na Mkalama mkoani Singida, Kondoa mkoani Dodoma na Meatu mkoani Simiyu.



Ofisa Lishe wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Silvania Kullaya, (aliyekaa chini akiwa amempakata mtoto) akimlisha chakula chepesi mtoto, mtoto huyo ni mmoja ya waliopelekwa kufanyiwa uchunguzi kuhusu lishe katika Kijiji cha Usari, wilayani hapa juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wakulima watakiwa kuenzi matumizi ya mbegu za asili

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KATIBU Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, amewataka wakulima nchini, kuenzi matumizi ya mbegu za asili ili kuepukana na tishio la kutoweka kwa mbegu hizo, kutokana na mwingiliano wa matumizi ya mbegu za kisasa zinazoendelea kushamiri kwa wingi.

Rai hiyo aliitoa wakati wa kufungua maonyesho ya mbegu na vyakula vya asili yaliyoandaliwa na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) yaliyofanyika wilayani Karatu. Mafunzo hayo yaliwakutanisha wakulima kutoka mikoa mbalimbali, na kuambatana na maandamano ya kuonyesha mbegu za mazao ya asili.

Aidha, alisema tatizo linalokabili mfumo wa mbegu ni wataalamu kutokufika kwa wakati kwa wakulima kutoa uratibu wa usambazaji wa mbegu, kitendo hicho kinasababisha wakulima wengi kutumia mbegu za kisasa zaidi kuliko za asili. Alisema kupungua kwa uhifadhi wa mbegu unasababishwa na ukame hivyo, aliwataka wakulima kutumia maonyesho hayo kupanua wigo kwa wakulima kutatua tatizo la utumiaji na upatikanaji wa mbegu za asili.

Mratibu wa MVIWATA Mkoa wa Arusha, Richard Masandika, alisema kupitia mradi wa kilimo endelevu, sheria ya mbegu ya mwaka 2016, imekuwa kikwazo kikubwa kwa wakulima katika kutekeleza mfumo wa mbegu za asili. Aliiomba serikali kutazama upya sheria hiyo ili matumizi ya mfumo usio rasmi utambulike na kufufua matumaini mapya kwa mkulima.

Alisema wadau wa kilimo endelevu waliamua kuwasaidia wakulima kupunguza kero ya upatikanaji wa mbegu kwa kufufua mfumo wa matumizi ya mbegu za asili ambao wakulima wengi wanautumia kwa kuhamasisha uhuru wa mbegu. Mwenyekiti wa (MVIWATA), John Safari, aliiomba serikali kutambua mfumo wa mbegu usio rasmi ili wakulima wapate uhuru wa matumizi yanayokubalika kwa kuwa sheria za mbegu nchini hazitambui mbegu za asili.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi waliohudhuria katika maonyesho hayo, Anastazia Tuta alipongeza hatua ya uandaaji wa maonyesho hayo, na kuiomba serikali kuzitambua mbegu za asili na kuweka sheria ya uandaaji wa mfumo ulio rasmi kwa kuwa mbegu hizo hazitumii gharama kubwa kama mbegu nyingine.

# Pampu umwagiliaji zanufaisha 15,000

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAKULIMA zaidi ya 15,000 wa mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Singida, wataondoka na adha ya kusubiri kilimo cha msimu wa mvua baada ya kampuni ya IYO ya jijini Arusha, kuanza kusambaza pampu za umwagiliaji maji, zinazotumia nishati ya jua katika maeneo ya mikoa hiyo.

Mkurugenzi wa Masoko na Uendeshaji wa Kampuni ya IYO Solar Pump Group, Abdull Sariko, alisema bodi ya wakurugenzi ya kampuni hiyo, imelenga zaidi kumkomboa mkulima wa hali ya chini kulima kisasa kwa kutumia pampu za jua kumwagilia mashamba na gharama yake ni nafuu na imemlenga mkulima wa hali ya chini.

"Pampu hizi tumeshasambaza kwa wakulima zaidi ya 15,000, tunaamini itakuwa njia mojawapo ya kumwondoa mkulima katika kilimo cha kizamani kwenda katika kilimo cha kisasa na kuacha kutegemea kilimo cha mvua pekee yake, ambacho hakina uhakika hasa wakati huu wa mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Sariko alisema uwezo wa pampu hizo ni mkubwa kwa kuwa ina uwezo wa kusambaza maji lita 40,000 kwa sasa na kilio cha wakulima kutegemea mvua... kwa sasa itakuwa historia na nchi itakuwa na mavuno ya kutosha ya chakula katika maeneo ya mikoa hiyo na mingine.

Alisema kampuni imejikita katika mikoa hiyo, na lengo ni kusambaa mikoa mbalimbali ikiwa ni mojawapo ya njia ya kuisaidia serikali kuboresha kilimo kuwa cha kisasa.

''Tumeshasambaza pampu hizi katika wilaya za Same, Mwanga, Simanjiro, Arumeru, na Singida na mahitaji ni makubwa sana, lakini tutajitahidi kukidhi mahitaji hayo,'' alisema Sariko.

Mmoja wa wakulima, Obed Mawalla, alisema ameshanunua pampu hiyo, na ameipeleka kijijini kwao Marangu mkoani Kilimanjaro na inafanya kazi vizuri ya kumwagilia mahindi na migomba, na kwamba imestawi tofauti na awali alipokuwa akitegemea mvua.

Alisema pampu hizo ni mkombozi wakulima kuacha kutegemea mvua.

Elias Qarro, mkazi wa Karatu aliitaka serikali kuipa sapoti kampuni hiyo ili ziwasaidie wakulima katika kilimo cha kisasa kuliko kutegemea mvua peke yake.

Qarro alisema amenunua pampu hiyo, na ameona matunda yake na iwapo wakulima nchini watazinunua, sekta ya kilimo itainuka na serikali haitakuwa na taabu katika suala la chakula.

Meneja Masoko ya Kampuni ya Iyo Solar Pump, Anna Mchome, alisema kampuni hiyo, imejipanga kusambaza mashine maji ziwamfikie wakulima na wafugaji.

Mchome alisema, mbali ya wakulima pia wafugaji watanufaika na mashine hizo kwa kuwa mifugo itapata maji kwa wingi na kilio cha wafugaji kwenda kulisha na kunywesha mifugo katika vyanzo vya maji itakuwa historia.





# Washangaa ujenzi kukwama miaka 7

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WANANCHI wa Kijiji cha Sinai, Kata ya Ormelili, Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, wameeleza kushangazwa na ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho kukwama kukamilika kwa zaidi ya miaka saba sasa.

Kutokana na mkwamo huo, baadhi ya wakazi wa kijiji hicho wamedai kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 15 kufuata huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Siha iliyopo eneo la mji mdogo wa Sanya Juu.

Walieleza masikitiko yao juzi, wakati Mkuu wa Wilaya hiyo, Onesmo Buswelu, alipotembelea kijiji hicho na kwenda kukagua maendeleo ya ujenzi wa zahanati hiyo.

Mmoja wa wakazi wa Sinai, Gloriana Shoo, alisema mkwamo katika ujenzi wa zahanati hiyo umewafanya watumie siku nzima kufuata huduma ya afya Sanya Juu na hivyo shughuli nyingine kama uzalishaji mali kusimama kwa sababu ya kukosa muda.

"Mimi binafsi naumia kusafiri muda mrefu, ninachoomba sasa hivi ni serikali itusaidie kusukuma ujenzi huu ukamilike mwaka huu na ikiwezekana kabla ya sikukuu ya Pasaka. Ukienda Sanya Juu mpaka urudi Sinai ni siku imeisha hiyo na huwezi kufanya kazi nyingine ya kukuingizia kipato," alieleza Shoo.

Naye Jafari Mwalisu, mkazi wa kijiji hicho alieleza kuwa baadhi ya wa wananchi wanatembea umbali mrefu kufuata huduma ya afya ikiwamo kliniki kwa kinamama, huku wakitumia gharama kubwa za usafiri.

"Unaweza kutumia zaidi ya Sh. 30,000 katika nauli kwa usafiri wa pikipiki maarufu kama bodaboda au pikipiki ya matairi matatu (bajaji) kwa nyakati za usiku kwa ajili ya kukupeleka hospitali ya wilaya. Hizi ni gharama kubwa kwa wananchi, ombi letu kwa serikali itusaidie kusogeza huduma hiyo hapa, kwa sababu wanaoumia zaidi ni wanawake na watoto," alisema Mwalisu.

Awali Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kilusu, Jacob Mollel, alisema ujenzi wa zahanati hiyo ulianza rasmi mwaka 2012, hadi kufikia sasa fedha zilizotumika ni Sh. milioni 59 ambazo zilitolewa na serikali kuu.

Mwalisu alisisitiza kuwa makisio ya ujenzi wa mradi huo yanaonyesha ili kukamilisha kwa zahanati hiyo kuna hitajika kiasi cha Sh. milioni 136.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, zahanati hiyo imeshapauliwa na kupigwa bati, lakini bado vitu mbalimbali ili kukamilika ikiwamo madirisha, milango, ujenzi wa choo, nyumba za watumishi na uzio.

Akijibu ombi la wananchi wa Sinai, Mkuu wa Wilaya hiyo, Onesmo Buswelu, alisema hatua za ukamilishaji wa mradi huo, upo katika dakika za lala salama na kwamba serikali imedhamiria kuona zahanati hiyo inaanza kutoa huduma ifikapo Februari mosi, mwaka huu.

# Kamati kuchunguza udanganyifu mradi wa maji

**Na Godfrey Mushi,** SAME

SERIKALI imeunda kamati maalumu kuchunguza madai ya udanganyifu katika utekelezaji wa mradi wa maji wa Vumari, unaotarajiwa kuhudumia vijiji 10 vilivyopo katika Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro.

Uamuzi wa kuundwa kamati hiyo, unatokana na taarifa kuwa mradi umekamilika kwa asilimia 80 na vitongoji vinavyopata huduma kwa sasa ni saba kati ya 10, huku taarifa za serikali zikionyesha uhalisia wa kitongoji kilichofikiwa na mradi huo ni kimoja pekee. Taarifa kuhusu kuanza kwa uchunguzi huo, ulithibitishwa jana kwa njia ya simu na Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule.

"Nimeipa kamati ya uchunguzi muda wa siku tano kuja na majibu, hata hivyo niliwaambia wahusika kwamba haiwezekani tukavumilia, tayari tumechukua hatua kunusuru mradi wa maji wa Vumari ambao unatekelezwa kwa fedha za serikali.

"Kimsingi huo mradi ulikuwa wa vijiji 10 na ulikuwa ukitekelezwa kwa fedha za umma tangu wakati wa utawala wa serikali ya awamu ya nne na mpaka serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk. John Magufuli, unaingia madarakani hadi kufikia sasa mradi huo haujaisha kwa wakati."

Kwa mujibu wa Senyamule, uamuzi wa kuchukua hatua ili kujiridhisha na kubaini chanzo cha tatizo hilo, unatokana na malalamiko ya wananchi wa Vumari kuiomba serikali kuchukua hatua za haraka kuunusuru usife.

Alisema alipigwa butwaa baada ya wananchi wa Vumari kumweleza kuwa wanashangaa kusikia mradi umekamilika kwa asilimia 80, wakati kati ya vitongoji saba vinavyotakiwa kupata maji, ni kitongoji kimoja pekee kinapata maji.

Alisisitiza Senyamule kuwa, "Mwisho wa siku wananchi wanataka maji, kwa hiyo hadithi za mchakato kwao si za muhimu kama maji hayatoka. Niwahakikishie tu wananchi wa Vumari kwamba nasubiri ripoti ya uchunguzi mezani na nitachukua hatua kwa yeyote aliyechelewesha utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa lengo la kuikwamisha serikali."

Mradi huo wa maji ulitengewa na serikali zaidi ya Sh. milioni 870 na kisha kukwama kwa zaidi ya miaka miwili kutokana na ukata wa fedha kufikia mwaka 2017.

Mradi huo ulisimama tangu Juni mwaka 2015 na ukaendelea tena mwaka 2017.

Kuchelewa kukamilika kwa mradi huo kunadaiwa kusababisha wananchi zaidi ya 3,700 kupoteza muda mwingi kutafuta maji, badala ya kufanya shughuli za kiuchumi.



Askari wa Jeshi la Kujenga Taifa Kitengo cha Uzalishaji (Suma-JKT) Kanda ya Nyanda za Juu wakisaidia kupakia kwenye gari mabati yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kwa ajili ya kukamilisha vyumba vya madarasa katika halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

# Udhaifu usimamiaji miche wamkasirisha Mgumba

**Na Mary Mosha,** HAI

UDHAIFU katika usimamizi wa miche bora ya kahawa inayozalishwa na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa nchini (TaCRI), kwenda katika halmashauri za wilaya hadi kwa wakulima wa zao hilo 'umemchefua' Naibu Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba.

Ameielekeza taasisi hiyo kuacha utaratibu wa kutoa miche hiyo bila kuwapo mpango kamili wa ufuatiliaji. Naibu Waziri Mgumba alieleza hayo mwishoni mwa wiki, wakati alipofanya ziara ya kikazi ya siku moja mkoani Kilimanjaro. Kutokana na udhaifu huo, aliitaka TaCRI kuhakikisha kila anayekabidhiwa miche hiyo ya kahawa kutoa mawasiliano yake na eneo analoenda kuotesha ili iwe rahisi katika ufuatiliaji.

"TaCRI imekuwa ikizalisha miche chotara inayovumilia magonjwa kwa gharama kubwa, lakini kumekuwa na usimamizi usio na tija katika halmashauri na baadhi ya vyama vya msingi. Jambo hili halina afya kwa sababu hakuna matokeo chanya yanayopatikana kwa serikali kama inavyotarajiwa," alisema. "Hatuoni mabadiliko katika zao hili la kimkakati, kwa sababu bado uzalishaji ni tani milioni 48 hadi tani 60 kwa mwaka. Hii haitoshi tunatakiwa kuona mabadiliko zaidi katika zao hilo."

Alisema ni vizuri halmashauri kushirikiana na TaCRI kwa kuimarisha kitengo cha ufuatiliaji na usimamizi wa miche, kinakopelekwa na kujua idadi ya wakulima ili iwe rahisi kitengo hicho kuhakiki miche yote.

Akitoa ufafanuzi wa kitaalamu kuhusu kauli hiyo ya Naibu Waziri Mgumba, Mtafiti wa Usambazaji Teknolojia na Mafunzo wa TaCRI, Sophia Malinga, alisema sababu za kutokuwapo kwa mwitikio chanya wa miche wanayoisambaza, ni baadhi ya wakulima kutokuwa na uelewa wa namna ya utunzaji wa miche hiyo. "Ni kweli hakuna ufuatiliaji wowote unaofanywa baada ya wananchi kukabidhiwa na halmashauri, ndio maana miche hiyo hufa. Pia kuna baadhi ya wakulima hawaoni umuhimu wa kuitunza miche hiyo kwa sababu wamepewa bure," alisema Malinga.

Awali, akitoa taarifa ya uzalishaji wa miche, Mkurugenzi Mtendaji wa TaCRI, Prof. Deusdedit Kilambo, alisema ufinyu wa bajeti umechangia kuzalisha miche chini ya matarajio.

NIPASHE JUMATATU JANUARI 6, 2020

Nipashe Spotika




VIUNGO WAKABAJI WA5 BORA ZAIDI DUNIANI UK. 16&17




## ISIKUPITE

Kiungo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Yaya Toure, aliifungia Manchester City mabao 79, anatajwa kuwa ni moja ya viungo bora waliowahi kuichezea klabu hiyo katika kipindi cha miaka 10 iliyopita. Nyota huyo alishinda mataji matatu ya Ligi Kuu England akiwa na City, mawili ya Kombe la Ligi na kabla ya kutua England, mwaka 2010 alishinda taji la La Liga akiwa na Barcelona.

# MSHIKEMSHIKE

Beki wa Barcelona, Gerard Pique (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya mshambuliaji wa Espanyol, Wu Lei, katika mechi ya Ligi Kuu Hispania iliyochezwa juzi usiku. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**



# UNITED, SOLSKJAER NA USAJILI WA JANUARI

**MANCHESTER,** England

MJADALA wa wachambuzi umekuwa mkubwa kuhusu nini Manchester United inachokitarajia kwenye usajili wa dirisha hili dogo la kipindi cha majira ya baridi Januari, nani ambaye watamsajili na nani ataondoka?

**NINI AMBACHO KOCHA AMESEMA?**

"Tunaendelea kwenda katika njia ambayo ni sahihi," alisema Ole Gunnar Solskjaer kabla ya kikosi chake kucheza na Manchester City Desemba mwaka jana.

**"Tunajua nini tunachokitaka kuimarisha kikosi chetu kuwa kipana na chenye ubora. Tumesajili wachezaji watatu wazuri zaidi kwa uhakika kabisa.**

"Tumepata wachezaji vijana, lakini bado kikosi kinahitaji kuwa kipana zaaidi hasa unapofikiria kuhusu majeruhi wote tulionao, na kushindwa kuwa kwenye kiwango chetu.

"Lakini wakati tukipata wapya nina uhakika kwamba pengo hilo tutakuwa tumeliziba.

"Naona kama nitatumia mamilioni ya pauni kwa wachezaji ambao hatuna uhakika nao? Kama nilivyosema, tunahitaji kujijenga upya kikosi, tunahitaji kubadilisha utamaduni.

"Tunataa utamaduni wa njaa na mafanikio binafsi ambayo wachezaji wengi wao wanayaonyesha.

"Una mtu kama (Scott) McTominays na (Marcus) Rashfords na (Jesse) Lingards, wachezaji ambao wanaijua Manchester United ilivyo."

**NINI AMBACHO MANCHESTER UNITED ILIKIFANYA KIPINDI CHA MAJIRA YA JOTO?**

Ole Gunnar Solskjaer aliwaleta wachezaji watatu kwenye usajili wake, Daniel James kutoka Swansea (kwa pauni milioni 15), Harry Maguire kutoka Leicester (kwa pauni milioni 80) na Aaron Wan-Bissaka kutoka Crystal Palace (kwa pauni milioni 45).

**NANI WAMEKUWA WAKIHUSISHWA NAO?**

Gedson Fernandes (Benfica), Danny Loader (Reading); Jadon Sancho (Borussia Dortmund), Eduardo Camavinga (Rennes); Dejan Kulusevski (Atalanta), Dries Mertens (Napoli); Christian Eriksen (Tottenham), Emre Can (Juventus); Arturo Vidal (Barcelona), Jack Grealish (Aston Villa), Moussa Dembele (Lyon), Ricardo Pereira (Leicester) na Richarlison (Everton).

**NANI ANAWEZA KUONDOKA?**

Nemanja Matic (Atletico Madrid); Matic (Inter Milan); Chris Smalling (Juventus na Inter Milan); Paul Pogba (Real Madrid na Juventus).

Kuhusu Paul Pogba, ambaye alionyesha wazi anataka kuondoka wakati wa kipindi cha majira ya joto kilichopita, akitajwa kuwaniwa na Real Madrid, ambao walikuwa wapo tayari kutoa pauni milioni 150 ada iliyokuwa inahitakiwa na United kwa Mfaransa huyo.

Nemanja Matic anaonekana kuwa ndiye mchezaji mwenye nafasi kubwa zaidi ya kuondoka, kwa sababu kwa sasa hana namba kwenye kikosi cha kwanza na klabu kadhaa zimeonyesha nia ya kutaka saini yake. Na hivyo kwa uhakika anaweza kuondoka.

Na Manchester United wanamuona kiungo wa Benfica, Gedson Fernandes kuwa ndiye anayeweza kuziba pengo lake katika kikosi hicho.

Wachezaji wengine ambao wanaonekana ni wazi kwamba wanaweza kuondoka kwenye kikosi hicho ni pamoja na Marcus Rojo na Eric Bailly ambaye ndiyo kwanza amerudi kutoka majeruhi pamoja na Timothy Fosu-Mensah.

Hata hivyo, kocha huyo anaonyesha kwamba hataki kuwatoa wachezaji hao kwa mkopo, kwani lengo lake ni kuwauza ili yeye aweze kubakia na wachezaji wenye damu changa kikosini mwake."

**JE, WAJUA?**



MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah, amefunga zaidi ya mabao 202 kwa nchi yake na klabu yake ya Liverpool katika kipindi cha miaka 10. Nyota huyo kwao Misri anaitwa Mfalme.

## MICHEZO



# YANGA ILIPOTUMIA MBINU ZA UD SONGO KUIBANA SIMBA

Kiungo wa Yanga, Papy Tshishimbi (katikati), akijaribu kuwatoa wachezaji wa Simba, Muzamiru Yassin (kushoto) na Shomary Kapombe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Na Adam Fungamwango**

DAKIKA 90 za mechi ya watani wa jadi kati ya Simba na Yanga zilimalizika kwa ubao ukisomeka 2-2, huku mashabiki wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Wekundu wa Msimbazi wakiwa hawaamini macho yao.

**Umati wa mashabiki wa Simba uliofurika kwenye Uwanja wa Taifa na kuwafunika wenzao wa Yanga, si tu kwamba waliamini kuwa watashinda, lakini hawakuamini kuwa watani zao wa jadi watarudi sha mabao yote mawili, baada ya kuongoza.**

Yalikuwa ni magoli ya Meddie Kagere kwa mkwaju wa penalti na Deo Kanda, lakini baadaye Mapinduzi Balama na Mohamed Issa 'Banka' walisawazisha magoli hayo.

Zipo sababu nyingi za kisaikolojia na kiufundi ambazo zilisababisha sare hiyo tofauti na watu walivyofikiri.

Kwanza kabisa Yanga ilipofika nje ya jengo la Uwanja wa Taifa walichukua muda mrefu kushuka kwenye gari. Walipoingia uwanjani, wachezaji wa Yanga walikata kona kuelekea upande wa Kaskazini mwa uwanja walipokuwa wachezaji wa Simba na wakakata kona kwenye kibendera cha upande wa Kaskazini Magharibi mwa uwanja, na kuingia uwanjani kurejea upande wao wa Kaskazini.

Walifanya hivyo badala ya kuingia na kukata kona kuelekea upande wa kusini moja kwa moja.

Yanga ilifanya mbinu hii ambayo ilitumiwa na UD Songo ya Msumbiji mwaka jana kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na mechi ikaisha kwa sare ya bao 1-1, Simba ikatolewa kwenye michuano hiyo. Hii ni mbinu ya kisaikolojia ambayo ilianza kuwatisha mashabiki wa Simba waliokuwa uwanjani kabla hata mechi haijaanza.

### 1. WACHEZAJI WA SIMBA WALIJIAMINI ZAIDI

Baada ya sababu za kisaikolojia zilizosababisha mechi hiyo imalizike kwa sare, sasa zinafuatia sababu za kiufundi ambazo moja ni kwamba wachezaji wa Simba walionekana kujiamini kupita kiasi.

Waliamini uwezo wao na walidhani watautawala zaidi mchezo kuliko wapinzani hao, hivyo kuwaweka kwenye wakati mgumu. Ilikuwa hivyo kipindi cha kwanza, lakini kipindi cha pili Yanga iliamka na kwa kipindi kirefu ilitawala mchezo, hasa katikati ya uwanja.

Wachezaji wa Simba hawa viungo nadhani hawakujiandaa kukutana na hali hiyo, hivyo walionekana kuchanganyikiwa na kupotezana.

### 2. YANGA ILICHEZA KITIMU ZAIDI

Labda kwa kutambua kuwa hawakuwa na wachezaji mmoja mmoja mwenye uwezo mkubwa kuliko wenzao, wachezaji wa Yanga kwa asilimia kubwa walicheza kitimu zaidi.

Walikaba kwa pamoja na wakienda mbele wanaenda kwa pamoja. Mastraika wao na mawinga walikuwa na uwezo wa kukaa na mpira na kuwasubiri wenzao wapande na wakati wa kuzuia walirudi nyuma mara moja.

Mbinu hii iliwasaidia kwa kiasi kikubwa, tofauti na wenzao wa Simba ambao walikuwa wanategemea zaidi viungo wao kupeleka mashambulizi.

### 3. VIUNGO SIMBA WALIINGIA KWENYE MTEGO

Viungo wa Simba Jonas Mkude, Mzamiru Yassin, Cleotus Chama kwa kiasi kikubwa walichangia timu yao kutopata ushindi kutokana na kutobadilika kiuchezaji, baada ya kuingia kwenye mtego wa viungo wa Yanga.

Hata goli la kwanza la Yanga lilitokana na tabia ya viungo wa Simba kutaka kukaa sana na mpira, kugeuka, kupiga chenga zisizokuwa za lazima na kutaka kuwaaminisha mashabiki wao kuwa wanajua kuuchezea mpira wanavyotaka.

Mzamiru alikuwa na mpira, huku wachezaji wenzake wakiwa tayari kupokea. Lakini alikaa nao kwa muda mrefu bila sababu akitaka kupiga chenga na kufanya madoido, kabla ya kunyang'anywa na Yanga kwenda kufunga bao la kwanza lililowarejesha mchezoni. Viungo wa Yanga, kina Mohamedi Issa, Mapinduzi Balama, Abdul-Aziz Makame, walihakikisha viungo wa Simba hawapati fursa sana ya kupeleka mipira mbele wakiwa huru.

Na kwa sababu udhaifu wa viungo wa Simba ni kukaa na mpira muda mrefu, huku wakiwa hawatumii nguvu na hawana uwezo wa kushindana nguvu mmoja kwa mmoja, walihakikisha wanakasi muda wote na wakafanikiwa.

### 4. KUUMIA KWA KANDA KULIIMALIZA SIMBA

Kuumia kwa winga Deo Kanda kwa kiasi kikubwa ndiko kulikoifanya mechi hiyo iende sare.

Kwenye mechi ya Jumamosi, Kanda alikuwa mwiba mchungu kwenye safu ya ulinzi wa Yanga kuliko mchezaji yoyote yule wa Simba. Baada ya kufunga bao la pili na kuumia, mchezaji huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), alitolewa nje.

Na baada ya hapo Yanga hawakuwa na tishio lolote lile, badala yake viungo wake badala ya kwenda kuwasaidia mabeki wa pembeni, waliingia zaidi kati ya kufanya kutawala dimba, mechi ikabadilika kabisa.

### 5. MANULA HAKUWA MCHEZONI

Kipa Aishi Manula Jumamosi iliyopita alikuwa kwenye siku mbaya ofisini. Aliruhusu magoli mepesi ambayo yanalalamikiwa sana na wanachama na mashabiki wa Simba.

Goli la kwanza ni aina ya magoli ambayo Manula huwa anafungwa mara kwa mara na goli la pili, ni goli ambalo ilibidi afungwe kipa ambaye si mzoefu kwenye mechi za Ligi Kuu, achilia mbali mechi za Simba na Yanga.

Ilibaki kidogo afungwe goli lingine la kizembe, kama si Paschal Wawa kuokoa na kuwa kona, kabla ya kuanza kumlalamikia.

### 6. MAPINDUZI NYOTA WA MCHEZO

Kiungo wa Yanga, Mapinduzi Balama alionyesha uwezo mkubwa kwenye mechi hiyo. Licha ya uchanga wake na kuwa ni mechi yake ya kwanza kubwa ya Simba na Yanga, aliwafunika viungo wazoefu wa Simba kina Mkude, Chama na Mzamiru. Na mchezaji huyo huyo ndiye aliyemnyang'anya mpira Mzamiru na kwenda kufunga bao la kwanza.

## NJE YA UWANJA

KIKOSI cha Manchester United kilichelewa kufika kwenye Uwanja wa Molineux, ikiwa ni saa moja kabla ya mechi ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya wenyeji Wolves. Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer, amewatupia lawama askari wa barabarani kwa kushindwa 'kusafisha' njia ili kuruhusu timu yao kufika mapema katika mechi hiyo iliyochezwa Jumamosi na kumalizika kwa sare ya bila kufungana. Pia kocha huyo alililalamikia ubovu wa vyumba vya kubadilishia nguo vya klabu hiyo.



## Extra Time

# VIUNGO WAKABAJI WATANO BORA ZAIDI DUNIANI

**LONDON,** England

UMUHIMU wa kuwa na kiungo mkabaji ni hitaji la lazima kwa timu katika soka la kisasa. Kiungo mkabaji anachukuliwa kama ndio 'ngao ya ulinzi' ya timu na mara zote amekuwa 'mkataji' wa mashambulizi kwenda kwenye lango lake.

**Siku hizi nafasi hii imekuwa msaada mkubwa kwa walinzi na nafasi yao ni kucheza kwa kuwasaidia walinzi na pia wakiwa na nafasi ya kutengeneza mashambulizi.**

Viungo kama Claude Makelele, Patrik Vieira, Frank Rijkaard na Roy Keane walishaonyesha kile walichokuwa nacho kwenye nafasi ya kiungo mkabaji wakati wao wa uchezaji na kuzisaidia timu zao kutwaa mataji mbalimbali.

Majina ya wachezaji hao ndio kwa kiasi kikubwa yameonyesha umuhimu wa kiungo mkabaji na mwenye uwezo wa kukaa na kugawa mipira sehemu mbalimbali na pia kuliwalisha washambuliaji wake.

Kwa wakati huu kuna wachezaji kadhaa wameonekana kuwa na mafanikio kwenye nafasi hiyo. Na mara nyingi wachezaji wa nafasi hii huonekana kuwa ndio viongozi wa timu.

Makala hii inawaangalia viungo wakabaji watano ambao ndio bora zaidi kwa soka la sasa duniani:

### 5. RODRI (MANCHESTER CITY)

Huyu ni mchezaji mwenye umri wa miaka 23, raia wa Hispania na amekuwa nguzo muhimu kwa kikosi cha Manchester City kwenye safu ya kiungo mkabaji pale kati tangu alipotua hapo akitokea Atletico Madrid kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Akitarajiwa kuwa ndiye mrithi wa muda mrefu wa Fernandinho, Rodri amekuwa na uwezo wa kukaba kukaa na mpira na kutengeneza pasi zenye macho, huku pia akiwa na uwezo wa kusukumiza mashambulizi mbele.

Akiwa amecheza mechi 16 kwa City, takwimu zake zinaonyesha kwamba ana wastani wa kukaba wa 2.5, huku akiwa na pasi zenye uhakika wa asilimia 93. Katika umri wake wa miaka 23, ameonyesha kwamba anaweza kuimarika zaidi na kuwa nguzo muhimu zaidi katika kikosi cha timu hiyo kwenye safu ya kiungo kwa siku zijazo.

### 4. CASEMIRO (REAL MADRID)

Kiungo huyu wa kimataifa wa Brazil, Casemiro amekuwa nyuma ya mafanikio yote ya Real Madrid katika miaka ya hivi karibuni akijiimarisha yeye mwenyewe kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi wa safu ya kiungo mkabaji duniani kwa sasa.

Casemiro, ameshinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Madrid, na amekuwa mmoja wa wachezaji wenye kipaji kisichochuja chenye mwendelezo chanya kwa kipindi cha misimu kadhaa sasa.

Katika umri wake wa miaka 27 amecheza kila mechi kwenye Ligi Kuu Hispania, La Liga, msimu huu na amekuwa na uwezo wa kukaba wa kiwango cha 3.7.

### 3. SERGIO BUSQUETS ( BARCELONA)

Mmoja wa viungo wenye 'udambwi udambwi' mwingi zaidi wa wakati wote, Sergio Busquets ambaye historia itamkumbuka kwa miaka mingi kuwa ndiye mmoja wa viungo wakabaji bora zaidi kuwahi kutokea katika nafasi hiyo.

Mhitimu huyu wa chuo cha kulelea vipaji vya soka cha pale La Masia amekuwa kama nguzo muhimu wa Barcelona kwenye nafasi ya kiungo kwa miaka mingi. Amebarikiwa uwezo na kipaji cha aina yake na kutawanya mipira na kumiliki mpira akiwa eneo lake la kujidai. Raia huyu wa Hispania mwenye umri wa miaka 31 amecheza mechi 16 kati ya 18 msimu huu na anahitaji kuendelea kuwa kwenye kiwango chake bora ili Blaugrana hao waweze kutetea taji lao msimu huu.

### 2. FABINHO (LIVERPOOL)

Baada ya kuanza taratibu maisha ya soka pale kwenye dimba la Anfield, Fabinho sasa anaonekana kama ameonyesha ubora wake na mmoja wa wachezaji muhimu zaidi wa kikosi hicho kwenye safu ya kiungo.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 26 amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi kwa wekundu hao na uwezo wake sasa umemfanya kuanza katika mechi 11 chini ya kocha Jurgen Klopp msimu huu.

Alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu wakati Liverpool ikitwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na kiwango hicho ameendelea nacho msimu huu. Sio jambo la kushangaza haraka amekuwa mmoja wa wachezaji wanaovutiwa zaidi na mashabiki wa klabu hiyo.

### 1. N'GOLO KANTE (CHELSEA)

Anayependa kutabasamu wakati mwingi, N'Golo Kante anachukuliwa na wengi ndio kama kiungo mkabaji bora zaidi duniani kwa sasa.

Mfaransa huyu amekuwa kwenye kiwango kizuri katika ukabaji, kugawa pasi za uhakika, na kutengeneza mashambulizi mbele.

Alikuwa nguzo muhimu zaidi kwa Leicester City wakati wakitwaa taji la Ligi Kuu England msimu wa 2015-16 na akashinda tena mwaka uliofuata akiwa na Chelsea, na kumfanya kuwa mshindi mara mbili mfululizo wa taji hilo.

Katika umri wake wa miaka 28 amekuwa nguzo muhimu kwa Chelsea katika kuwasukumizia mbele mipira washambuliaji wake na pia kufunga mabao kwa jina lake.


Alikuwa nje ya dimba mwanzoni mwa msimu huu, lakini amerudi akiwa imara na ameonyesha kwa uhakika kabisa kile alichokuwa wanakimisi Blues hao.



N'GOLO KANTE

## Nukuu

"Mikel (Arteta), ni kocha mkubwa na anayeufahamu vema mpira wa miguu. Ni mchezaji mkubwa, anatuletea vitu vipya na ninaamini katika filosofia yake. Tunatarajia kufanya mambo makubwa ndani ya muda mfupi ujao, lakini tutaenda hatua kwa hatua, huwezi kubadilisha kutoka sifuri mpaka namba 10 kwa siku moja, wiki moja, mwezi mmoja," **alisema beki wa Arsenal, David Luiz.**



"Pengine tunaweza kumaliza katika nafasi ya saba au nane kwenye msimamo, lakini kwa sababu hatujaribu, mechi ziko pale na tulicheza vizuri, Nimehamasika na kiwango cha timu, wachezaji walionyesha ari nzuri na morali ya juu," **Pep Guardiola, Kocha wa Manchester City alisema baada ya mchezo dhidi ya Everton uliomalizika kwa kushinda mabao 2-1.**



"Peke yangu siwezi kufanya lolote, ninahitaji ushirikiano kutoka kwa wachezaji wenzangu ili tufikie malengo, kila siku ninaamini kujituma ili kuisaidia timu yangu iweze kufanya vema katika mashindano mbalimbali," **alisema kiungo wa kimataifa wa Yanga Mnyarwanda Haruna Niyonzima, baada ya kurejea katika klabu hiyo kwa mara ya pili.**



# MAGOLI NANE YA MBALI ALIYOTUNGULIWA MANULA




**Na Adam Fungamwango**

KIPA chaguo la kwanza wa Simba na Timu ya Taifa, (Taifa Stars), Aishi Manula, Jumamosi iliyopita alipata wakati mgumu kutoka kwa wanachama na mashabiki wa klabu yake kwenye Uwanja wa Taifa baada ya kufungwa moja ya mabao ambayo yanajirudia mara kwa mara.

**Baada ya mechi kumalizika na Simba kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Yanga licha ya kuongoza mabao 2-0, lakini yalirud ishwa kwa muda mfupi tu, mashabiki wa Simba wal ionekana kutoa 'povu' kwa Manula kuwa yeye ndiye aliyesababisha sare hiyo kwa sababu amefungwa magoli mepesi ambayo hayakupaswa kwa kipa wa aina yake.**

"Kila mara amekuwa akifungwa magoli ya aina hii hii, hivyo hajifunzi? Hivi makocha wa makipa Simba wanafanya kazi gani? Kwa nini mechi hii asingedaka Kakolanya (Beno)?"

Ni baadhi ya maneno yaliyosikika kutoka kwa mashabiki wa Simba walioonekana kuchukizwa na sare hiyo, wakiwaacha wenzao wa Yanga wakiserebuka kwa ngoma, shangwe na hoi hoi.

Ni kweli, rekodi zinaonyesha kuwa Manula tangu msimu uliopita ana udhaifu wa kufungwa magoli ya mbali ambayo mashabiki wa Simba wamekuwa wakilalamika mara kwa mara, lakini ni kama vile imekuwa ni donda ndugu lisilotibika.

Rekodi zinaonyesha kuwa amefunga magoli manane ya mbali, ukimjulisha na la Jumamosi tangu msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara, matano akifungwa msimu uliopita na msimu huu tayari ameshafungwa bao la tatu la aina hiyo.

Haya ndiyo baadhi ya magoli ya mbali ambayo Manula amekuwa akiruhusu na kuwakera mashabiki wa klabu yake.Kwa bahati nzuri kwake ni kwamba nyingi Simba imekuwa ikipata ushindi.

**1. SIMBA VS MTIBWA SUGAR (NGAO YA JAMII)**

Ilikuwa ni mechi ya Ngao ya Jamii, kufungua msimu wa Ligi Kuu 2018/19, Simba ikicheza dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Simba ilianza kupata bao dakika ya 29 lililofungwa na Meddie Kagere.

Kelvin Sabato akiwa umbali ya mita 30, aliachia mkwaju wa mbali uliompita kichwani kipa Manula na kukaa wavuni, Mtibwa Sugar ikisawazisha bao dakika nne tu baada ya Simba kupata bao. Shukrani kwa bao la Hassan Dilunga dakika tatu ya nyongeza ya kipindi cha kwanza lililozima kelele za lawama.

**2. SIMBA VS MWADUI (LIGI KUU)**

Charles Ilamfya wa Mwadui FC alimtungua Manula bao la mbali kwenye mechi ya Ligi Kuu msimu wa 2018/19 kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga Septemba 22, 2018, Simba ikishinda mabao 3-1.

Baada ya kutangulia kwa mabao ya John Bocco akifunga mawili, na Meddie Kagere, Ilamfya alifunga bao la kufutia machozi dakika ya 81 alipokimbizwa na beki Pashal Wawa.

Wakati huo huo Manula naye aliamua kutoka goli, lakini bila mahesabu, mfungaji akiwa mita 25 akaubetua juu, mpira ukatinga wavuni.

**3. SIMBA VS AFRICAN LYON (LIGI KUU)**

Awadh Juma wa African Lyon akiwa mita 35 hivi, aliachia shuti kali na mpira kujaa wavuni kwenye mechi ya Ligi Kuu, Oktoba 5, 2018, Ligi Kuu 2018/19 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na kuwafanya mashabiki wa Simba na wasiwasi wa goli kurudishwa kwani sasa ubao ukawa unasomeka mabao 2-1.

Awali Simba ilipata mabao yake kupitia kwa Shiza Kichuya na Emmanuel Okwi na mechi ikaisha mabao 2-1.

**4. SIMBA VS ALLIANCE (LIGI KUU)**

Oktoba 24 mwaka 2018, Simba iliichapa Alliance mabao 5-1 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam yaliyofungwa na Emmanuel Okwi aliyefunga mawili, Asante Kwasi, Adam Salamba na Cleotus Chama, lakini goli la kufutia machozi la Alliance lililofungwa na Zabona Hamisi dakika ya tatu ya nyongeza kabla ya mechi kumalizika, lilikuwa ni shuti la mita 25 lililomshinda Manula na kujaa wavuni.

**5. SIMBA VS COASTAL UNION (LIGI KUU)**

Ilikuwa ni Mei 8, 2019 ikiwa ni Ligi Kuu msimu iliopita 2018/19, Simba ilipoifunga Coastal Union mabao 8-1 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Sar es Salaam.

Manula alifungwa bao mita 30 kwa shuti la mbali lililopigwa na Raizin Hafidh dakika ya 34, lakini halikuwauma mashabiki wa Simba kwa sababu timu yao ikishinda mabao 8-1, ya Okwi matatu, Kegere matatu, Dilunga na Chama.

**6. SIMBA VS JKT TANZANIA (LIGI KUU)**

Agosti 29 mwaka jana, Ligi Kuu msimu huu, Simba ilishinda mabao 3-1 dhidi ya JKT Tanzania yaliyofungwa na Kagere mawili na Miraji Athumani.

Edward Songo alimtungua Manula shuti la mbali mita 30 dakika tatu kabla ya mechi kumalizika na mpira kwenda moja kwa moja wavuni, ingawa halikuwanyima pointi tatu.

**7. SIMBA VS MWADUI (LIGI KUU)**

Kichwa cha mbali kilichopigwa na Gerald Mathis, kilimkuta Manula akiwa ametoka golini na hata alipojaribu kurudi nyuma alikuwa amechelewa na mpira ukajaa ndani ya wavu, Simba ikilala bao 1-0 kwenye Uwanja wa Kambarage, mechi iliyochezwa Oktoba 20 mwaka jana Ligi Kuu msimu huu.

**NAJUA WAJUA**



MSHAMBULIAJI mpya wa Yanga, Ditram Nchimbi, ndiye alifunga bao la ushindi lililoipeleka Timu ya Taifa (Taifa Stars), katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambazo zitachezwa Aprili mwaka huu nchini Cameroon.

SOKA




# NYOTA WA5 WANAOTAKIWA KUSAJILIWA BARCELONA JANUARI

SANCHO

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wameingia mwaka mpya wakiwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Hispania, La Liga, kwa tofauti ya pointi mbili na wapinzani wao wa jadi kwenye soka la Hispania, Real Madrid.

**Inaonekana kama mambo yanakwenda sawa tu kwa vijana hao wa kocha, Ernesto Valverde hasa baada ya kufuzu hatua ya 16 bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Hata hivyo, kuna sehemu ambazo kikosi hicho kinatakiwa kufanyiwa marekebisho.**

Huku wachezaji kadhaa wakiwa wanahusishwa na uwezekano wa kutua pale kwenye dimba la Nou Camp akiwamo Neymar, kwa vyovyote dirisha hili la usajili wa Januari linaweza kuwa bize zaidi kwa kila mmoja, na hapa tunaangalia wachezaji ambao wanaweza kusajiliwa na klabu hiyo ya Katalunya.

**DANI OLMO (WINGA/KIUNGO MSHAMBULIAJI)**

Huku usajili kwa kwenda Barcelona ukionekana kukaribia kwa mshambuliaji huyo wa Dinamo Zagreb, litakuwa jambo la maana kumweka kwenye orodha hii. Barça imeripotiwa imetoa ofa kwa mchezaji huyo wa Hispania na kwamba kwa sasa mambo yanaonekana kwenda sawa.

Anaijua vizuri Barca kwa sababu alikaa pale miaka saba akiwa kwenye akademi yao na wakamruhusu kuondoka. Kiungo huyu ambaye ana uwezo wa kucheza nafasi yoyote ya ushambuliaji, Olmo anaweza kuwa mtu muhimu zaidi kwa kuifungia mabao Barca.

**JADON SANCHO (WINGA)**

Sahau kuhusu Neymar. Hakuna winga ambaye Barcelona wanatakiwa kumchukua kama nyota huyu wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho.

Akiwa na mabao tisa na 'asisti' 10 kwenye mechi 15 za Bundesliga, Mwingereza huyu ameendelea kuonyesha dunia ni namna gani alivyo bora. Bila shaka Barca watakumbana na ushindani mkubwa wa kuwania saini yake, lakini Barcelona ndio sehemu haswa inayomfiti mchezaji huyu kucheza pamoja na Lionel Messi na kwa uhakika watakuwa na safu kali zaidi ya ushambuliaji.

**DONNY VAN DE BEEK (KIUNGO WA KATI)**

Van de Beek kwa muda mrefu amekuwa akihushwa na mpango wa kutakiwa na wapizani wao Real Madrid, lakini Barcelona ndiko sehemu ambako kunaweza kumfaa zaidi.

Wanamhitaji kiungo wa kati na litakuwa jambo jema zaidi kwao kama wataweza kumsajili Van de Beek na kuungana na Frenkie de Jong pale katikati. Rakitic na Vidal washapitwa na wakati, Van de Beek ndio kwanza ana umri wa miaka 22 na anaonekana atakuwa nguzo muhimu zaidi.

De Jong na Van de Beek wakicheza pamoja pale kwenye kiungo ya kati kutaifanya Barcelona kuwa tishio zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**MILAN SKRINIAR (BEKI WA KATI)**

Bahati mbaya, Gerard Piqué anazeeka sasa na Barcelona wanahitaji kupata mbadala wake. Clement Lenglet na Samuel Umtiti wataendelea kupambana kule nyuma, lakini mkali huyu wa Inter, Skriniar atakuwa suluhisho zuri zaidi la kuchukua mikoba ya mkongwe huyo raia wa Hispania.

Beki aliyetulia, mwenye uwezo wa kukaba na kupanda mbele, kwa uhakika kabisa raia huyo wa Slovakia ni aina ya mchezaji ambaye Barcelona wanahitaji kwenye kikosi chao na ni rahisi kumwondoa kutoka pale kwenye dimba la San Siro.

**DONYELL MALEN (FOWADI)**

Bahati mbaya kwa Barcelona, Piqué sio ndio mchezaji pekee kwenye kikosi chao cha kwanza ambaye umri unamtupa mkono. Luis Suarez umri wake sasa ni miaka 32 na amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda kumalizia soka lake kule kwenye Ligi Kuu Marekani, MLS.

Malen ni mmoja wa kizazi kipya chenye vipaji cha Uholanzi. Barcelona kama wakifanikiwa kumsajili nyota huyu kwa uhakika, Malen atakuwa msaada kwa kufunga mabao.

TIMU ya Coastal Union ya jijini Tanga imeendeleza kasi ya ushindi katika mechi za Ligi Kuu Bara baada ya mwishoni mwa wiki kupata ushindi wa tatu mfululizo na kufikisha pointi 26 zilizowapaisha hadi nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo.



NDANI YA 18

Nipashe
Spotika



UMUHIMU wa kuwa na kiungo mkabaji ni hitaji la lazima kwa timu katika soka la kisasa. Kiungo mkabaji anachukuliwa kama ndio 'ngao ya ulinzi' ya timu na mara zote...

Uk. 16&17



RONALDO

# NYOTA 5 WANAOWANIA KIATU CHA DHAHABU KUMPIKU MESSI

**BARCELONA,** Hispania

KWA sasa tumeshaingia katikati ya msimu wa 2019/20. Mchezo wa soka unazidi kupamba moto na klabu za Ulaya zikishindana kuwania mataji mbalimbali.

Pamoja na hilo wachezaji pia wamekuwa kwenye wakati wa kujitengenezea mafanikio yao binafsi.

Tuzo za kiatu cha dhahabu inatolewa kwa mchezaji mwenye mabao mengi zaidi katika ligi kubwa tano Ulaya. Kwa sasa mshindi wa tuzo hiyo ni nahodha wa Barcelona, Lionel Messi, ambaye alikuwa kinara wa mabao kwa ligi zote tano Ulaya msimu uliopita akifunga mabao 36.

Hata hivyo, raia huyo wa Argentina msimu huu ameanza vibaya kwani mwanzo wote aliukosa kutokana na kusumbuliwa na majeruhi.

Pamoja na yote, Messi mwenyewe sio kwamba amepoa, kwani hadi sasa ana mabao 12 kwa jina lake katika mechi alizocheza kwenye Ligi Kuu Hispania, hivyo ushindani unaweza kuwa mkubwa zaidi msimu huu kuliko wakati wowote. Sasa hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao msimu huu wanaweza kumpiku Messi na kutwaa kiatu cha dhahabu kwa ufungaji wa mabao mengi:

**5. CRISTIANO RONALDO**

Nyota huyu wa Juventus haitaji maswali mengi unapomwelezea. Ni mshindi mara tano wa Ballon d'Or pamoja na mchezaji bora wa mwaka wa Fifa.

Msimu huu pia Ronaldo unaonekana anaendeleza makali yake, kwani hadi sasa amefunga mabao 10 katika mechi 14 alizocheza kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, hivyo kwa vyovyote mengi zaidi yatakuja kutoka kwake.

**4. JAMIE VARDY**

Mshambuliaji huyu wa Uingereza naye yupo kwenye mbio za kuwania kiatu cha dhahabu msimu huu.

Vardy hadi sasa amefunga mabao 17 katika mechi 19 alizocheza kwenye Ligi Kuu England, EPL. Na sasa ndiye anayeongoza kwenye orodha ya wachezaji wenye mabao mengi kwenye ligi hiyo.

**3. CIRO IMMOBILE**

Mara ya mwisho mshambuliaji kutoka kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, kutwaa kiatu cha dhahabu Ulaya ilikuwa nmwaka 2016 wakati Gonzalo Higuain alipowazidi Lionel Messi, Luis Suárez na Cristiano Ronaldo wakati alipofikisha mabao 36 akiwa na Napoli.

Kwa sasa Higuain hayupo kwenye kiwango kizuri, lakini amechomoza mwingine kutoka ligi hiyo na si mwingine bali ni nyota wa Lazio, Ciro Immobile.

Kwa sasa anaongoza kwenye orodha ya wafungaji bora kwenye Ligi Kuu Italia akiwa na mabao 17 katika mechi 16 za Serie A hadi sasa msimu huu.

**2. TIMO WERNER**

Mashabiki wengi wa soka wanamwimbia mapambio ya kumsifu, mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski kwa kufunga mabao mengi huko kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Hata hivyo, kuna jina jingine linakuja kwa kasi zaidi na huyo ni nyota wa RB Leipzig, Timo Werner.

Nyota huyu wa kimataifa wa Ujerumani kwa sasa ana mabao 18 kwa jina lake katika ligi hiyo baada ya kushuka dimbani mara 17 kwenye mechi za Bundesliga.

**1. ROBERT LEWANDOWSKI**

Hii ni bunduki ya mabao ya Bayern Munich. Robert Lewandowski kwa sasa ametawala kwenye ligi kubwa tano za Ulaya kwa kupachika mabao msimu huu. Kwa uhakika kabisa ana nafasi kubwa ya kutwaa tuzo hiyo mwishoni mwa msimu.

Raia huyo wa Poland hadi sasa amefunga mabao 17 katika mechi 17 alizocheza kwenye Ligi Kuu Ujerumani.

Anapewa nafasi kubwa zaidi ya kuibeba tuzo hiyo mwishoni mwa msimu kwani, kasi yake ni wazi kwamba inatisha.

**USILOLIJUA**



ALIYEKUWA nahodha wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Vincent Enyeama, alizaliwa katika kijiji cha Akwa Ibom mnamo Agosti 29, mwaka 1982 na aliichezea nchi yake mechi 101 katika kipindi cha kuanzia mwaka 2003 hadi 2015, alipotangaza kustaafu soka la kimataifa.



# Wakulima waomba bwawa kuvunia maji

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKULIMA wa mpunga wa Skimu ya Mnazi wanaounda Ushirika wa Nguvu Kazi Mwanavala katika Wilaya ya Mbarali, wameiomba serikali kuwajengea bwawa la kuvunia maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ili kuepuka uharibifu wa Mto Ruaha.

Wakulima hao ambao wapo zaidi ya 5,000 wanalima mashamba yenye ukubwa wa hekta 5,000 ambazo zinategemewa kwa ajili ya uzalishaji wa malighafi za viwanda 15 vya kusindika mpunga vilivyopo katika Kata ya Ubaruku wilayani humo.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, ambaye alikagua viwanda mbalimbali wilayani humo na kuzungumza na wana ushirika hao kujua changamoto wanazokabiliana nazo kwenye kilimo. Meneja wa Ushirika huo wa Nguvu Kazi Mwanavala, Christopher Uhagile, alisema mashamba hayo mbali na kuwa tegemeo kwenye uzalishaji wa malighafi za viwanda, lakini yanazalisha ajira kwa idadi kubwa ya wananchi.

Alisema endapo watajengewa bwawa hilo na serikali, watakuwa na uwezo wa kuongeza mavuno na kuwa na uhakika wa viwanda vya eneo hilo kufanya kazi mwaka mzima tofauti na sasa ambapo kuna wakati baadhi ya viwanda huwa vinasimama kutokana na kuishiwa malighafi.

"Viwanda hivi vyote vikubwa vilivyopo katika Kata ya Ubaruku, vinaendeshwa kwa malighafi zinazotoka katika mashamba haya ya ushirika kwa zaidi ya asilimia 70, sasa tunaamini serikali ikitujengea bwawa itakuwa rahisi hata viwanda vingine kuongezeka," alisema Uhagile.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema wilaya hiyo ina fursa kubwa ya maendeleo katika sekta ya kilimo, ambayo wananchi wanaitumia ipasavyo kuibua fursa nyingine ikiwamo uanzishwaji wa viwanda. Alisema viwanda vingi katika wilaya hiyo ni vya kusindika mpunga kutokana na kwamba ndio zao kuu linalozalishwa katika wilaya hii, ikilinganishwa na maeneo mengine ya nchi ambayo yanazalisha mazao mchanganyiko.

Alisema wilaya hiyo inazalisha ziada ya mpunga kwa zaidi ya tani 150,000 ambayo wanaitumia kwa ajili ya biashara baada ya kujitosheleza kwa chakula na viwanda vilivyopo.


"Ukipita kwenye maghala utakuta kuna magunia ya kutosha ya mpunga ambayo yamehifadhiwa na mashine zinaendelea kuchakata kwa ajili ya kusafirisha kwenda kwenye masoko mbalimbali ya ndani na nje ya nchi," alisema Mfune.

Akizungumza na wakulima hao pamoja na wamiliki wa viwanda wa Wilaya ya Mbarali, Naibu Waziri Manyanya alisema changamoto hizo ataziwasilisha kwa wenzake ili waone namna ya kuzitatua.

Alisema pamoja na hayo pia watahakikisha wanatekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na Rais John Magufuli aliyoyatoa wakati alipokuwa ziarani wilayani humo.

"Tutawaita wadau mbalimbali ili tujadiliane namna ya kutatua matatizo haya mliyoyasema, na ni muhimu kuboresha kilimo katika kipindi hiki ambacho tunakazana kujenga uchumi wa viwanda," alisema Manyanya.

Baadhi ya wamiliki wa viwanda vya kusindika mpunga, waliomba serikali kuwaboreshea miundombinu ya barabara kwa maelezo kuwa barabara inayoingia kwenye viwanda hivyo sio nzuri.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, akikagua ubora wa mchele unaozalishwa na moja ya viwanda vilivyopo katika Kata ya Ubaruku wilayani Mbarali juzi, alipokuwa kwenye ziara ya kukagua viwanda. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Chakula tani milioni nne kuzalishwa 2020

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya unakusudia kuzalisha tani milioni 3.93 ya mazao ya chakula na biashara katika msimu huu wa kilimo ili kukidhi mahitaji ya wananchi kwa chakula na ziada kuuzwa.

Hayo yalisema na Katibu Tawala Msaidizi (kilimo na uzalishaji), Said Madito, na kuwa ukubwa wa eneo litakalolimwa kwa mwaka mzima ni hekta 559,589 kwa mkoa mzima.

Alisema pamoja na hali ya uzalishaji kukadiriwa kuwa kubwa, lakini mahitaji ya mkoa kwa ajili ya chakula ni asilimia 17 pekee ya chakula, hivyo kuna matarajio ya ongezeko la usafirishaji wa mazao hayo nje ya Mkoa kwa ajili ya biashara.

"Kwa sasa tunawahamasisha wadau wote wa sekta ya kilimo katika Mkoa huu, kuendelea kuwahamasisha wananchi na kuwasaidia kuzalisha kwa tija ili ikiwezekana tuvuke lengo tulilojiwekea," alisema Madito.

Alisema kwa sasa hali ya usalama wa chakula katika mkoa huo ni ya kuridhisha kwa kutumia kigezo cha ufikaji katika mashamba na kwenye masoko.

Alisema tathmini iliyofanyika kufikia mwezi Oktoba 2019 inaonyesha kuwa bei ya mazao katika masoko mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya hasa mazao ya kipaumbele ilikuwa chini kiasi kwamba ilikuwa ni rahisi kila mwananchi kumudu kununua.

Alisema bei ya mahindi ambayo ndiyo zao kuu la chakula ilikuwa ni wastani wa Sh. 600 kwa kilo mpaka Sh. 800, mchele ilikuwa Sh. 1,500 mpaka 2,200 kwa kilo moja, maharage ilikuwa Sh. 1,500 mpaka Sh. 2,200 kwa kilo moja.

Aliyataja mazao mengine ya kipaumbele ni ndizi ambazo zilikuwa zinauzwa Sh. 500 mpaka Sh. 1,000 kwa kilo na viazi ilikuwa Sh. 300 mpaka Sh. 700.

# Chalamila awajia juu wanaharakati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewajia juu baadhi ya watetezi wa haki za binadamu nchini waliomkosoa alipowacharaza bakora wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kiwanja wilayani Chunya kwa kosa la kuchoma mabweni, lakini wako kimya wakati watoto wanaibwa.

Akizungumza juzi katika uwanja wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) wakati wa kuwapokea watoto wawili wa familia moja waliokuwa wamepotea jijini Mbeya na kukutwa mkoani Tabora, Chalamila alisema wakosoaji wake hao hawana maana.

Alisema walikuwa mstari wa mbele kuwatetea wanafunzi waliochoma mabweni, lakini hawajaonekana mahali popote kutetea watoto waliokuwa wameibwa na kwamba anahisi pengine kwao watoto hao hawana haki ya kuishi.

"Ninyi ni mashahidi, lile tukio la mimi kuwachapa wanafunzi waliochoma mabweni kule Chunya, lilivaliwa njuga na wanaojiita watetezi wa haki za binadamu mpaka likasikika hata kimataifa, lakini kwenye hili la watoto wetu kupotea wako kimya, sasa sijui haki za binadamu kwao zina maana gani," alisema Chalamila. Hata hivyo, aliyashukuru makundi mbalimbali ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa ushirikiano walioonyesha kwenye tukio la kupotea kwa watoto hao likiwamo Jeshi la Polisi, vyombo vya habari, machifu pamoja na viongozi wa dini. Aidha, aliagiza watoto hao wakapimwe afya zao katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya na wataalamu wa masuala ya saikolojia wawasaidie wazazi kupatiwa ushauri ili suala hilo lisiendelee kuwatesa.

Katika hatua nyingine, Chalamila alisema pamoja na kwamba baadhi ya taarifa zinaonyesha kuwa mwizi wa watoto hao ambaye ni Hawa Mkalipa (40) na matatizo ya akili, lakini yeye ana maono tofauti.

"Kichaa anaokota makopo lakini huyu aliacha makopo akaokota watoto, sasa ukimwangalia kwa haraka haraka unaona kila dalili za ushirikina, kwa sasa tuliache Jeshi la Polisi liendelee kumuhoji ili aseme alikuwa ametumwa na nani na alikuwa anawapeleka wapi watoto," alisema Chalamila.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema mwizi huyo wa watoto baada ya kuwachukua nyumbani kwao Ituha jijini Mbeya, alipita mkoani Songwe, akaingia Rukwa, Katavi na hatimaye akatokea Tabora.

Alisema mama huyo ambaye ni mkazi wa Kariakoo jijini Dar es Salaam, alikuwa anaelekea na watoto hao mkoani Mwanza, lakini alipofika Tabora mtoto mmoja akaugua na ndipo akamwacha wa kiume na kumkimbiza hospitalini mdogo.

Alisema baada ya kufika hospitalini ndipo watu walipomshtukia kuwa mtoto siyo wa kwake na hatua za kumkamata zikaanza kuchukuliwa na taarifa zikaletwa ofsini kwake akatuma baadhi ya maofisa kwenda kufuatilia.

"Hili tukio limetunyima sana usingizi, wananchi wa Mbeya wameonyesha ushirikiano mkubwa sana kwenye hili tukio, walishiriki kutafuta na kusambaza taarifa, sasa huyu mama kinachofuata ni mahakamani na tutahakikisha anafungwa maana tukio la kuiba watoto ni baya," alisema Matei.

Baba wa watoto hao, Mashaka Juma, aliwashukuru wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa ushirikiano waliomwonyesha wakati wa kuwasaka watoto hao na kwamba tukio hilo limemuumiza sana.

Alisema ni mara ya kwanza kukutana na tatizo kama hilo kwenye maisha yake na hivyo akawashauri wananchi kuwalinda watoto wao ili kuepuka shida kama aliyoipata.





# Mchungaji awachongea wakwepa kodi ya serikali

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MCHUNGAJI Kiongozi wa Kanisa la Evangest Assembles of God Tanzania (EAGT) Ipagala mkoani Dodoma, Evance Lucas, amesema Watanzania wanaokwepa kulipa kodi ni wapinga maendeleo yanayofanywa na uongozi wa serikali ya awamu ya tano na pia wanakwamisha ukuaji wa uchumi. Lucas aliyasema hayo alipokuwa akihubiri kwenye ibada maalumu ya kukaribisha Mwaka Mpya wa 2020, iliyofanyika katika Kanisa la EAGT Ipagala jijini hapa, na kusema wanaokwamisha ulipaji huo wa kodi ni sawa na wapinzani wa maendeleo. Katika mahubiri yake alisema maendeleo mbalimbali yanayojitokeza kwa hivi sasa yanatokana na kodi hizo zinazotolewa na Watanzania, hivyo ni wajibu kuhakikisha kila Mtanzania analipa kodi mwenyewe, bila kufuatiliwa.

Alisema kuwa kodi hiyo isipotolewa hakuna miundombinu itakayoonekana kama ilivyo sasa katika awamu ya tano ya uongozi wa Rais John Magufuli, ambapo maendeleo mbalimbali yamepatikana ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara, afya, usafiri wa ndege na elimu.

"Mnajua uendeshaji wa serikali yoyote ile unakuwa mgumu kutokana na wananchi wake kutolipa kodi, lakini pale inapolipwa kodi hizo bila kushurutishwa uchumi wake unakua kwa haraka na maendeleo yake yanakua kwa kasi kubwa, hivyo ni muhumi kodi zikalipwa kwa wakati na tena siyo kwa kudaiwa kwa nguvu," alisisitiza.

Pia aliwataka Watanzania kuhakikisha wanawajibika katika kuombea uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka huu ili ufanyike kwa amani na utulivu.

Kadhalika, aliwaomba viongozi wa madhehebu mbalimbali ya dini kutumia nyumba zao za ibada kuhakikisha waumini wanakuwa na utamaduni wa kufanya sala na dua ili uchaguzi huo uwe huru na haki.



Wazazi wa wanafunzi wakiwanunulia watoto wao sare za shule kama walivyokutwa eneo la kibiashara la One Way jijini Dodoma mwisho wa wiki, ikiwa ni maandalizi ya shule ambazo zimefunguliwa leo Jumatatu. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Wenyeviti wa mitaa 222 walia kunyimwa mihuri

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HATIMA ya wenyeviti wa serikali za mitaa 222 wa Jiji la Dodoma kucheleweshewa mihuri inatarajiwa kujulikana kesho.

Kesho watajadiliana ni kwanini wamekuwa wakizungushwa kwa zaidi ya miezi miwili sasa kupatiwa mihuri na maofisa watendaji wao.

Akizungumza na waandishi wa habari, mwenyekiti wa wenyeviti wa mitaa hiyo 222, Jiji la Dodoma, Matwiga Kyatya, alisema:

"Katika kikao chetu, hatutashiriki kwa maandamano tutafanya kikao kwa njia ya amani, lengo letu ni kutafuta muafaka wa kupewa mihuri kwa ajili ya kuhudumia wananchi... baada ya kuapishwa na hakimu hatukuambiwa lolote tuliambiwa tuwahudumie wananchi na kutumia mihuri na kufuata kanuni taratibu na kanuni za nchi." Aidha, alisema wananchi wamekuwa wakikutana na changamoto ya kutembea umbali mrefu kuwatafuta watendaji wa kata ili wapate huduma hiyo ya kugongewa mihuri.

"Sasa hivi wanahudumiwa na baadhi ya mihuri ya watendaji wa kata, lakini kunakuwa na usumbufu mkubwa wananchi wengi wanaishi mbali kwa sababu mitaa mingine haina watendaji.

Mwenyekiti huyo alitoa wito kwa serikali kuhakikisha wenyeviti wanapewe mihuri kwa ajili ya kuhudumia wananchi kwani mikoa mingine wameshapewa. "Tatizo hili ni kwa Jiji la Dodoma tu, kwa sababu sehemu nyingi wenyeviti tayari wana mihuri yao isipokuwa kwa Jiji la Dodoma tu," alisema.

Pia alisema katika kikao hicho watajadiliana mambo mabalimbali ikiwamo, utendaji kazi, namna gani ya kuleta maendeleo katika mitaa pamoja na kuhakikisha ulinzi na usalama unakuwapo katika mitaa.

Juzi baadhi ya wakazi wa Jiji la Dodoma, wakizungumza na waandishi wa habari, walidai kwamba walitegemea baada ya kuapishwa wenyeviti hao mihuri wangeipata kwa urahisi, lakini wanalazimika kutembea umbali mrefu kwenda kwa watendaji wa kata ili kuipata mihuri hiyo.

Juma Matonya, ni mkazi wa Mtaa wa Kisabuje jijini hapa, alisema ametembea umbali mrefu kwenda mpaka eneo la Kizota kumtafuta mtendaji wa kata hiyo ili apate kupigiwa mihuri barua yake ya maombi ya kazi.

"Tunakutana na wakati mgumu kutokana na wenyeviti wa mitaa kutokuwa na mihuri, imenibidi nipande bodaboda mpaka Kizota kwa ajili ya kumfuata Mtendaji wa Kata, jambo hili tunaomba liangaliwe.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, alisema suala hilo lipo kwa Ofisa Utumishi, lakini aliahidi kulifuatilia ili kujua sababu ni nini.

# Uhaba wafanyausafi walikumba soko kuu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU wa Soko Kuu la Majengo jijini hapa, Eliamini Mollel, ameliomba jiji kuongeza wafanyausafi katika soko hilo kwa kuwa waliopo hawatoshi.

Soko lina wafanyausaji sita tu ambao hawatoshi kuhudumia soko hilo lenye mamia ya wafanyabiashara.

Mollel alisema soko hilo lenye wafanyabiashara zaidi ya 2,000 lina wafanyausafi wasiopungua sita walioletwa na Ofisi ya Jiji la Dodoma.

"Wafanyausafi ni wachache hawazidi sita kwa soko zima, soko ni kubwa tungekuwa na angalau 12 au 15 soko ni kubwa," alisema.

Pia alisema walifanikiwa kuzibua mitaro kabla ya mvua kuanza kunyesha kwa kutumia michango ya viongozi wa soko hilo.

Mollele alisema kuna uhaba wa vitendea kazi na vifaa vya kutupia uchafu vinavyoletwa na Jiji la Dodoma hali ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikichangia mrundikano wa uchafu katika eneo hilo.

Alisema awamu ya kwanza za michango zilipatikana Sh. 150,000 na awamu ya pili zilipatikana Sh. 110,000 fedha ambazo zilitimika kuwalipa watu waliozibua mitaro ya ndani na nje nya soko hilo. Aidha, alisema changamoto nyingine katika soko hilo ni ongezeko la bei ya huduma ya choo kutoka Sh.100 hadi Sh. 200.

"Saula hilo bado ni kitendawili tumejaribu kulalamikia ongezeko hilo hatujasikilizwa tumepuuzwa na ofisi ya Mkurugenzi, tumejaribu kuonana ana kwa ana, lakini hatujafanikiwa," alisema.

Alisema wafanyabiashara wanalipa bei mpya ya Sh. 200 kwa shingo upande.

"Ongezeko la bei ya huduma ya choo limeleta uchafuzi wa mazingira kwani baadhi ya watu wanakojoa kwenye chupa za maji kisha kuzitupa, tulifanya msako wa kusaka wanaofanya hivyo lakini sasa tatizo hilo limepungua," alisema.

Alisema soko hilo lina vyoo vitatu vinavyoendeshwa na kampuni tofauti na vyote bei ya huduma imepanda.

"Uongozi wa soko haukushirikishwa kwenye ongezeko hilo la bei ilikuwa ni amri hakuna ushirikishwaji tulisomewa kama tangazo," alisema.

Akizungumzia juu ya kuezekwa kwa eneo la 'stock yard' alisema wanasubiri mkandarasi akamilishe michoro na kununua vyuma ili eneo hilo liezekwe kwani bati zipo.

Alisema wahandisi wa tatu kutoka Jiji la Dodoma walifika kwa ajili ya ukaguzi wa kazi hiyo na kinachosubiriwa ni vyuma.

Alisema eneo hilo lina makundi matatu ya wafanyabiashara wa jumla wa nyanya, vitunguu na mahindi.

Aidha, akizungumzia hali ya biashara kwa kipindi cha sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya zilizopita alisema hali ya biashara ilikuwa ya wastani.

Alisema gunia la viazi mviringo lenye kilo 45, liliuzwa kwa Sh. 70,000 kutoka Sh. 45,000 ya hapo awali viazi hivyo ni kutoka mikoa ya Mbeya na Njombe na kilo moja ilikuwa ikiuzwa kwa Sh. 1,200 hadi Sh. 1,500.

Alisema ongezeko hilo la bei ni kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika mikoa mbalimbali hali inayosababisha usafirishaji kuwa mgumu.

"Viazi vingi tulikuwa tunategemea kutoka Njombe sasa ni vigumu kuvipata sababu kubwa ni mvua, biashara ni ya kawaida licha ya kuwa na sikukuu tofauti ni ndogo sana labda sababu ya uchumi wa wananchi unaweza kuwa ni mgumu," alisema.

Alisema bidhaa kama mchele bei zimekuwa za kawaida kwa Sh. 1,700 hadi Sh. 2,200 kwa kilo moja na bei ya kuku imeendelea kuwa ile ile kwa kuku wa kienyeji wanaanzia Sh.10,000.



## HABARI ZANZIBAR

# Z'bar yaingia mchakato uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuwa Zanzibar imeingia katika mchakato wa kutekeleza uchumi wa bluu na tayari hatua kubwa zinachukuliwa kuhakikisha lengo hilo linafikiwa.

Alisema kuwa watu wa Zanzibar wamezungukwa na bahari, lakini hiyo haijatumiwa vizuri na badala yake watu kutoka nje ya nchi huwaiba samaki wa Zanzibar wakiwamo aina ya jodari.

Akizungumza juzi wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa soko la samaki na bandari ya uvuvi huko Malindi Mjini Unguja, alisema samaki wakubwa na wazuri wako bahari kuu ambako kufikia huko kunahitajika uwezo wa vifaa vya kuvulia. Alisema haiwezekani Zanzibar izungukwe na bahari, lakini haivui samaki ipasavyo na kutokuwa na kiwanda cha kusindika.

Dk. Shein alisema serikali inajenga bandari pamoja na soko la Malindi ambalo idadi ya wastani ya watu 6,000 watafanya kazi katika eneo hilo la soko jambo ambalo litaleta tija katika sekta ya uvuvi.

Alisema historia ya Zanzibar inaonyesha watu wa Zanzibar walianza kuvua kwanza kuliko kulima, hivyo uvuvi una historia kubwa na ambayo ni uvuvi.

"Uvuvi wa samaki ni sehemu moja tu katika uchumi wa bluu, lakini katika uchumi huo ni vyema kukawapo maandalizi ya usafiri wa uhakika wa baharini, boti za kisasa na kuwawezesha wavuvi wa hapa nchini," alisema.

Alisema serikali itakapojenga bandari mpya ajira na biashara vyote vitaongezeka kwa kiasi kikubwa hasa ikizingatiwa kuwa Zanzibar ina historia ya biashara.

Naye Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, alisema wizara hiyo imeweka utaratibu maalumu wa kufuatilia miradi yao ili kuhakikisha inamaliza kwa wakati na inakuwa bora.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wavuvi ili waweze kuvua uvuvi wenye faida na kipato ili waondokane na uvuvi wa mazoea.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mariam Juma Abdalla Saadalla, alieleza kwamba uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa soko hilo na bandari ya wavuvi ni matokeo ya jitihada za muda mrefu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alieleza kuwa jengo hilo la soko la kisasa na bandari ya uvuvi, linajengwa na Kampuni ya Rinkai Nissan Construction Co. Ltd kutoka nchini Japan ikisaidiana na SCI Co. Ltd ya Dar es Salaam na Coastal Dredging Co. Ltd ya Zanzibar.

Alisema kuwa ujenzi huo utagharimu Sh. bilioni 26.491 kati ya hizo Sh. bilioni 22.776 ni msaada kutoka Serikali ya Japan kupitia (JICA) na Sh. bilioni 3.715 ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mkataba wa ujenzi ulifungwa rasmi Machi 26, 2019 na ujenzi kuanza mwezi Juni, 2019.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mohamed Aboud Mohamed, akizungumza na wananchi wa Uroia baada ya kuzindua mradi wa majisafi na salama wa kijiji hicho, akimwakilisha Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wananchi wahakikishiwa majisafi, salama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imewahakikishia wananchi wote kwamba itaimarisha utoaji wa huduma za majisafi na salama hadi lengo la kuwafikia wananchi linatekelezwa ipasavyo.

Utekelezaji huo ni mwendelezo wa dhamira za waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 wenye azma ya kwenda sambamba na malengo yaliyowekwa na jumuiya za kimataifa katika kukidhi mahitaji ya maji kwa binadamu ambayo ni chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Akizungumza jana kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Waziri Mohamed Aboud Mohamed, kwenye uzinduzi wa mradi wa majisafi na salama wa Bambi - Uroa, alisema upatikanaji wa huduma hiyo huleta faida kubwa katika jamii hasa kwa wanawake na watoto. Alisema baadhi ya vijiji vilivyopakana na bahari kikiwamo kijiji cha Uroa, wananchi wake wanatumia maji ya chumvi ambayo sio mazuri kiafya na kufikia uamuzi wa kuwaondolea shida hiyo kwa uchimbaji wa kisima hicho.

Aliwaomba wananchi wa Uroa na vijiji vitakavyotumia huduma hiyo kuchangia ili kuiwezesha Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kumudu, kuyalinda, kuyasambaza na kuyafanya maji kuwa huduma inayoendelea.

Akitoa taarifa ya kitaalamu ya mradi huo wa Bambi - Uroa, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, Ali Khalil Mirza, alisema Uroa ni vijiji vilivyoanza kupata huduma ya majisafi na salama baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Mirza alisema Serikali ya Zanzibar ililazimika kufanya juhudi ya kuchimba kisima kwa ushirikiano na Serikali ya Rais Al - Khaimah, baada ya maji waliyokuwa wakitumia kuchanganyika na maji ya chumvi. Alisema mradi huo wa majisafi na salama kutoka Bambi hadi Uroa, wenye urefu wa kilomita nne, umegharimu zaidi ya Sh. 349,000,000, utakuwa na uwezo wa kuzalisha lita 960,000 wakati mahitaji halisi ni lita 800,000 kukiwa na akiba ya lita 160,000.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini kwa niaba ya wananchi wa mkoa huo, Ayoub Mohamed Mahmoud, alisema wananchi wa Mkoa wa Kusini wamefarijika kutokana na kukamilika kwa mradi huo kutoka Bambi kwenda Uroa na kuondoa changamoto iliyodumu kwa kipindi kirefu.

Ayoub alisema mradi huo utasaidia kufaidisha wananchi wa Shehia ya Uroa iliyozungukwa na vijiji vinne wakati Shehia saba ndani ya Wilaya ya Kati bado zinaendelea kukumbwa na tatizo la ukosefu wa majisafi na salama.

## Mapinduzi yasifiwa kuondoa ubaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAPINDUZI ya Zanzibar yameelezwa kuwa yameleta usawa, umoja, udugu na maelewano na kuondoa ubaguzi wa aina zote na kuwafanya Wazanzibari wawe wamoja.

Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alisema Zanzibar inayoonekana sasa na ile ya miaka 60 iliyopita ni tofauti. Dk. Shein aliyasema hayo jana katika hafla ya uwekaji wa mawe ya msingi ya Michenzani Mall na jengo la Sheikh Thabit Kombo, hafla iliyofanyika katika viwanja vya Mapinduzi Square, ikiwa ni shamrashamra za sherehe za miaka 56 ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964.

Akieleza historia ya Zanzibar, Rais Dk. Shein alisema wazee walipata madhila na hawakuwa na maisha mazuri kama ilivyo hivi sasa na kuwataka Wazanzibari kutosahau historia yao ikiwa ni pamoja na kujua walikotoka, walipo na wanakokwenda.

Alieleza historia ya mji wa Zanzibar na mipaka yake kabla ya Mapinduzi matukufu ya Januari 12, 1964 na jinsi Waafrika walivyokuwa wakiishi katika nyumba zisizostahiki kuishi binadamu. Alisema lazima historia ielezwe kwa watoto, wajukuu, virembwe na vinyinginya hasa ikizingatiwa kuwa kabla ya Mapinduzi Mwafrika alikuwa hana haki ya kufanya jambo lolote la maendeleo hata kustarehe nchini mwake. Alisema hatua hiyo ndiyo iliyofanya mapambano ya miaka saba katika kupigania uhuru wa Mwafrika, Zanzibar na hatimaye kufanywa kwa Mapinduzi matukufu ya Januari 12, 2964.

Alisema ni jambo la kusikitisha kwa wanaokebehi Mapinduzi kwa kuwa Mapinduzi yamefanyika nchi nyingi duniani ikiwamo Ufaransa, Marekani, Cuba, Misri, China na nyinginezo kwa lengo la kuondoa dhuluma.

Alisema Michenzani ni kitovu na historia ya Mapinduzi na mambo yote wakati huo yalikuwa yakipatikana Michenzani hivyo, ni vyema historia hiyo ikaimarishwa. Alisema, jengo la Thabit Kombo, linatokana na historia ya mwasisi huyo ambaye ameitumikia nchi na ana historia kubwa ya Zanzibar, biashara na historia ya ASP na baadaye CCM.

Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohammed Ramia Abdiwawa, alisema eneo hilo lina historia yake katika vuguvugu la Mapinduzi ya Januari 12, 1964. Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Khamis Mussa, katika risala yake alisema ujenzi wa maduka hayo katika eneo la Michenzani ni miongoni mwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015/2020 ambayo kwa Zanzibar, Rais Dk. Shein amekuwa akiitekeleza kwa vitendo.

Kwa upande wa jengo la Sheikh Thabit Kombo, alisema kuwa huo ni ubia kati ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika eneo la maskani ya MwembeKisonge kwa ajili ya mradi wa jengo la biashara lenye maduka, ofisi na kumbi za mikutano.

# Malalamiko ya wafungwa yamwibua RC

**Hamisi Nasiri,** MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, ameunda timu maalum ya kuchunguza malalamiko yaliyotolewa na wafungwa na mahabusi waliopo katika Gereza la Kilungu mkoani Mtwara.

Byakanwa alichukua hatua hiyo baada ya kufanya ziara katika gereza hilo, ambayo ililenga kusikiliza kero za wafungwa na mahabusi wa gereza hilo.

Alisema amekasirishwa sana na malalamiko ambayo ameyapokea kutoka kwa baadhi ya mahabusi hao na wafungwa waliopo kwenye gereza hilo.

Byakanwa alisema moja ya malalamiko hayo ambayo yamemsukuma hadi kufanya maamuzi ya kuunda timu ya kuchunguza ni mahabusi kupewa kesi ambazo haziendani na makaosa yao.

Alisema malalamiko mengine ambayo yametolewa na baadhi ya wafungwa ni ya uwapo wa wafungwa zaidi ya 75 kutoka Ethiopia ambao wao wenyewe wameeleza kuwa kifungo chao kimemalizika, lakini wameendelea kukaa gerezani.

Byakanwa alisema malalamiko hayo kwake ni tosha kabisa kumfanya aunde timu maalum kwa ajili ya kuchunguza kile kinachoelezwa na wafungwa hao ili kupata majibu halisi ya pande zote mbili.

"Naunda tume hii na nataka ifanye kazi ndani ya siku saba halafu inipe majibu ya kile kinacholalamikiwa na wafungwa hawa inakuwaje wafungwa wawe wamemaliza kifungo chao halafu wasema bado wapo gerezani?" Alihoji Byakanwa.

Mkuu huyo wa Mkoa aliendelea kufafanua kuwa kwa jambo hilo lazima sheria ifanye kazi yake waliokosa washtakiwe kuendana na makosa yao waliofanya na sio kubambikiziwa makosa ambayo hawajayafanya.

Alisema timu hiyo itafanya kazi kwa haki na itatoka na taarifa yote halisi juu ya malalamiko hayo na yeye atayafanyia kazi.

Akizungumza kwa niaba ya mahabusi wa gereza hilo, Leonard Igogo, alisema yeye anakabiliwa na kesi ya madai ya Sh. milioni tatu, lakini kesi hiyo imeguuzwa na kuwa kesi ya uhujumu uchumi ya kudaiwa Sh. bilioni tatu.

Alisema ameshangazwa kuona kesi yake kwa sasa kugeuzwa kuwa ya uhujumu, na kwamba tangu kesi yake hiyo ifunguliwe alishakuwa tayari kulipa deni hilo Sh. milioni tatu, lakini alikataliwa na baadaye kesi kugeuzwa na kuwa ya uhujumu uchumi.

"Mahabusu katika gereza wamekuwa wakibadilishiwa kesi zao halisi na kupewa kesi ambazo haziendani na makosa, hivyo tunakushukuru sana mkuu wa mkoa kwa kuja kutusikiliza malalamiko yetu hapa," alisema Igogo.

Naye mfungwa ambaye ni miongoni mwa wafungwa raia wa Ethiopia, Tagabu Tambabre, alisema wao wamemaliza kifungo chao miaka miwili iliyopita, lakini bado wapo gerezani hadi sasa.

Alisema wanaiomba serikali ya Tanzania kuwaachia uhuru, na kuwafanyia utaratibu wa kurudi nchini kwao, ili wakaendelee na maisha yao na familia zao kwani kifungo chao kimemalizika, hivyo na hakuna sababu ya wao kuendelea kuwa wafungwa.




Lori la mizigo likiwa limekata barabara katika mteremko wa Simikoe jijini Mbeya kwenye barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam) baada ya kushindwa kupanda mlima na kuanza kurudi nyuma. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Waomba viwanda vya kisasa kukamua mawese

**Na Ashton Balaigwa,** KIGOMA

WAKULIMA wa michikichi katika mkoa wa Kigoma walioitikia wito wa serikali wa kulima zao hilo, wameiomba kuwajengea viwanda vyenye teknolojia ya kisasa pamoja soko maalumu la kuuza mafuta ya mawese kwa bei elekezi.

Wametoa ombi hilo kutokana na kuwapo kwa mkakati wa kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Wameeleza kuwa kutokuwapo kwa soko maalum kwa ajili ya kuuza mafuta ya mawese inewasababisha kuuza kwa bei ya chini, hivyo kushindwa kujikwamua kimaisha.

Mmoja wa wakulima hao mkazi wa Kata ya Mahembe, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Dina Cosmas, alisema pamoja na kuitikia wito wa serikali kulima michikichi kwa kutumia mbegu za kisasa aina ya Tenera, lakini bado kuna changamoto ya viwanda vya kukamulia michikichi ili kutengeneza mafuta.

Alisema viwanda vilivyopo vya kukamulia mafuta ya michikichi ni vya teknolojia ya zamani ambavyo vinachangia upotevu wa mafuta, hivyo kusababisha baadhi ya wakulima wanaozalisha zao hilo kupata hasara kutokana na gharama wanazotumia katika kilimo hicho.

Naye John Ndumiwe kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, alipongeza mkakati wa serikali wa kufufua zao la michikichi kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta, na kutaka uende sambamba na ujenzi wa soko la kisasa kwa ajili ya kuuza na kununua mafuta ya mawese kwa bei itakayopangwa ili wakulima waondokane na ulanguzi unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara kutoka maeneo mbalimbali.

" Tumeitikia wito wa serikali wa kulima zao la michikichi kwa ajili ya kuzalisha mafuta ya kula yatayosambazwa nchini, lakini changamoto kubwa hakuna soko la uhakika la kuuza mafuta... kila mkulima anajikamulia mafuta na kuuza kwa bei anayokubaliana na mteja, lakini wengi wao tunauza kwa hasara dumu la lita 20 linauzwa mpaka mpaka Sh. 26,000," alisema Ndumiwe.

Mwenyekiti wa Muungano wa Vyama vya Wakulima wa Michikichi katika mkoa wa Kigoma (AMCCOS), Hussein Ally, alisema kwa kuungana wanakusudia kuzifuata taasisi za fedha kwa ajili kuomba mkopo kujenga soko la kisasa la kuuzia mafuta ya mawese ili kuondokana na ulanguzi.

Akizungumzia tatizo la viwanda vya kukamulia mafuta hayo, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari), Dk. Geofrey Mkamilo, alisema mkakati wa kwanza uliwekwa ni kuzalisha mbegu za kisasa aina ya tenera ambazo zinatoa mafuta mengi ya mawese kwa ajili ya kuwapa bure wakulima ili waachane na mbegu za zamani aina ya dura ambao umepata mafanikio makubwa.

Alisema baada ya hapo serikali kupitia taasisi zake wameanza kuweka nguvu katika ujenzi wa viwanda vya kisasa kwa ajili ya kuchakata mafuta ya mawese kwa kuwa vilivyopo sasa ni vya teknolojia ya zamani ambayo inachangia kupotea kwa asilimia 40 ya mafuta ya mawese yanayokamuliwa.

Naye ofisa kilimo katika Sekretarieti ya mkoa wa Kigoma, Joseph Rubuye, akizungumzia changamoto za viwanda vya kisasa vya kukamulia mafuta na soko la mawese, alisema zimeshapatiwa ufumbuzi wa uhakika kutokana na kujitokeza kwa baadhi ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kujenga viwanda vya kisasa ili kununua michikichi kisha kukamua mafuta ya mawese.

# Changamoto chanjo ya homa ya ini

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MTAALAMU wa maabara wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Simiyu, Raphael Kambona, amesema wanakutana na changamoto ya upatikanaji wa chanjo za kutosha ya homa ya ini hali inayowalazimu kusitisha huduma hiyo kwa vipindi.

Kambona alisema hayo jana na kubaini kuwa ndani ya miezi sita tangu hospitali hiyo ianze kutoa huduma hiyo, mwitikio wa wananchi wa kupima na kupatiwa chanjo umekuwa mkubwa sana.

Alisema kwa sasa mwitikio wa wananchi ni mkubwa hali inawalazimu kusitisha kupokea wateja wapya wa chanjo kwani kutokana na akiba waliyonayo kuwa kidogo.

"Mwitikio wa wananchi kupima na kutambua afya zao umekuwa mkubwa... watu wanajitokeza kwa wingi kupima na kupatiwa chanjo ya homa ya ini baada tu ya kutangaziwa huduma hiyo kutolewa hospitalini hapo," alisema na kuongeza:

"Ila tunakutana na changamoto ya uhaba wa chanjo, maana akiba iliyopo inahifadhiwa kwa ajili ya kukamilisha chanjo za wale walioanza."

"Tumekuwa tukiwarudisha wateja wetu wengine kwa sababu ya uhaba wa hizi chanjo...na tunafanya hivyo ili wale walikwishaanza waweze kupata kwa mtiririko unaotakiwa na tukishawaanzishia ni lazima tuwakamilishie dozi ya awamu tatu," alifafanua Kambona.

Kambona alieleza kuwa kwa kipindi cha miezi sita jumla ya wananchi 251 sawa na asilimia 3.2 walijitokeza kupata huduma ya upimaji na chanjo ya homa ya ini na kati ya hao nane waligundulika na homa hiyo na kupewa rufani za kwenda Hospitali ya Bugando kwa ajili ya matibabu zaidi.

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Simiyu, Dk. Matoke Mahanji, alisema kadri hospitali inavyoendelea kufanya kazi ndivyo itakavyoweza kujitosheleza kwa kila kitu.

Alisema bado hospitali hiyo ni changa ila ni matumaini yao watazidi kupanuka na kuboresha huduma muhimu ambazo hazijakamilika.

HABARI KIMATAIFA

## Museveni aanza matembezi ya siku sita jangwani

**KAMPALA,** Uganda

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, ameanza matembezi ya siku sita jangwani, kama sehemu ya kumbukumbu ya jinsi vikosi vyake vilivyopambana kuchukua madaraka mwaka 1986, kutoka kwa Idi Amin na Milton Obote.

Wapinzani wake wamekosoa matembezi hayo, wakidai kuwa na mpango wa kujipatia umaarufu kabla ya uchaguzi mkuu mwaka ujao, Museveni anatarajiwa kugombea urais kwa muhula wa sita.

Rais Museveni anakabiliwa na upinzani kutoka kwa msanii wa zamani wa muziki na mwanasiasa, Bobi Wine, ambaye anajinadi kama mkombozi wa maskini.

Katika matembezi hayo atakamilisha katika mji wa magharibi wa Birembo, eneo ambalo mapigano makali yalizuka kati ya vikosi vya waasi vikiongozwa na yeye (Museveni) na wanajeshi wa aliyekuwa Rais wa Uganda wakati huo Milton Obote, Junuari 10, mwaka 1986.

Katibu Mkuu wa Mawasiliano ya Rais, Don Wanyama, ameliambia shirika la habari la AFP kuwa safari hiyo inayoongozwa na Rais, ni hatua ya kukumbuka yaliyopita ili kujivunia hali ilivyo sasa.

"Safari hii itadumu kwa wiki moja jangwani, kupitia njia iliyopitiwa na wakombozi wa nchi wakiongozwa na Museveni." Alisema.

Bobe Wine ambaye jina lake halisi ni Robert Kyagulanyi, ameliambia shirika hilo kwamba matembezi hayo ya Rais ni ya kupoteza muda. **BBC**

## Trump atishia kuvishambulia vituo 52 vya Iran

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameonya kuwa nchi yake itayashambulia haraka na vikali maeneo 52 ya Iran iwapo nchi hiyo italipiza kisasi mauaji ya Jenerali Qassem Soleimani.

Katika ujumbe wa kitisho kupitia ukurasa wa Twitter, Trump amesema maeneo yatakayolengwa ni yale yaliyo muhimu kwa Iran na utamaduni wake, na akaonya Marekani haiko tayari kuendelea kutishwa.

Ujumbe huo wa Trump unafutia onyo la makundi ya wanamgambo yanayoiunga mkono Iran, la kuvishambulia vituo vya Marekani nchini Iraq kutokana na mauaji ya kamanda huyo.

Katika ishara za mwanzo za uwezekano wa kulipa kisasi, makombora mawili yalilipiga eneo lililo karibu na ubalozi wa Marekani mjini Baghdad mapema jana.

Makombora mengine mawili yalishambulia kambi ya kijeshi ambayo inahifadhi wanajeshi wa Marekani, lakini hakuna athari kubwa zilizoripotiwa. **DW**

# Wanamgambo Al Shabab wauawa uwanja wa ndege

**NAIROBI,** Kenya

**Wakazi wa eneo hilo wamesema walikuwa wanasikia milipuko na baadaye milio ya risasi.**

KUNDI la kigaidi la Al Shabaab, limefanya shambulio katika uwanja wa ndege wa jeshi unaotumiwa na vikosi vya Marekani na Kenya katika eneo la Lamu, Kusini Mashariki mwa Kenya.

Kundi hilo la kigaidi la mtandao wa Al-Qaeda limesema kuwa tukio hilo halina uhusiano wowote na malumbano yanayoendelea kati ya Iran na Marekani.

Jeshi la Kenya limethibitisha kutokea kwa shambulio hilo katika Uwanja wa Ndege wa Lamu.

Msemaji wa jeshi la Kenya, amesema kuwa wameweza kuthibiti shambulio hilo na wamekuta miili minne ya wanamgambo wa Al Shabaab.

Hakuna maelezo zaidi yaliyotolewa. Mji wa Lamu, kusini mashariki mwa Kenya

Al Shabaab walikuwa wanajaribu kuelekea kambi ya karibu inayotumiwa kwa pamoja Marekani na Jeshi la Kenya.

Wakazi wa eneo hilo wamesema walikuwa wanasikia milipuko na baadaye milio ya risasi. Moshi mzito ulionekana katika eneo la tukio.

Uwanja wa Ndege wa Lamu umefungwa kwa muda usiojulikana. **BBC**



Uwanja wa Ndege wa Manda, uliopo Lamu Kusini Mashariki mwa Kenya. **PICHA: BBC**

# Maelfu wamuaga Jenerali Soleimani

**BAGHDAD,** Iraq

MAELFU ya waombelezaji wamekusanyika katika mji mkuu wa Iraq, Baghdad kushiriki maandamano ya mazishi ya kamanda wa jeshi la Iran, Qasem Soleimani.

Jenerali Soleimani (pichani), aliuawa katika shambulio la angani lililotekelezwa na Marekani siku ya Ijumaa.

Kamanda hiyo alikuwa kiungo muhimu katika operesheni ya Iran Mashariki ya Kati, hata hivyo taifa hilo limeapa kulipiza kisasi kwa mauaji yake.

Mkusanyiko huo wa mjini Baghdad ni mwanzo wa siku kadhaa ya maombolezi ya Soleimani.

Pia makundi ya watu mjini humo wanaomboleza kifo cha Abu Mahdi al-Muhandis, mmoja wa kamanda wa Iraq ambaye kundi lake la Kataib Hezbollah, linaungwa mkono na Iran.

Waandamanaji walianza kukusanyika mjini Baghdad mapema jana wakipeperusha bendera ya Iraq na ya waasi wakiimba 'kifo kwa Amerika'.

Watu walizunguka barabara za mji huo wakibeba mabango nyenye picha ya Soleimani, huku wengine wakiwa na picha ya kiongozi mkuu wa kidini wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei.

Ripoti zinasema mwili wa raia huyo wa Iran aliyeuawa katika shambulio hilo, ulisafirishwa nchini mwake jana jioni ambako siku tatu ya maombolezo imetangazwa kwa heshima ya jenerali huyo.



Mazishi yake yatafanyika siku ya Jumanne nyumbani kwake Kerman, eneo la kati la Iran.

Baadhi ya raia wa Iran walisherehekea taarifa za kuuawa kwa Soleimani mjini Baghdad.

Alilaumiwa kwa kupanga ghasia na kuvunja maandamno ya amani ya kupigania demokrasia katika miezi ya hivi karibuni.

Televisheni ya taifa ya Iraq, imetangaza mashambulio mengine ya angani nchini humo saa 24 baada ya kuuawa kwa Soleimani.

Vyanzo vya habari vya jeshi nchini humo vimeliambia shirika la habari la Reuters, kuwa watu sita wameuawa katika shambulio hilo jipya, ambalo lililenga msafara wa waasi wa Iraq jana.

Msemaji wa Jeshi la Muungano linaloongozwa na Marekani, katika eneo hilo amesema hawakuhusika na shambulio hilo.

Marekani imesema kuwa wanajeshi 3,000 wa ziada watapelekwa mashariki ya kati kujibu hatua yoyote ya kulipiza kisasi.

Akizungumza na vyombo vya habari katika mgahawa wa Mar-a-Lago mjini Florida, Rais Donald Trump alisema Jeshi la Marekani katika opereshini stadi ilifanikiwa kumuua gaidi nambari moja duniani, Qassem Soleimani.

"Soleimani alikuwa anapanga kushambulia wanadiplomasia na maofisa wa kijeshi wa Marekani, lakini tulifanikiwa kupata kabla hajatekeleza mpango wake na kumwangamizwa," alisema Trump. **BBC**

## Waliofariki mafuriko wafikia 60

WATU 60 wamefariki dunia kutokana na maporomoko ya udongo na mafuriko yaliyoukumba mji mkuu wa Indonesia, Jakarta na maeneo jirani.

Waokoaji wanaendelea na juhudi za kuwaokoa wale waliofukiwa na kifusi cha tope.

Mvua kubwa za masika zimesababisha mito kufurika na kuathiri wilaya kadhaa za mji wa Jakarta kwa kufunikwa na maji na kutokea maporomoko ya udongo yaliyowafukia watu kadhaa.

Msemaji wa ofisi ya taifa ya kukabiliana na majanga, Agus Wibomo, amesema waliokufa ni pamoja na wale waliozama au kunaswa na umeme wakati kingo za mito zilipopasuka Jumatano iliyopita.

Mafuriko hayo ni mabaya zaidi tangu yale ya mwaka 2007, ambapo watu 80 walikufa katika kipindi cha siku kumi. **DW**

# Vijiji 57 kunufaika na fursa ya umeme

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

VIJIJI 57 vikiwamo 10 utakapopitia mradi mkubwa wa kusafirisha na kupoza umeme wa kutoka Kijiji cha Ibadakuli mkoani Shinyanga hadi mkoani Geita kupitia Mbulyanhulu wenye urefu wa kilometa 180 vitanufaika.

Mbali na vijiji 57 kati yake vijiji 47 vipo mkoani Geita, na mradi huo baada ya kukamilika pia serikali itauuzia

Mgodi wa dhahabu wa Geita megawati 46 hatua itakayoingizia serikali mpato kutokana na uhitaji wa sasa kwa mji wa Geita ambao ni megawati 12.7 wakati umeme utakapokuwa ukipatikana baada ya mradi kukamilika ni megawati 85.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema hayo juzi wakati akizindua mradi wa kusafirisha na kupoza umeme katika mtaa wa Mpovu Kata ya Mtakuja mkoani Geita mradi ambao umelezwa utakuwa mwarobaiani wa matatizo ya uhitaji wa umeme wa muda mrefu mkoani Geita, hivyo kufungua milango ya ujezi wa Tanzania ya viwanda.

Mradi huo utagaharimu Sh. bilioni 53 na vituo vingine vya mradi kama huo 34 vinaendele kujengwa kote nchini, huku miradi mingine 34 inatarajia pia kujengwa kwa lengo la kuhakikisha kila mkoa una kuwa na huduma hiyo ikiwa ni hatua ya kutekeleza kwa vitendo adhima ya kujenga Tanzania ya viwanda.

Mbali na mradi huo kuwa mkombozi, pia imeelezwa utawezesha serikali kupitia Tanesco kuuzia mgodi wa dhahabu wa Geita jumla ya megawati 46 za umeme kwa ajili ya uendeshaji wake kutokana na uhitaji wa sasa wa huduma ya umeme kwa sasa kwa Geita ni megawati 12.7, hivyo kuliingizia Taifa mapato.



Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Stephen Masele, akizungumza na wajumbe wa kamati ya siasa ngazi ya matawi kutoka Chama Cha Mapinduzi CCM Kata ya Chamaguha, na kuwataka washikamane kutumikia wananchi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Homa ya uchaguzi CCM, Chadema

INATOKA UK.8

barua kwa Jeshi la Polisi nchini kuomba ulinzi katika mikutano ya hadhara ili kujiandaa na uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

"Lilitolewa agizo kuwa mikutano ya siasa haitafanyika mpaka mwaka 2020 si mnakumbuka jamani?" Alihoji Msigwa na kuendelea:

"Na huu ndio mwaka 2020 sasa mimi kama Mwenyekiti wa Kanda naagiza kwamba viongozi wote wa kanda hii kuandika barua polisi za kutoa taarifa kwa mujibu wa taratibu tufanye mikutano ya hadhara."

Akizungumza na wanachama wa chama hicho, Msigwa alidai sasa ni wakati wa kujiandaa na uchaguzi mkuu ujao baada ya kile alichodai kuvurugika kwa mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa ambapo chama hicho na vyama vingine vya upinzani vilisusia baada ya kudai kuenguliwa kwa wagombea wao kinyume cha utaratibu, hivyo kutokuwa na wagombea katika uchaguzi huo.

Msigwa alidai pamoja na kutokufanya mikutano hiyo kwa miaka minne kutokana na kuzuiliwa, lakini bado chama hicho kipo imara na kipo tayari kushindana na CCM katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Juni mwaka 2016, Rais John Magufuli alitoa amri ya kuzuia kufanyika kwa mikutano ya kisiasa hadi mwaka 2020, akisema wabunge na madiwani ndio pekee wanaoruhusiwa kufanya mikutano kwenye maeneo waliyochaguliwa.

**WAITARA ATANGAZA KUMNG'OA HECHE**

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, amewatangazia wananchi wa Jimbo la Tarime Vijijini kuwa endapo chama chake kitampa ridhaa atagombea ubunge katika jimbo hilo.

Waitara ambaye kwa sasa ni Mbunge wa Ukonga, alieleza kuwa ni mzaliwa wa Tarime na kuwa huko ni nyumbani kwao.

"Mwaka 2020 mimi ni mmoja ya watia nia Jimbo la Tarime Vijijini, ikitokea chama changu kikanipitisha kuwa mgombea," alisema Waitara ambaye awali alipata ubunge wa jimbo hilo kwa tiketi ya Chadema.

Alipoulizwa Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, kuhusu kauli hiyo ya Waitara, alisema hana sababu ya kumpa umaarufu Naibu Waziri huyo zaidi ya kujielekeza katika mipango yake binafsi.

"Hiyo siyo 'concern' (hainihusu) yangu sina sababu ya kumpa umaarufu ambao hana," alisisitiza Heche.

Waitara alidai kuwa mwaka 2010 alipoamua kugombea kwa mara ya kwanza katika Jimbo la Tarime Vijijini kupitia Chama Cha Mapinduzi hakuwa na fedha na kudai kuwa ilisababisha kushindwa kupewa nafasi na chama hicho.

Alisema jambo hilo ndiyo ilikuwa sababu ya yeye kukihama chama hicho na kwenda Chadema na kupata nafasi ya kugombea ubunge Jimbo la Ukonga mwaka 2015.

"Wakati ule katika Chama Cha Mapinduzi kulikuwa na utaratibu kwamba mwenye pesa ndiye anayepewa nafasi na mimi sikuwa na pesa wala refarii na katika serikali sina shangazi wala mjomba," alisema.

Mwaka 2010 jimbo hilo liliongozwa na Nyambari Nyangwine kutoka Chama Cha Mapinduzi likiwa ni jimbo moja akipokea kutoka kwa marehemu Chacha Wangwe aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, kupitia Chadema na baadaye mwaka 2015 jimbo hilo liligawanya na kuzaliwa majimbo mawili Tarime Mjini na Tarime Vijijini ambayo yote kwa sasa yanashikiliwa na wabunge wa Chadema.

***Imeandikwa na Elisante John, SINGIDA, na Enock Charles, DAR***

# Walalamikia uchakavu miundombinu sokoni

**Na Stevie chindiye,** TUNDURU

WAFANYABIASHARA wa soko kuu la Azimio wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, wamelalamikia uchakavu wa miundombinu ya soko hilo.

Kufuatia hali hiyo, wengi ya wafanyabiashara hao wamedai kuwa wamekuwa wakipata hasara endapo watachelewa kufunika bidhaa zao pindi mvua zinaponyesha.

Walisema mbali na kulalamikia ubovu huo kwa muda mrefu kwa viongozi wa Halmashauri hiyo, lakini wamekuwa hawayafanyii kazi na kufanya kero hiyo kuendelea kudumu kwa muda mrefu na kufanya shughuli zao kwa shida.

Wakifafanua taarifa hiyo kwa niaba ya wafanyabiashara wenzao katika soko hilo, Edgar Nyakunga, Abas Chilumba na Mwenyekiti wa Soko hilo, Mohamed Ngaunje, walisema kinachowashangaza ni namna viongozi hao wanavyotoa majibu ya halmashauri kutokuwa na fedha za kufanya ukarabati huo.

Walisema wakati hao yakiendelea wao hulipa fedha za ushuru, pango la vibanda na ada mbalimbali wanazo watoza sokoni hapo, lakini inapofika kwenye matumizi ya kuboresha miundombinu yao kunakuwa na ugumu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya yaTunduru, Gasper Balyomi, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo, na kwamba tayari amekwisha watuma wataalamu kwenda kufanya uhakiki.

Alisema baada ya kupatiwa taarifa hizo pia amewatuma wafanye tathmini ya kutafuta ghalama ambazo zitatumiwa katika ukarabati wake ili waweze kufanya marekebisho hayo.

Kufutia hali hiyo, Balyomi amewataka wafanyabiashara hao kuwa wavumilivu wakati taratibu hizo zikifanyiwa kazi kwa ajili ya kutafuta suluhisho la kudumu.

**Baada ya kupatiwa taarifa hizo pia amewatuma wafanye tathmini ya kutafuta gharama ambazo zitatumiwa katika ukarabati wake ili waweze kufanya marekebisho hayo.**

# Wakulima korosho walia utitiri makato

**Na Stevie chindiye,** TUNDURU

WAKULIMA wa koroshoa wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wamelalamikia utitiri wa makato wanayo tozwa kipindi cha kuuza mazao yao.

Walitoa malalamiko hayo wakati wakizungumza na wataalamu kutoka Asasi ya TUPACE ambao wamekuwa wakupita katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo ili kutafuta kero za wakulima wakiwamo wa korosho na kuwashirikisha viongozi wa wilaya hiyo kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu.

Walisema kipindi cha kuandaa mashamba, kununua pembejeo, kupulizia, kuokota korosho zao huwa peke yao mashambani, lakini korosho zinapofika sokoni wanakatwa makato ambayo hawajui chanzo chake ni nini.

Walisema uwapo wa makato hayo umekuwa ukiwafanya wapate fedha kidogo na kuwafanya washindwe kutimiza malengo yao.

"Makato tunayokatwa kila tunapo uza korosho zetu kumekuwa kukitufanya tupate Fedha kidogo na kushindwa kutimiza ndoto zetu za kujiimarisha kiuchumi," alisisitiza Abilay Adam, Mkulima wa Kijiji cha Sisi kwa Sisi.

Walisema kutokana na hali hiyo, baadhi ya wakulima wa korosho wamekuwa wakiacha kuhudumia mashamba yao na kufanya kilimo cha zao hilo kufifia.

Katika taarifa hiyo wakulima hao walitolea mafano vyama vilivyopo mjini makato ya kisheria ni Sh. 238.52 kwa kila moja inayo uzwa katika mnada na ghalama za Usafirishaji ni Sh. 36 kwa kila kilo na kwamba gharama zinaongezeka kutokana na umbali ambapo vipo vyama vinavyouza korosho zake kulingana na umbali wa yalipo maghala ya AMCOS za kuleta katika ghala kuu la mnada.

Akizungumzia hali hiyo Mkurugenzi wa Asasi ya TUPACE, John Nginga, alisema kuwa shirika lake lilibuni mbinu hiyo baada ya kubaini kuwapo kwa changamoto na kero mbalimbali kutoka kwa wakulima wakiwamo wa zao la korosho.

Alisema baada ya kuziibua kutoka kwa wakulima shirika lake huwahusisha wataalamu na viongozi ndani ya wilaya hiyo na kushirikiana katika kuzitafutia ufumbuzi.

Kaimu Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Tunduru, Method Pilli, alisema kuwa makato ya kuendeleza zao kupitia Chuo cha Utafiti Naliendendele Sh. 300 na makato ya usajili wa mkulima hivi sasa ni bure.

Alisema makato mengine yaliyopitishwa kisheria kwa ajli ya kusaidia maendeleo ya elimu wilaya na michango ya elimu itaendelea.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo (katikati), akizungumza na wananchi wa Kata ya Chalangwa wilayani Chunya katika Kituo cha Afya cha Kata hiyo, alipokuwa ziarani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Polisi yataja mwarobaini wa migogoro ya kifamilia

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

KATIKA kukabiliana na matukio ya watu kujichukulia sheria mkononi, Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga limeitaka jamii kutumia viongozi wa serikali za mitaa na vijiji na taasisi za dini katika kutatua migogoro mbalimbali ikiwa ni pamoja na ile ya kifamilia.

Kauli hiyo imetolewa jana na Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Deborah Magiligimba, wakati akizungumza na Nipashe, ikiwa ni siku chache baada askari Polisi mwenye Namba H, 8980 Pc Kazimiri kujeruhiwa sehemu za siri na mke wake kutokana na mgogoro wa ndoa.

Alisema matukio mengi ya kujichukulia sheria mkononi yamekuwa yakisababishwa na ugomvi wa kifamilia, na kwamba viongozi wa serikali wakiwamo wa madhehebu ya dini wana nafasi kubwa katika kutatua migogoro hiyo.

Kamanda Magiligimba alisema wanandoa wamekuwa na desturi ya kukaa na migogoro bila kuwashirikisha watu wao wa karibu, jambo ambalo ni hatari katika maisha yao kwani anaweza kusababisha maafa kwa watu kujichukulia sheria mkoani.

Katika hatua nyingine, Kamanda Magiligimba, alisema katika kipindi cha sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya hakuna matukio makubwa ya uhalifu yaliyoripotiwa, na kwamba Jeshi la Polisi lilikuwa limeimarisha ulinzi wa raia na mali zao pamoja na usalama barabarani.

Aidha, Kamanda Magiligimba alisema kuwa katika mwaka 2020, Jeshi la Polisi mkoani humo limejipanga kikamilifu kutokomeza matukio ya uhalifu na wahalifu kwa kuimarisha doria na ushirikishwaji wa wananchi na kuwataka wananchi wazidi kuwa karibu na Jeshi la Polisi.

Nao baadhi ya wananchi wilayani hapa walisema kuwa wanandoa wengi wanashindwa kuwashirikisha viongozi wa serikali na dini ili kuficha siri ya migogoro yao, hali ambayo inasababisha migogoro kuwa mikubwa, na kwamba elimu izidi kutolewa kwa jamii ili kuwa na uelewa huo.

# Watumiaji maji sasa kufungiwa mita za Luku

**Na Dege Masoli, TANGA**

UFUNGAJI mita za Luku kwa wananchi na kwenye taasisi za serikali utaondoa mzigo wa madeni kwenye taasisi hizo na kuondoa kero zilizopo za utoaji wa huduma hizo kwa wateja.

Ofisa Huduma kwa Wateja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga-Uwasa), Devota Mayala, alisema hayo wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Mwanzange, jijini hapa kwenye kazi ya uelimishaji kuhusu huduma zao.

Mayala alisema ufungaji wa mita za Luku kwa wananchi na kwenye baadhi ya taasisi za serikali kutasaidia kupunguza madeni na kuondoa kero.

Siwaeleza wananchi hao kuwa elimu hiyo inahusiana na matumizi sahihi ya maji ili waweze kuondokana na malalamiko ya kuletewa bili kubwa.

Alisema lengo la kutolewa kwa elimu hiyo ni kutaka kupunguza madeni na kuondoa kero kwa wananchi wanaodai kubambikiwa bili kubwa hivyo uwapo wa mfumo huo, utawezesha kulipia huduma hiyo kabla ya kulipia.

Alisema kwa sasa luku hizo zimefungwa katika taasisi kubwa za serikali na wateja ambao ni wadaiwa sugu na bado wapo kwenye majaribio na kuangalia jinsi zinavyofanya kazi na changamoto zake.

Awali, akizungumza wakati wa uelimishaji, Ofisa Ankra Msaidizi wa Tanga-Uwasa, Ausi Anthony, alisema mita hizo zimeanza kufungwa kwa taasisi kubwa na zina gharama kidogo na kwa wateja binafsi wanafungiwa bure.

Mkazi wa Mwanzange, jijini hapa, Mashaka Shabani, alisema ufungaji wa mita hizo utakuwa mkombozi kwao kwa kuwa utawasaidia kutumia maji kwa uangalifu mkubwa ambao utakuwa chachu.

Alisema mfumo huo utakuwa kama wanavyofanya kwenye Luku ya umeme.

Mkazi wa Mwanzage, Beatrice Benjamin, alisema bili inaweza kuja kubwa mtu akashindwa kulipia kutokana na kukosa fedha, lakini uwapo wa mfumo wa mita za Luku utawawezesha kuwa makini na kujiandaa na malipo muda wowote.

# CUCURELLA AKANUSHA KUMUITA MILITAO NYANI




**MADRID,** Hispania

BEKI wa Getafe, Marc Cucurella amekanusha madai ya kumtolea maneno ya kibaguzi nyota wa Real Madrid, Eder Militao wakati wa mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, uliochezwa juzi Jumamosi.

Wawili hao walionekana kubwatukiana katika kipindi cha pili wakati Madrid wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0 kwenye mchezo huo uliopigwa kwenye Uwanja wa Coliseum Alfonso Perez.

Ilidaiwa kwenye vyombo vya habari kwamba, Cucurella, ambaye amejiunga na Getafe kwa mkopo wa muda mrefu akitokea Barcelona Julai mwaka jana, alimuita Militao kwa jina la 'mico', ambalo lina maana ya nyani kule Katalunya.

Cucurella alisema alitumia neno la kihispania la 'mico', ambalo mdomoni alionekana ametamka tofauti.

"Napenda kufafanua kwamba, sikumtukana Militao. Maneno yangu yalikuwa ni 'funga mdomo wako'," aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter.

"Naomba radhi kwa yoyote aliyekwazika na hili. Hiyo ndio sentesi pekee niliyotamka mdomoni mwangu. Asanteni."



# Zidane: Madrid inawafungaji wengi

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane anaamini uwezo wa Raphael Varane kufunga mabao mawili kwenye ushindi wa 3-0 dhidi ya Getafe umeonyesha jinsi gani Real Madrid hawategemi fowadi tu kufunga mbao.

Los Blancos walirudi kwenye ligi wakiwa wamefunga mara moja katika mechi zao tatu zilizopita kwenye ligi, lakini mchezaji wa kimataifa wa Ufaransa, Varane alifunga mabao mawili dhidi ya vijana hao wa kocha, Jose Bordalas.

Luka Modric alifunga la tatu na kuipa ushindi huo mkubwa zaidi tangu Novemba 9, mwaka jana na Zidane alisema kikosi chake kilitulia na kuweza kupata ushindi huo.

"Nilishasema kwamba, tunatakiwa kutulia mbele ya goli," alisema kocha huyo wa Madrid akiwaambia waandishi wa habari.

"Unatakiwa kutulia kwa sababu wakati mwingine mchezo unakuwa mgumu. Na mabao ya leo kutoka kwa Varane, inaonyesha jinsi gani Madrid wana vyanzo vingi vya kufunga.

"Kwa upande wetu, ni muhimu kushinda kwa sababu ulikuwa mchezo mgumu wa ligi. Vijana walicheza kwa kujituma tangu dakika ya kwanza na walionyesha nguvu kubwa."

Zidane pia alimsifia golikipa wake, Thibaut Courtois, ambaye alicheza mchezo wake wa tatu mfululizo bila kuruhusu bao na kusema kwamba, alikuwa kwenye kiwango bora.

# Cavani, Paredes kubaki PSG

**PARIS,** Ujerumani

THOMAS Tuchel anatarajia Edinson Cavani na Leandro Paredes watabakia katika klabu ya Paris Saint-Germain wakati huu wa dirisha dogo la usajili.

Mfungaji wa wakati wote wa PSG, Cavani amekuwa na wakati mgumu wa kupata namba kikosi cha kwanza, baada ya kumsajili wa mkopo Mauro Icardi.

Mchezaji wa kimataifa wa Argentina, Paredes pia ameripotiwa kutaka kuondoka baada ya kuanza kwenye mechi nane tu katika mashindano yote msimu huu, lakini Tuchel ameonyesha imani kwa wachezaji wote wawili.

"Paredes alicheza mwishoni mwa mwaka," alisema. "Alionyesha uwezo mkubwa na kuwa mchezaji muhimu kwenye mchezo wetu.

"Na kwa Edinson, nilishasema hapo kabla – ilikuwa ni ngumu kumpa nafasi wakati akiwa ametoka majeruhi kwa sababu hakuwa fiti bado.

"Lakini yupo hapa akiwa fiti na kila mmoja anajiandaa kuwa kwenye ubora wake wakati wowote anapohitajika.

"Nawaamini wao na nafikiri watabakia na sisi. Sio muhimu kufikiria kitu kingine chochote."

Nyota wa Juventus, Mattia De Sciglio na Emre Can wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kutua pale Parc des Princes, lakini Tuchel bado hajafikiri kuhusu usajili mpya.

"Chochote kinaweza kutokea, lakini sijaomba chochote hadi sasa," alisema. "Naipenda timu yangu na wachezaji wangu. Napenda kufanya nao kazi na tuna uhusiano mzuri."



HABARI MICHEZO

# Oblak ni kipa bora duniani – Simeone

**MADRID,** Hispania

JAN Oblak ni golikipa bora duniani na Atletico Madrid wanatakiwa kumshukuru baada ya kuwasaidia kupata ushindi wa 2-1 dhidi ya Levante Jumamosi, kocha Diego Simeone, amesema.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Slovenia, Oblak, alionyesha ubora wake wakati alipookoa mpira wa kichwa uliopigwa na Enis Bardhi dakika ya 93 kwenye mchezo huo uliopigwa dimba la Wanda Metropolitano.

Kipa huyo ameokoa mashuti 14 kati ya 17 kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, yakiwamo mawili dhidi ya Levante.

Atletico sasa imeshinda mechi nne zilizopita kwenye mashindano yote na Simeone alimsifia Oblak.

"Kwa upande wetu yeye ni golikipa bora duniani. Ni mmoja kati ya manahodha wetu. Kwa uhakika kabisa yeye ni golikipa bora duniani," alisema Simeone.

"Anatupa uwezekano wa kushinda mechi ambazo zilionekana kwamba tungeweza kushindwa.

"Vichwa vya habari ni Oblak ameiokoa Atletico, lakini tungeweza kuokolewa kama tungetumia nafasi yetu mapema.

"Siamui nani anashinda tuzo. Sio poa kuzungumza kuhusu magolikipa wengine, lakini ni wazi kwamba yeye ni golikipa bora duniani."



# GUARDIOLA KUTOWAPA NAFASI VIJANA



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema hawezi kuwapa nafasi ya moja kwa moja "wakati huu" wachezaji wake vijana kutoka kwenye akademi ya Manchester City, lakini anaamini Taylor Harwood-Bellis na Phil Foden wanaweza kuwa na mchango kwenye kikosi cha kwanza.

Harwood-Bellis mwenye umri wa miaka 17 na Foden mwenye miaka 19, walianza na kufunga katika ushindi wa magoli 4-1 kwenye Kombe la FA dhidi ya Port Vale Jumamosi, huku Tommy Doyle mwenye umri wa miaka 18 alitokea benchi.

Foden amepewa nafasi zaidi kuliko wachezaji wenzake vijana, akiwa ameanza kwenye Ligi Kuu, lakini Guardiola amewashauri wachezaji hao kujituma zaidi ili kupata nafasi ya kucheza.

"Bila shaka ni muhimu kuwa na wachezaji vijana kutoka kwenye akademi yetu kama Taylor na Phil - na Tommy," alisema Guardiola. "(Doyle) alicheza mwezi uliopita kwenye Kombe la Carabao na alicheza dakika chache leo (juzi).

"Sio kwa sababu wao ni Waingereza - tunaamini wanaweza kufanya vizuri kwa sababu ni wachezaji wazuri. Hatuwapi nafasi wakati huu. Wanatakiwa kuzitafuta wao wenyewe.

"Katika mechi hizi, kuna nafasi kwa kila mmoja. Lakini kutokana na kile tulichokiona hadi sasa, wana ubora wa kutusaidia.

"Wachezaji vijana hawatakiwa kuzungumza sana, wanatakiwa kujifunza na kusikiliza na kujifunza zaidi. Wanatakiwa kujifunza.

"Dakika ni nzuri zaidi kwa maendeleo yao, na majaliwa yao ya baadaye yapo mikoni mwao. Kitu muhimu kwao ni kuhakikisha wanapata dakika nyingi za kucheza kwenye timu yao."

# Barca yalalamikia kadi ya De Jong

**BARCELONA,** Hispania

ERNESTO Valverde amesema kwamba, kutolewa nje kwa kadi nyekundu kwa Frenkie de Jong kuliiumiza Barcelona wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 kwenye 'dabi' ya Katalunya dhidi ya Espanyol na kubainisha kikosi chake kilikabiliwa na wakati mgumu.

Blaugrana walitoka nyuma ya bao moja kwenye Uwanja wa RCDE na kuongoza kwa 2-1 shukrani kwa mabao ya Luis Suarez na Arturo Vidal, lakini De Jong alionyeshwa kadi ya pili ya njano dakika 15 kabla ya mchezo kumalizika.

Hiyo ilikuwa ni kadi ya kwanza nyekundu kwa kiungo huyo katika maisha yake ya soka na Espanyol ilipigana na kuweza kupata sare baada ya Wu Lei kufunga la kusawazisha na kuwawezesha kupata pointi moja kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Valverde, ambaye kikosi chake kimeshinda mechi moja kati ya nne zilizopita, alikitaka kikosi chake kupambana ili kupata ushindi.

"Tunatakiwa kupambana katika kila mechi," alisema Valverde akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulianza vibaya, tuliweza kurudi mchezoni, lakini bahati mbaya tukabakiwa na wachezaji 10 na wakasawazisha.

"Kutolewa kwa Frenkie kulituathiri. Hatukuwa na uwezo wa kufunga la tatu. Huu ndio mchezo wa soka.

"Ulikuwa mchezo wenye ushindani mkubwa, dabi yenye umakini mkubwa. Kama ukishinda na kusawazisha, unaacha nafasi kwa kupoteza pointi mbili."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER AFIKIRIA KUMSAJILI JIMENEZ

## Amemtaja nyota huyo ni mshambuliaji mzuri, anaweza kuongeza nguvu katika safu...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ameshindwa kuondoa uwezekano wa kumsajili nyota wa Wolves, Raul Jimenez baada ya mchezo wa Kombe la FA, juzi Jumamosi.

**Baada ya Erling Haaland kuamua kujiunga na Borussia Dortmund, United imekuwa ikihusishwa na mshambuliaji huyo wa Wolves, Jimenez wakati huu wakiangalia uwezekano wa kuimarisha safu yao ya ushambuliaji.**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Mexico, Jimenez amefunga mabao nane kwenye Ligi Kuu England msimu huu katika mechi 17 alizoichezea Wolves kwenye mashindano yote.

Alipoulizwa kuhusu Jimenez baada ya kutoka sare ya kutofunga na Wolves, Solskjaer aliwaambia waandishi wa habari: "Mchezaji mwingine mzuri ambaye tumekuwa tukihusishwa nae.

"Ni wachezaji wengi ambao tumekuwa tukuhishwa nao sisi. Niliona aliingia na alifanya vizuri leo (juzi). Lakini siwezi kuzungumzia kuhusu uvumi."

Kocha wa Wolves, Nuno Espirito Santo pia aliulizwa kuhusu uvumi huo na alisema: "Ni mara ya kwanza nasikia hilo. Ole (Gunnar Solskjaer) hajazungumza chochote kuhusu hilo.

"Lakini dirisha la usajili lipo wazi kwa sasa. Likishafunguliwa kitu chochote kinaweza kutokea. Hata hivyo, tunajisikia fahari kuwa na Paul."

Pia majaliwa ya nyota wa United, Paul Pogba yametawala vichwa vya habari, wakati huu ambapo dirisha la usajili la Januari likiwa limefunguliwa.

Huku akiwa majeruhi baada ya kuumia enka, Pogba amekuwa akihusishwa na klabu za Juventus, Inter na miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid.

Hata hivyo, Solskjaer ameiambia BBC: "Hamtashuhudia Paul (Pogba) akiondoka Januari hii."

## ZISIKUPITE

### EMERSON AKARIBIA JUVE

JUVENTUS imeanza mawasiliano na wawakilishi wa beki wa kushoto wa Chelsea ili kujadili uwezekano wa kumsajili Mbrazili, Emerson, ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Calciomercato)***

### UNITED KUMTOA LINGARD

MANCHESTER United imesema iko tayari kumtoa kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard (27), ili kufanikisha mchakato wa kumsajili nyota wa Leicester City, James Maddison (23), kwa dau la pauni milioni 45. ***(Sunday Mirror)***

### CITY, WEST HAM VITANI

WEST Ham United itajaribu kupambana na Manchester City kuwania saini ya beki wa Napoli, Kalidou Koulibaly, ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Sunday Express)***

### WEST HAM, BENFICA KUTETA

MABOSI wa West Ham United maarufu The Hammers wanatarajia kukutana na viongozi wa Benfica ili kujadili kuhusu nia ya kumsajili kwa mkopo, Gedson Fernandes, 20. ***(Record, via Daily Star Sunday)***

### MILAN YAMTAKA ERIKSEN

INTER Milan imeweka wazi nia yake ya kumsajili kiungo wa Tottenham Hotspur, Christian Eriksen kwa dau la pauni milioni 20, licha ya nyota huyo wa Denmark mwenye umri wa miaka 27 kuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu. ***(Sun on Sunday)***

### MARTINEZ ANUKIA UNITED

MANCHESTER United wamemweleza Kocha Antonio Conte kuwa wanamhitaji straika wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lautaro Martinez (22), kabla ya kumruhusu kiungo wao Mfaransa, Paul Pogba (26), kuhamia San Siro. ***(Sunday Mirror)***

### ANCELOTTI AMTAKA RODRIGUEZ

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, anataka kumsajili kiungo mchezeshaji wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez (28), kutua Goodison Park kwa mkopo. ***(Sunday Mirror)***

### TOSUN ANUKIA PALACE

KLABU ya Crystal Palace imeweka wazi nia ya kumsajili straika wa Everton na Timu ya Taifa ya Uturuki, Cenk Tosun, ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Mail on Sunday)***

### MUSTAFI SAFARI IMEIVA

BEKI wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Shkodran Mustafi, ambaye ana umri wa miaka 27, anatarajia kuondoka katika klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England mwishoni mwa mwezi huu. ***(Sunday Mirror)***

### DEMIRAL ATAJWA LEICESTER

KOCHA wa Leicester, Brendan Rodgers, amekataa kuthibitisha au kukubali taarifa za klabu yake kuanza mchakato wa kumsajili beki wa Juventus na Timu ya Taifa ya Uturuki, Merih Demiral (21). ***(Mail on Sunday)***

### SPURS YAMWANIA PARROTT

MABOSI wa Tottenham wanaamini kuwa straika wa Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Ireland, Troy Parrott (17), atakubali kusaini mkataba mpya wa muda mrefu na klabu hiyo ifikapo mwezi ujao. ***(Evening Standard)***

## HABARI MICHEZO

## JKT yajipanga kusajili wapya

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Abdallah Mohammed 'Bares' (pichani chini), amesema kuwa uongozi wa timu hiyo umeanza mchakato wa kusajili mchezaji mpya atakayeziba nafasi ya beki, Adeyum Saleh, ambaye amejiunga na Yanga katika kipindi hiki cha dirisha dogo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Bares, alisema kuwa anaamini usajili atakaofanya katika dirisha dogo, utasaidia kuimarisha kikosi chake ili kitimize malengo waliyoweka katika msimu huu.

Bares alisema kuwa ameshabaini makosa ambayo timu hiyo ilifanya katika mechi zilizopita na sasa ni wakati wa kurekebisha upungufu ili watakapoanza mzunguko wa pili wawe imara.

"Hatuna majeruhi, tunaamini tutajipanga zaidi, ili kutimiza malengo yetu, bado tuko mahali pazuri, lakini hatutabweteka, ligi ni ngumu na ina ushindani mkubwa," alisema Bares.

Kocha huyo aliongeza kuwa anaushukuru uongozi wa JKT Tanzania kwa kumpa ushirikiano mzuri na yeye pamoja na benchi la ufundi, wanaahidi watapambana kuhakikisha wanamaliza kwenye nafasi za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Bara msimu huu.



## Singo kufungua tenisi Afrika leo

**Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Maendeleo ya Michezo Tanzania, Yusuph Singo, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa mashindano ya tenisi ya vijana barani Afrika yanayotarajiwa kuanza leo kwenye Viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam.

Mashindano hayo yanayoshirikisha timu nane yatafanyika kuanzia 3:00 asubuhi na maandalizi yake yamekamilika.

Mwenyekiti wa Chama cha Tenisi Tanzania (TTA), Denis Makoi alisema mashindano hayo ni ya kalenda ya mwaka ya Shirikisho la Kimataifa la mchezo huo (ITF) na lile la Afrika (CAT).

Makoi alisema. "Tayari wachezaji kutoka nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Somalia, Comoro, Shelisheli na Eritrea wamewasili, wataungana na wenyeji Tanzania kusaka bingwa wa michuano hiyo," alisema Makoi.

Alizitaja nchi za Sudan, Djibouti na Ethiopia zimejitoa kushiriki mashindano hayo ya mwaka huu.

Kiongozi huyo alisema kuwa kikosi cha Tanzania kimeandaliwa kwa kiwango bora kwa lengo la kubakisha ubingwa wa michuano hiyo.

# AZAM WATAMBA KUTETEA UBINGWA MAPINDUZI CUP

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Azam inatarajia kuanza kampeni ya kutetea ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa kuvaana na Mlandege katika mechi ya Kundi A itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, alisema kuwa kikosi chake kimejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na anaamini wataanza vema kampeni ya kutetea kombe hilo wanalolishikilia.**

Cheche alisema kuwa kikosi chake kimeimarika na hiyo inatokana na kiwango kizuri walichokionyesha kwenye mechi mbili zilizopita za Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tumejiandaa vizuri na tunaamini tutafanya vema, tunajua michuano hii ni migumu kwa sababu tunakutana na timu zinazoshiriki ligi nyingine, lakini wachezaji wangu ni wazoefu na wamejipanga kuhakikisha wanarudi na ubingwa," alisema Cheche.

Katibu wa Kamati ya Kombe la Mapinduzi, Khamis Said, alisema maandalizi yamekamilika na wanatarajia kuwa na mashindano yenye ushindani.

Said alisema kuwa timu kutoka nje ya Zanzibar zinazoshiriki michuano hiyo, zilitarajiwa zote kuwasili visiwani hapa hadi jana jioni, tayari kuanza kampeni ya kuwania kitita cha Sh. milioni 15.

"Maandalizi yamekamilika hapa Unguja, lakini hali hii ipo katika kituo cha Kisiwani Pemba, tayari kamati imeshaandaa mazingira mazuri ya kufikia timu na mahitaji yote muhimu," alisema Said.

Aliwataka mashabiki kufika uwanjani kwa wingi kuangalia michuano hiyo ambayo idadi ya mechi zitakazochezwa mwaka huu zimepungua, kutokana na kucheza kwa mtindo wa mtoano.

Mechi nyingine ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba itakuwa ni kati ya wenyeji Chipukizi dhidi ya Mtibwa Sugar wakati kesho Simba itavaana na Zimamoto huku Yanga wakiwakabili Jamhuri.



Wachezaji wa Simba kutoka kushoto, Meddie Kagere, Deo Kanda na Muzamiru Yassin, wakishangilia bao la pili katika mechi ya Ligi Kuu dhidi ya watani zao Yanga iliyochezwa juzi. Timu hizo zilitoka sare ya 2-2. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Taifa Jang'ombe kusajili nyota sita*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Timu ya Taifa Jang'ombe inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, umesema unatarajia kusajili wachezaji wapya sita ili kuimarisha kikosi chao katika kipindi cha dirisha dogo ambalo litafungwa rasmi Ahamisi wiki hii, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Mohamed Ali, alisema wachezaji hao watakaosajiliwa watakuwa wenye viwango vya juu kwa sababu wanahitaji kuona wanapanda daraja na kucheza Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

Ali alisema pia timu hiyo imepanga kuacha wachezaji sita ambao wameshindwa kuendana na kasi ya timu hiyo tangu kuanza kwa msimu huu.

"Tutasajili wachezaji sita na tutaacha wachezaji sita, nyota wanaochwa sio kama hawana viwango, lakini tunataka kusajili wachezaji ambao wataipandisha daraja timu na kucheza Ligi Kuu msimu ujao," alisema Ali.

Hata hivyo, kocha huyo hakuweka wazi majina ya wachezaji watakaoachwa katika kikosi hicho ambacho kilianza vizuri msimu huu, lakini wakapata matokeo ya sare mfululizo kabla ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.

Taifa Jang'ombe yenye pointi 21, iko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja yenye kushirikisha klabu 13.

# Michezo

Jumatatu Januari 6, 2020

Nipashe




Solskjaer afikiria kumsajili Jimenez HABARI UK.30



Beki wa Simba, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' (kushoto), akiwania mpira dhidi ya winga wa Yanga, Deus Kaseke katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mkwasa: Tutafika tunapopataka

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, amesema mashabiki wa timu hiyo watarajie kuona mambo mazuri baada ya wachezaji walioongezwa katika dirisha dogo la usajili kuzoeana na wenzao.



Mkwasa alisema kuwa anatarajia kuona kikosi hicho kikiwa imara zaidi ndani ya muda mfupi na dalili zimeonekana baada ya kuonyesha kiwango kwenye mechi dhidi ya watani zao Simba hapo juzi.

"Wenzetu wamekaa muda mrefu wako pamoja, wanacheza kitimu, lakini sisi pia tunajenga timu yetu, nilikuwa na wakati mgumu baada ya kufungwa magoli mawili, ilikuwa mechi ngumu na yenye burudani, ni moja kati ya mechi bora za Simba na Yanga, nadhani watu wote waliokuwa wamefurahi," alisema Mkwasa.

Kocha huyo aliongeza kuwa anaamini kikosi chake kitaendeleza 'moto' huo katika mechi nyingine za Ligi Kuu Tanzania Bara zitakazofuata baada ya wachezaji wake kuzoeana zaidi.

Alisema usajili wa dirisha dogo walioufanya umelenga zaidi kuimarisha kikosi hicho ambacho jana kilielekea Zanzibar kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yanatarajiwa kuanza leo kwa kushirikisha timu nane za hapa nchini.

Yanga itaanza kampeni ya kuwania kombe hilo kesho kwa kucheza dhidi ya Jamhuri wakati Zimamoto itawakaribisha Simba kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba.

# Simba yaumia, Yanga kicheko

**Na Somoe Ng'itu**

## ●●● Ni baada ya matokeo ya sare ya 2-2 katika mchezo wao wa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Bara...

BAADA ya mechi ya watani wa jadi nchini iliyochezwa juzi kumalizika kwa sare ya mabao 2-2, upande wa mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ndio umeonekana kuwa na 'machungu' zaidi ukilinganisha na Yanga ambayo imefurahia matokeo hayo ya kugawana pointi.

**Kwa matokeo hayo, Simba imeendelea kujiimarisha kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 35 baada ya kucheza mechi 14, wakati Yanga yenye michezo miwili pungufu imefikisha pointi 25 na kusalia kwenye nafasi nne kwenye msimamo.**

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, alisema kuumia kwa wachezaji wake na watani zao Yanga kupata mabao ya haraka ya kusawazisha kuliwaondoa nyota wake 'mchezoni'.

Sven alisema walicheza katika kiwango kizuri hasa kipindi cha kwanza, lakini wapinzani walikuwa vizuri zaidi katika safu ya kiungo.

"Nilikuwa na wachezaji wawili majeruhi, na wao walipata nafasi ya kusawazisha mabao yote mawili, kama tungekuwa 11 wasingeweza kufunga, walicheza na viungo wengi lakini sisi (Simba), tulitawala mchezo, kwa kifupi nimeridhishwa na namna wachezaji wake walivyocheza, lakini si matokeo waliyopata," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Kocha huyo aliongeza kuwa baada ya Yanga kusawazisha mabao yote mawili ndani ya dakika tatu, timu yake ilipoteza mwelekezo, lakini ilizinduka dakika 20 za mwisho ambazo Yanga walijitahidi kuwabana na kutoruhusu bao lingine.

Kufuatia matokeo hayo, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, amesema kuwa wachezaji wa timu hiyo hawatimu kama walivyo wapinzani wao licha ya kulipwa kwa wakati na kupewa huduma muhimu na za kiwango cha juu.

Manara alisema kuwa wachezaji wa Simba wanatakiwa kubadilika na kujua thamani ya jezi hiyo na heshima wanayopata kutoka kwa mashabiki wao.

"Kweli mpira una matokeo matatu, ila kwa jana (juzi), bila kupepesa macho ile sare haikustahili kwa ukubwa wa Simba, mmewaangusha sana mashabiki wetu ambao kila siku wanakuja kuwapa nguvu, bodi yetu makini mmeiangusha, viongozi wenu tumelowa, na mnampa wakati mgumu tajiri (Mohammed Dewji), anayeweka fedha zake, kwa kifupi mmetuudhi, ukweli mchungu," alisema Manara.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, alisema kikosi chake kilikuwa na wakati mgumu baada ya kuwa nyuma kwa mabao 2-0, lakini juhudi za wachezaji wake zilibadilisha matokeo hayo.

Mkwasa alisema kuwa penalti ambayo Simba walipata ilichangia wao kucheza chini ya kiwango, lakini baadaye waliimarika na hatimaye kurejea mchezoni.

Aliongeza kuwa baada ya kusawazisha, wachezaji wake walitawala mchezo huo na kama muda ungeongezeka zaidi, walikuwa na uwezo wa kufunga bao la tatu.

Vigogo hao wa soka nchini waliondoka jijini Dar es Salaam jana mchana na kuelekea kushiriki katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi, na endapo timu hizo zitafanya vema, watakutana tena kwenye mchezo wa fainali ya michuano hiyo itakayochezwa Januari 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Amaan.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >